Nipashe
Ijumaa Mei 17, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579920
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Serikali yaeleza sababu ya kuvunja mkataba korosho

UKURASA 2





DRC: Mji wa Kisangani wakabiliwa na mgawo wa umeme

Ukurasa 20

BUFE

Ijumaa Mei 17, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Mjasiriamali aliyeajiriwa afunguka neema kuwepo vitambulisho vipya

UDSM YAWEKEZA BIL 1/- KWENYE UTAFITI

Pinda awaambia kioo cha taaluma yao, fimbo inayokomboa mipango uchumi

Na Salome Kitomari

KATIKA taasisi ya elimu ya juu yoyote, sifa na wajibu wake mkuu ni uwezo wake katika kufundisha, kutafiti na kuishauri kitaaluma. Wasifu wa wataalumu wake, pia wanaofunzwa unapimwa katika vigezo vya ubora katika eneo hilo. Katika eneo la utafiti, kunajulikana kuwa nyenzo muhimu katika kutatua matatizo ya jamii husika au ile itakayoomba kuhudumiwa. Hicho inakifanya kuwa moja ya kipimo chenye upekee katika kutathmini chuo chochote cha elimu ya juu; namna wanafanya tafiti, kuzichapisha na matatizo ya jamii duniani kote, ikiwemo maendeleo ya nchi husika. Ni jambo linaofanya sifa ya taaluma wake ni kufanya utafiti na kuchapisha kwenye machapisho ya ndani na nje ya nchi, hasa katika majarida ya kitaaluma. Ndivyo vigezo pia vinavyopandisha hadhi ya chuo husika.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

Habari katika picha

Ukurasa 17

UKURASA 13

# Mbunge amgomea Spika Ndugai



• **Aitwa** kuhojiwa na kamati za maadili za Bunge na CCM, uwakilishi wake Afrika wasitishwa, Chadema wamtetea...*Uk.2*



Wakazi wa Kijiji cha Masebe, Kata ya Mwaya, wilayani Kyela, Mkoa wa Mbeya, wakitengeneza daraja la mianzi kwa ajili ya o **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Taarifa ya hesabu za Ofisi CAG rasmi bungeni

UKURASA 3

## Mafuriko yaua watano, mamia wakosa makazi

UK.21

**MICHEZO** **YANGA KUTWAA UBINGWA HIVI** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# 75 wabainika kuwa na dengue kila siku nchini

**Na Mary Geofrey**

WATU 75 wanabainika kila siku kuwa na virusi vya homa ya dengue, hivyo idadi ya wagonjwa kuongezeka kufika 1,901, tangu ulipoingia nchini, Januari mwaka huu.

Kati ya wagonjwa hao, 1,809 ni wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, 89 kutoka Tanga mmoja (Singida), mmoja Kilimanjaro na mmoja (Pwani).

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Mohammed Kambi, aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya ugonjwa huo nchini.

"Katika kipindi cha siku tisa ambazo wizara ilikuwa ikikusanya mwenendo wa hali ya ugonjwa huu nchini, kuna ongezeko la wagonjwa 674 sawa wastani wa wagonjwa 75 kwa kila siku, ikiwa ni tofauti ya wastani wa wagonjwa 32 waliopatikana kila siku kwa mwezi ulipita," alisema Prof. Kambi.

Alisema ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa uelewa, kuhusu ugonjwa huo kwa wananchi wengi wenye dalili, hivyo wanajitokeza kupata huduma za uchunguzi ambazo zimeendelea kupanuka kwenye vituo vya afya katika mikoa ya Dar es Salaam na Tanga.

Prof. Kambi alisema miongoni mwa wagonjwa hao mmoja kutoka Kilimanjaro na mwingine Mkoa wa Pwani, walitoka na virusi hivyo jijini Dar es Salaam.

Aidha, alisema idadi ya vituo vinavyopima ugonjwa huo imeongezeka hadi 19 tofauti na vituo saba vilivyokuwapo awali ili kutoa fursa kwa wananchi kupata huduma.

"Ugonjwa huu unapimwa kwenye vituo vyetu vya serikali na tunaendelea kuimarisha upatikanaji wa vipimo vya ugonjwa huu bure, na niwatake watoa huduma za afya wote na wananchi watambue kuwa si kila homa ni dengue, chunguza au chunguzwa maradhi mengine na wataalamu kwenye vituo vyetu vya huduma kwanza kabla ya kupima," alisema Prof. Kambi.

Alitaja vipimo vinavyopima ugonjwa huo ni Hospitali ya Taifa, Muhimbili, Maabara kuu Muhimbili, Amana, Temeke, Mwananyamala, Sinza, Vijibweni, Mnazi Mmoja, Lugalo, Mbagala na FFU Ukonga jijini Dar es Salaam.

Vingine ni Bombo na Horohoro katika mkoa wa Tanga; Hospitali ya Tumbi, Mkuranga, Utete Rufiji na Mafia, Morogoro na Manyara.

"Aidha, natambua vipo pia vituo binafsi vinavyotoa huduma za upimaji. Katika mikoa mingine

INAENDELEA UK. 8

# Mbunge CCM kuhojiwa Kamati ya Maadili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesitisha uwakilishi wa Mbunge wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele (CCM), katika Bunge la Afrika (PAP) kutokana na tuhuma za utovu wa nidhamu.

Masele ambaye katika serikali ya awamu ya nne alikuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini na baadaye Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa sasa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa PAP.

Kutokana na uamuzi huo wa Spika Ndugai, Masele ambaye kwa sasa yuko Afrika Kusini kwenye vikao vya PAP, ametakiwa kurejea nchini ili kuhojiwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge huku akidokeza kuwa hata Kamati ya Maadili ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) nayo itamhoji.

Akitoa taarifa jana bungeni, Ndugai alisema katika uwakilishi wa Masele kwenye Bunge hilo la Afrika, kumejitokeza matatizo makubwa ya kinidhamu.

"Nisingependa kuyafafanua leo (jana) muda hautoshi. Tumelazimika kumtafuta Masele kumrudisha nyumbani kuanzia Jumatatu, badala yake amekuwa akionyesha kugoma. Hata jana (juzi) kwenye Bunge hilo tumeona 'clips' zilionyesha akihutubia Bunge hilo japo ameitwa na Spika.

"Baada ya kumwandikia arudi nyumbani, aje ahudhurie kwenye Kamati ya Maadili, akahutubia Bunge akisema japo ameitwa na Spika, ameambiwa na Waziri Mkuu akaidi wito wa Spika, aendelee na mambo yake kule, kitu ambacho ni uongo na kuidhalilisha nchi," alisema.

Kiongozi huyo wa Bunge la Tanzania alidai Masele ni kiongozi ambaye amekuwa akifanya mambo ya ovyo ovyo ndiyo maana ameitwa kwenye Kamati ya Maadili.

"Tumemwita aje atufafanulie, huenda yuko sahihi lakini kwa mtazamo wetu, tunaona anafanya mambo ya hatari ikiwamo kugonganisha mihimili," Ndugai alisema.

"Amekuwa akipeleka mhimili wa juu kabisa wa serikali maneno mengi ya uongo na kudhalilisha Bunge na ushahidi upo. Ni kiongozi ambaye amejisahau, sijui

INAENDELEA UK. 8



Mama wa Kimaasai muuza za dawa za tiba asilia akifanya mabadiliko ya bei za bidhaa zake kwenye ubao, nje ya soko la Sabasaba, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## SAKATA LA KOROSHO

# Serikali yaeleza sababu kuvunja mkataba na Kampuni ya Power Solutions ya Kenya

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, amesema Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi na Gavana wa Benki Kuu (BoT), Prof. Florens Luoga, hapaswi kulaumiwa kutokana na kushindwa kwa Kampuni ya Indo Power Solutions ya Kenya kununua korosho nchini.

Jumatatu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imewasilisha hotuba yake bungeni kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka ujao wa fedha na kuwataka viongozi wote, wakiwamo Prof. Kabudi na Prof. Luoga, walioshiriki kutia saini makubaliano ya serikali na kampuni hiyo Kenya, kujiuzulu kutokana na kuisababishia serikali hasara kubwa.

Kambi hiyo iliiambia Bunge kuwa uamuzi wa viongozi hao kuingia mkataba wa ununuzi wa korosho tani 100,000 umeisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani milioni 500 (Sh. trilioni 1.18) baada ya kampuni hiyo kushindwa kununua zao hilo.

Hata hivyo, katika mkutano wake na waandishi habari kwenye Ukumbi wa Idara ya Habari na Elimu ya Bunge jijini Dodoma jana, Waziri Kakunda alisema Prof. Kabudi na Prof. Luoga hawapaswi kulaumiwa kutokana kushindwa kwa Kampuni ya Indo Power kununua korosho kwa kuwa hawakushiriki mazungumzo ya serikali na kampuni hiyo.

Alisema taarifa kwamba Kampuni ya Indo Power ni ya kitapeli si za kweli kwa kuwa serikali ilijiridhisha uhalali wake kutoka kwa Balozi wake nchini Kenya na Balozi wa Kenya nchini.

"Kila tuliyekubaliana naye bei, tulitia saini naye mkataba. Kampuni ya kwanza kutia saini mkataba ilikuwa Indo Power Solutions ya Kenya ambayo ilitia saini mkataba Novemba 30, 2018," Kakunda alisema na kufafanua zaidi:

"Yule Mkurugenzi wa Indo Power Solution alitia saini na Mkurugenzi wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko mkoani Arusha na sisi (mawaziri) tulikuwa mashahidi.

"Wizara yangu kupitia mimi ndiyo niliwaalika na Waziri wa Sheria na Katiba wakati huo alikuwa Prof. Kabudi na nilimwalika mahsusi kwa sababu mkataba ule ulifanyiwa mapitio kwa kina na Ofisi ya AG (Mwanasheria Mkuu wa Serikali) ambayo ipo chini yake.

"Nilimwalika Gavana wa BoT ambaye malipo yote ya korosho

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# JWTZ watumia ATCL kwenda Darfur

**Na Luteni Selemani Semunyu**

MAOFISA na askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wanaoshiriki ulinzi wa amani katika Jimbo la Darfur nchini Sudan, wametumia Ndege ya Shirika la Ndege ya (ATCL), kwenda nchini humo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Mafunzo na Utendaji Kivita wa (JWTZ), Meja Jenerali Alfred Kapinga, alisema Jeshi ni taasisi inayoongozwa na uzalendo, uadilifu, uhodari hivyo ni faraja kubwa kwao na wapiganaji kuunga mkono jitihada za serikali.

Alisema hatua ya kupanda ndege hiyo ni sehemu ya mchango wao katika kuonyesha uzalendo kwa vitendo kwa kutumia vitu vya nyumbani kwa maslahi mapana ya taifa.

"Tumekuwa tukitumia ndege zetu za Jeshi, lakini tumekuwa tukitumia ndege za mataifa mengine kwa mikataba kutoka Umoja wa Mataifa, sasa ni faraja kwani tumefanikiwa kuwashawishi Umoja wa Mataifa kutumia ndege zetu," alisema Meja Jenerali Kapinga.

Aidha, Meja Jenerali Kapinga, aliwaasa maofisa na askari hao kuhakikisha wanapeperusha vyema bendera ya nchi na kuendelea kuitangaza kwa sifa nzuri za utendaji kimataifa.

Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi, alisema ni fursa nzuri kwa ATCL na wanalishukuru Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kupitia kwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi kwa mchango mkubwa kufanikisha kupata zabuni hiyo.

"Namshukuru Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali, Venance Mabeyo na watendaji wake kwa uzalendo wake na kuhakikisha anafanikisha ATCL kupata fursa kwa mara ya kwanza na hii itakuwa mwanzo mzuri na tutahakikisha tunaitumia vizuri fursa hii kujitangaza zaidi kimataifa kwa maslahi ya nchi " Alisema Mhandisi Matindi.

Vilevile Mhandisi Matindi aliongeza kuwa ndege ya Dream Liner ina uwezo wa kusafiri kwa saa 12 bila kusimama, hivyo kwa kutumia saa tatu kusafiri kutoka nchini mpaka Sudan ni sehemu ndogo ya uwezo wake na ni nafasi ya kuwajaribisha watendaji wa ndege wa ATCL katika kuhudumia safari ndefu.

Naye Kamanda wa kikosi cha TANZBATT- 13, Luteni Kanali Khalfan Kayage anayekwenda na Kikosi hicho alisema kuwa inawapa nguvu kupeperusha bendera ya Tanzania kupitia ndege na ameahidi kufanya kazi kwa bidii kuendeleza jina na sifa nzuri ya Tanzania kimataifa.

# CAG naye akaguliwa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

RIPOTI ya ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kwa mwaka wa fedha 2017/18, imekabidhiwa bungeni.

Kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania ya Mwaka 1977, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ndiye mkuu wa NAOT.

Akitoa taarifa bungeni jana, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema amepokea ripoti ya ukaguzi wa hesabu za ofisi hiyo kwa mwaka unaoisha Juni, 2018 na kuipa jukumu Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuipitia na kuichambua.

"Katika ukaguzi wa hesabu, CAG kwa mujibu wa Kifungu cha 46(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sheria Namba 11 ya Mwaka 2008, hesabu za CAG zinapaswa kukaguliwa angalau mara moja kwa mwaka na PAC huwa ina jukumu la kuteua mkaguzi wa kukagua hesabu za ofisi hiyo," alisema.

Alisema Bunge ndiyo linatafuta mkaguzi wa hesabu hizo na ripoti aliyoipokea, ilifanywa na kampuni ya ukaguzi wa Hesabu ya EK Mangesho & Company.

"Katika hesabu zilizowekwa mezani wakati ule hesabu za ofisi ya CAG huwa haziwekwi mezani pale. Sasa utaratibu ni huu ninaoeleza. Nimepokea taarifa hii na nimeipitia, kuna mambo... na utaratibu ni kupeleka PAC watapitia na kuichambua na kuwasilisha kwangu, mengine yatafuata," alisema.

Spika Ndugai alisisitiza kuwa katika masuala ya ukaguzi hakuna ambaye anabaki na hakuna anayejikagua bali kila watu wanaangalia wenzao.

Aprili 13, mwaka jana, CAG Prof. Mussa Assad, aliwaambia waandishi wa habari bungeni jijini Dodoma kuwa ofisi yake nayo huwa



IPP media

IPP Media tunatoa shukurani za dhati kwa Vyombo vyote vya Habari vilivyoshirikiana nasi katika kuchapisha na kurusha mubashara **MSIBA MZITO wa MPENDWA WETU MWENYEKITI MTENDAJI WA IPP - DKT. REGINALD MENGI.**

Aidha tunawashukuru kwa mchango wenu wa hali na mali mliotoa katika kipindi chote cha **MSIBA.**

***Tunasema asante sana kwa:-***

**TV WASHIRIKA:**
1. CLOUDS TV
2. AZAM TV
3. TBC
4. STAR TV
5. CHANNEL 10
6. TV ONE
7. TV E
8. TOP TV UKONGA
9. RISE AND SHINE TV
10. WASAFI TV
11. DIRA TV
12. UPENDO TV

**RADIO WASHIRIKA:**
1. CLOUDS FM
2. MAGIC FM
3. E FM
4. TIMES RADIO
5. RADIO FREE AFRICA
6. RADIO 5
7. PASSION FM
8. PAMBAZUKO FM IFAKARA
9. TOP RADIO MOROGORO
10. HIGHLANDS FM
11. PLANET FM
12. KILI FM MOSHI
13. SUNRISE RADIO ARUSHA
14. UHAI FM
15. UPENDO RADIO
16. WASAFI RADIO

**MITANDAO:**
1. CLOUDS DIGITAL
2. GLOBAL ONLINE TV
3. MILARD AYO
4. MICHUZI BLOG
5. POA TV
6. AZAM DIGITAL
7. WASAFI DIGITAL

**MAGAZETI:**
1. MWANANCHI/THE CITIZEN
2. DAILY NEWS/HABARI LEO
3. MTANZANIA
4. TANZANIA DAIMA
5. GLOBAL PUBLISHERS
6. UHURU/MZALENDO
7. JAMHURI
8. MAJIRA
9. TAZAMA

***Na kwa wengine wote walioshiriki nasi kwa njia moja au nyingine tunasema AHSANTE SANA NA MUNGU AWABARIKI.***

HABARI KITAIFA

# Mashamba yaliyofutiwa milki yote kupitiwa upya

**Na Munir Shemweta,** KILOSA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema serikali kupitia wizara yake itapitia upya mashamba yote yaliyofutwa na Rais katika wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro.

Lukuvi alisema hayo jana katika kata ya Chanzulu, wilayani hapa, alipozungumza na wananchi alipokwenda kutatua mgogoro wa ardhi katika wilaya hiyo ikiwa ni jitihada za wizara kumaliza migogoro ya ardhi nchini.

Waziri Lukuvi alisema katika maeneo mbalimbali yako mashamba yaliyofutwa na Rais lakini hayajawekewa utaratibu wa kuyatumia, hivyo kutoa fursa kwa wajanja wachache kujigawia na mengine kuyauza kwa wananchi bila kufuata utaratibu.

Alisema katika kuhakikisha mashamba yote yaliyofutwa na Rais katika wilaya ya Kilosa na kuzua mgogoro baina ya

INAENDELEA UK. 26



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ndungile Yudas (wapili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa taarifa ya ugonjwa wa homa ya Dengue na kutaja sehemu zilizoathirika na ugonjwa huo kuwa ni Dar es Salaam na Tanga. Kushoto ni Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Mohamed Kambi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## KESI YA ZITTO
# Shahidi adai maneno yalimfanya kuichukia polisi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeambiwa na shahidi wa Jamhuri, Mashaka Duma, katika kesi ya uchochezi inayomkabili, Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, kwamba yeye ni shabiki wa mbunge huyo, anaposikia sauti yake anafurahi na anapomuona kwenye televisheni.

Alidai kuwa alipomsikia akizungumzia mauaji ya Uvinza Kigoma, aliamini na kuwachukia polisi.

Mashaka alitoa madai hayo jana katika mahakama hiyo wakati akitoa ushahidi wa Jamhuri mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, anayesikiliza kesi hiyo.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, shahidi alidai roho yake imetulia baada kutoa hisia zake mahakamani kwamba analichukia Jeshi la Polisi kwa kitendo wanachodaiwa kukifanya Uvinza Kigoma.

Shahidi mwingine, Shabani Hamisi, amedai kitendo cha Tundu Lissu, kushambuliwa kwa risasi na hajawahi kukamatwa mtu kuhusiana na tukio hilo kilimfanya aamini maneno ya mshtakiwa kuwa Kigoma Uvinza kuna watu waliuawa.

Alidai polisi walipokuwa wakipita na gari lao Manzese walikuwa wakizomea kwamba wauaji hao.

INAENDELEA UK. 26






# Upelelezi kujipatia fedha kwa jina la Janeth Magufuli haujakamilika

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imeambiwa kwamba upelelezi wa kesi ya kujipatia na kutakatisha Sh.milioni 4.487 kwa kutumia jina la Mke wa Rais wa Tanzania, Janeth Magufuli, bado haujakamilika.

Kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde.

Washtakiwa katika kesi hiyo wanadaiwa kuwa watu wa familia moja ambao ni Saada Uledi, Maftaa Shabani, Heshima Ally na Shamba Mdaila.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika uliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Kasonde alisema kesi hiyo itatajwa Mei 30, mwaka huu.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka manne wanayodaiwa kutenda katika tarehe tofauti kati ya Januari 2017 hadi Machi, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Ilidaiwa kwamba katika tarehe hizo washtakiwa hao walikula njama ya kutenda kosa la kuchapisha taarifa za uongo kupitia mtandao wa Facebook.

Ilidaiwa kuwa, washtakiwa hao katika tarehe hizo ndani ya Jiji la Dar es Salaam, walifungua akaunti ya Facebook yenye jina la Janeth Magufuli ambaye ni Mke wa Rais Magufuli na kuchapisha taarifa ya uongo.

Taarifa hiyo ilieleza, 'Janeth Magufuli amefungua taasisi ya kutoa mikopo kwa watu na moja ya sharti la mkopo huo ni kutuma fedha kwanza kama kinga ya mkopo atakaopewa', wakati wakujua ni uongo.

Katika shtaka lingine, wanadaiwa kuwa kupitia taarifa hiyo ya uongo na kwa nia ovu, walijipatia Sh. 4,487,000 fedha ambazo zilitumwa kwa njia ya simu kupitia ya Paul Kunambi.

Washtakiwa hao pia wanadaiwa kutakatisha fedha Sh.4, 487,000 huku wakijua zilitokana na kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

HABARI KITAIFA

# Rais wa AfDB aipongeza Tanzania ukuaji uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinwumi Adesina, ameipongeza Tanzania kwa ukuaji mzuri wa uchumi wa wastani wa asilimia saba kwa mwaka na hivyo kuendelea kuwa miongoni mwa nchi zenye uchumi unaokua kwa kasi kubwa duniani.

Dk. Adesina alitoa pongezi hizo jana Ikulu jijini Dar es Salaam muda mfupi baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na Rais Dk. John Magufuli kuhusu ushirikiano kati ya benki hiyo na Tanzania katika maeneo mbalimbali ya maendeleo.

Dk. Adesina alimpongeza Rais Magufuli kwa dhamira yake njema na msimamo wake wa kuwapigania Watanzania na alimtaka aendelee na mwelekeo huo ambao umeendelea kuimarisha uchumi kwa ukuaji wa wastani wa asilimia saba ikilinganishwa na wastani wa ukuaji wa uchumi wa dunia wa asilimia 3.5.

Alimpongeza kwa ushirikiano na nchi jirani kama vile Uganda na hivyo kufanikisha ujenzi wa mradi mkubwa wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi lenye urefu wa kilometa 1,443 kati ya Hoima nchini Uganda na Bandari ya Tanga nchini kwa kushirikisha sekta binafsi.

Aidha, Dk. Adesina alisema wamezungumzia kuhusu kilimo na kwamba AfDB ipo tayari kusaidia kutatua tatizo la

**INAENDELEA UK. 26**



Ofisa Mawasiliano wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa), Joseph Mkonyi (kulia), akibandika stika kwenye moja ya magari ya yanayosambaza huduma ya majisafi katika zoezi la usajili wa magari hayo, jijini humo na miji ya Bagamoyo na Pwani, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbarawa ateua wakurugenzi maji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amefanya uteuzi wa wakurugenzi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji ya Kigoma, Shinyanga ma Musoma.

Taarifa iliyotolewa jana ilisema Prof. Mbarawa amefaya uteuzi huo kwa mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa kifungu Na. 17 cha Sheria Na. 12 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009,

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, ilisema katika uteuzi huo, Mhandisi Mbike Lyimo ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kigoma (Kuwasa).

Kabla ya uteuzi huo, taarifa ilieleza kuwa Lyimo alikuwa Meneja wa Ufundi katika mamlaka hiyo.

Naye Flaviana Kifizi ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Shinyanga (Shuwasa). Kabla ya uteuzi huu, Bi Kifizi alikuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji na Meneja wa Rasilimali Watu na Utawala wa Shuwasha.

Aidha, Mhandisi Lupoja ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Musoma (Muwasa). Kabla ya uteuzi huu, Mhandisi Lupoja alikuwa akikaimu nafasi hii.

# Makumbusho ya Taifa yandaa Mama na Mwana

**Na Romana Mallya**

MAKUMBUSHO ya Taifa (NMT), imeandaa Tamasha la Mama na Mwana ambalo litatoa fursa kwao kupata elimu ya mambo ya kale ikiwa ni jitihada za kuamsha ari ya Watanzania kujifunza tamaduni za urithi wa mababu.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa NMT, Prof. Audax Mabula, wakati akizungumzia Siku ya Makumbusho Duniani inayotarajia kuadhimishwa kesho.

Prof. Mabula alisema ari ya kujifunza urithi wa asili ulioachwa na mababu na bibi umeshuka kwa watu wazima ikilinganishwa na idadi kubwa ya watoto ambao hujitokeza kila mara kwenda makumbusho mbalimbali za taifa.

"Tumeandaa tamasha la mama na mwana ambapo wazazi wataambatana na watoto wao siku ya Jumamosi kushiriki siku hii ya makumbusho duniani ambayo kitaifa itafanyika Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama, Dar es Salaam ili kukumbushana umuhimu wa tamaduni zetu," alisema.

Alisema tamasha hilo litatanguliwa na maandamano yatakayoanzia eneo la Bamaga hadi Kijiji cha Makumbusho ambako washiriki na watoto wao watajifunza tamaduni za makabila mbalimbali na kula chakula cha asili bure.

"Tunatarajia kuwa na wageni 400 wakiwa na watoto wao ambao watatembelea nyumba za asili zilizopo kwenye vijiji vya makumbusho maeneo tofauti Tanzania, kutakuwa na michezo ya jadi kama kuruka kamba, mdako, rede, kombolela na kidali poo," alisema.

Prof. Mabula aliwakaribisha Watanzania siku hiyo watembelee makumbusho na nyumba za utamaduni na Kijiji cha Makumbusho kwenye mikoa mbalimbali ili wapate elimu kwa sababu hakutakuwa na kiingilio.

Alisema Siku ya Makumbusho Duniani kwa mwaka huu imebebwa na kaulimbiu isemayo, "Makumbusho kitovu cha utamaduni: Hatima ya mila na desturi."

Alisema kwa mwaka jana siku hiyo iliadhimishwa duniani katika makumbusho 40,000 zilizopo nchi 152.

Alisema kwa mwaka huu Makumbusho ya Taifa ikishirikiana na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa), Hifadhi ya Ngorongoro (NCA-Makumbusho ya Bonde la Olduvai) na Idara ya Mambo ya Kale kwa pamoja zitashiriki kuadhimisha siku hiyo.

Alisema lengo ni kuleta uelewa kwa umma kwamba Makumbusho ni taasisi muhimu ambayo urithi wa utamaduni wa nchi unahifadhiwa, unabadilishana, unahuishwa na kurutubishwa ili kujenga amani kwa wananchi.


**LIQUIDATION NOTICE**

**NAKHAR LIMITED**

**( REG NO: Z0000016138 )**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN TO THE GENERAL PUBLIC,**

"THAT at an extraordinary general meeting of the above named company. held at Zanzibar on 31st Day of March 2019, the following special resolution was passed,viz:

"THAT the Company be wound up voluntarily under the provisions of the Company Act No 15 of 2013 and that Mr. Seif S. Issa of IMARA CONSULTANTS be hereby appointed LIQUIDATOR for the purpose of such winding'

Any claim for / against the company must be addressed to the Liquidator ( as addressed below ) within fourteen days from the date of the first appearance of this notice.

Dated at Zanzibar this 15th Day of May , 2019.

SEIF S. ISSA
Imara Consultants
P O Box 1941
Tel: 024 2235303, 0777 410069
Zanzibar.

215232502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dengue inatisha, hatua za ziada zichukuliwe

**PAMOJA** na tahadhari inayoendelea kutolewa na mamlaka za serikali kwa wananchi kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa wa homa ya dengue, kasi ya maambukizi imeendelea kuongezeka.

Jana serikali ilitangaza kwamba watu 75 wanabainika kila siku kuwa na virusi vya homa ya dengue, hali iliyosababisha idadi ya wagonjwa kuongezeka kufika 1,901, tangu ugonjwa huo ulipoingia nchini Januari mwaka huu.

Kati ya wagonjwa hao, 1,809 ni wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, 89 kutoka Tanga mmoja (Singida), mmoja Kilimanjaro na mmoja (Pwani).

Aliyebainisha haki hiyo ni Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Mohammed Kambi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya ugonjwa huo nchini.

Kwa mujinu wa Prof. Kambi, katika kipindi cha siku tisa ambazo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jinsia, Wazee na Watoto ilikuwa ikikusanya muenendo wa hali ya ugonjwa huu nchini, kuna ongezeko la wagonjwa 674 sawa wastani wa wagonjwa 75 kwa kila siku, ikiwa ni tofauti ya wastani wa wagonjwa 32 waliopatikana kila siku kwa mwezi uliopita.

Alisema ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa uelewa, kuhusu ugonjwa huo kwa wananchi wengi wenye dalili, hivyo wanajitokeza kupata huduma za uchunguzi ambazo zimeendelea kupanuka kwenye vituo vya afya katika mikoa ya Dar es Salaam na Tanga.

Kimsingi, hali ya maambukizi ni ya kasi sana katika Mkoa wa Dar es Salaam kutokana na taarifa ya Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Yudas Ndugile, ambaye aliyataja maeneo yenye wagonjwa wengi kuwa ni Ilala (253), Vingunguti (86), Kariakoo (79), Sinza (223), Mbezi (78), Kimara (65), Masaki (56), Msasani (50), Wazo (49), Kinondoni (45) na Mikocheni (40). Mengine ni Gerezani (40), Tabata (41), Mbezi Beach (37), Tandale (38), Ukonga (26), Kijitonyama (34), Mwenge (28) na Tegeta (27).

Kwamba hivyo ni vituo ambavyo vimetoa wagonjwa zaidi ya 25, lakini zipo kata nyingine nyingi ambazo zina wagonjwa wa homa ya dengue katika wilaya zote za jiji hilo.

Tunaamini kuwa elimu iliyotolewa kwa jamii imesaidia sana watu wengi kujitokeza baada ya kuona dalili na kukutwa wakiwa na homa ya dengue, kisha kuanzishiwa matibabu.

Hata hivyo, tunapata wasiwasi pia kwamba huenda watu wengi hawajachukua hatua dhidi ya tahadhari inayoendelea kutolewa na wataalamu wa afya. Pengine ndiyo maana kila siku wanabainika wagonjwa 75, ambayo ni idadi kubwa.

Hata kama elimu dhidi ya ugonjwa huo imetolewa na kuongeza mwamko wa watu kwenda katika vituo vya huduma za afya, lakini tunaona kwamba ni vizuri jambo hilo likaenda sambamba na na serikali pamoja na wananchi kuchukua tahadhari za kuzuia.


Miongozi mwa hatua hizo ni kuweka mazingira katika hali ya usafi pamoja na kuharibu maeneo yote ya mazalia ya mbu ambao wanaeneza ugonjwa huo.

Kwa Mkoa wa Dar es Salaam ambao takwimu zinaonyesha kuathirika wa kiasi kikubwa, tulitarajia kuona mamlaka husika zikiwamo za maji pamoja na za halmashauri na Manispaa za Jiji zikichukua hatua ya kupuliza dawa katika maeneo yenye majimaji na maeneo mengine ambayo ni mazalia ya mbu.

Tunapongeza hatua ya utoaji wa elimu ambayo imewezesha watu wengi kututokeza kupima, lakini tunashauri kuwa tahadhari ni nzuri zaidi kuliko kusubiri tiba, hivyo hatua za kudhibiti maambukizi zitakuwa endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Fursa kuchangamkia kilimo cha Bonde Bugwema, Musoma Vijijini

Na Sabato Kasika

**BENKI** ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imeingia mkataba na Halmashauri ya Musoma, kwa ajili kuboresha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, katika bonde la Bugwema.

Mbali na kilimo hicho, bonde hilo lenye zaidi ya ekari 800 limegawanywa pia kwa ajili ya malisho ya mifugo, kujenga shule, zahanati na ofisi ya serikali ya kijiji na taasisi nyingine za serikali.

Mkataba huo ulifanyika hivi karibuni mbele ya viongozi mbalimbali, akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima na wengine. Benki hiyo itatoa vifaa vya kilimo kwa wananchi.

Utaratibu wa kurejesha mkopo unalenga kuhakikisha unawanufaisha wakulima wa vijiji vya Kata ya Bugwema, watakaokuwa ndani ya mradi huo wa kilimo cha umwagiliaji.

Pembejeo zitakazotolewa na mwekezaji ni zana za kisasa za kilimo, mbegu, mbolea na huduma nyingine pale zitakapokuwa zinahitajika, huku mazao ya kuanzia yakiwa ni mpunga, mahindi na vitunguu.

Inaelezwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Musoma, John Kayombo, kuwa katika awamu ya kwanza, wanufaika watakuwa wakazi wa Bugwema na kwamba kadri mradi utakavyokuwa unaendelea, wakazi nje ya Bugwema watakaribishwa.

Kwa utaratibu uliopo ni kwamba mwekezaji akisharudisha gharama zake, mradi huo wa kilimo cha umwagiliaji utakabidhiwa kwa wananchi, chini ya usimamizi wa halmashauri yao.

Inaelezwa, kuwa gharama kamili za mwekezaji zitajulikana na baadhi ya miezi michache ijayo na kwamba, kwa sasa anaendelea na kukamilisha mambo kadhaa yatakayomwezesha kufanikisha mradi huo.

Nimeanza kueleza kwa kirefu kile ambacho kinaendelea katika bonde hilo, lengo ni kutaka kuwaambia wakazi wa Bugwema kuchangamkia fursa hiyo ili waweze kunufaika na kilimo hicho.

Bugwema ipo jimbo la Musoma Vijijini, ambalo kwa sasa limejikita kwenye mambo matatu, ambayo ni kuboresha elimu, huduma ya afya na kilimo cha umwagiliaji kikiwamo cha bustani.

Kazi hiyo inafanyika kwenye kata vijiji 68, huku mbunge wa jimbo hilo, akigawa bure mbegu za mazao mbalimbali zikiwamo za alizeti ambalo, ni zao jipya katika jimbo hilo na Mkoa wa Mara kwa ujumla.

Mwekezaji katika bonde hilo ni moja ya mikakati ya kuinua kilimo, ili kiweze kuwa na tija jimbo humo, kwa wananchi kupata mazao ya chakula na biashara, hivyo wananchi hawana budi kuchangamkia fursa hiyo.

Kupata mbegu bure, pia kupata mwekezaji ni hatua nzuri inayoweza kuwafanya wakulima wakainuka kiuchumi iwapo watachangamkia fursa hiyo, hasa vijana ambao hukimbilia mijini badala ya kujikita katika kilimo.

Vijana ni nguvukazi katika nyanja zote, lakini kwenye kilimo wamekuwa ni wazito, baadhi yao wamekuwa wakikwepa kukimbilia mjini kutafuta vibarua, kama vile kilimo hakina tija.

Musoma Vijjini mmepata mwekezaji katika bonde la Bugwema. Bahati nzuri mbunge wenu amekuwa mstari wa mbele kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kujiletea maendeleo.

Hivyo, njia pekee ya kufanikisha kilimo hicho ni wakulima wa maeneo husika kushiriki kikamilifu na hatimaye mradi huo kuwa mkubwa zaidi wa kuweza kunufaisha jimbo zima badala ya Bugwema pekee.

Ikumbukwe kuwa maendeleo ya uhakika kwenye kilimo hayawezi kupatikana, kama wakulima hawatazingatia kile ambacho wanaelekezwa na wataalam wa kilimo.

Najua kwamba, kwa muda mrefu wataalamu wa kilimo wa Halmashauri ya Musoma Vijijini, wamekuwa wakihamasisha kuhusu mbinu za kisasa kwenye kilimo ili kupata mazao mengi.

Mbinu hizo ambazo wameelekezwa ndizo wanapaswa kuzitumia kwenye kilimo cha umwagiliaji katika bonde hilo la Bugwema lililoanzishwa na Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere katika miaka ya 70.

# Wafungwa waomba kupewa vyeti vya ujuzi

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imeahidi kulifanyia kazi ombi la wafungwa la kupewa vyeti wanapomaliza vifungo vyao wakiwa na ujuzi walioupata magerezani.

Mtaalam wa kuchakata ngozi, Abuu Shaban, aliwasilisha ombi hilo jana mbele ya Kamishna Jenerali wa Magereza Tanzania, CGP. Faustine Kasike.

Aliomba serikali iangalie uwezekano wa kupata vyeti vya ujuzi wanapotoka gerezani ili iwe rahisi kupata kazi na kujiajiri mitaani.

"Kamishna nakuomba hawa vijana wanapotoka huku mjaribu kuwapatia vyeti ili wakajiendeleze huko mtaani, tunataka wakiwa mtaani wafanye kazi ili tukomeshe wimbi la ujambazi na wizi," alisema.

Alisema vijana anaowafundisha namna ya kuchakata ngozi gerezani wamemuomba awasilishe ombi hilo la vyeti kwake.

Pia alisema wafungwa hao walimuomba wakiwa uraiani awatafute ili waendeleze ujuzi walioupata magerezani.

Akizungumzia kuhusu ombi hilo, Kamishna Martine alisema amelipokea na kumweleza Shaban kuwa wanaweza wakaandaa eneo moja ili iwe rahisi kuwasaidia hata kwenye masuala ya mitaji.

"Hili wazo ni zuri na nimelichukua kwa sababu tunaweza kuwatumia wenzetu wa Veta kwa sababu ndizo mamlaka zinazoweza kutusaidia katika eneo hili katika kutoa vyeti," alisema.

Alisema lengo ni kuwasaidia wafungwa waliomaliza vifungo vyao na kupitia program ya urekebishaji na kupata ujuzi wa aina mbalimbali wanapotoka wajiajiri.

Alisema wamekuwa wakiwashirikisha Veta katika programu mbalimbali wanazoziendesha magerezani hususani za utoaji ujuzi wa aina tofauti.

"Utoaji wa vyeti kwa wafungwa waliomaliza vifungo vitawasaidia kutambulika uraiani hata kuanzishiwa umoja na kufanya shughuli halali na kujiepusha na uhalifu na kurudi gerezani," alisema.

# Serikali yaahidi jeshi la kisasa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SERIKALI imesema mwaka ujao wa fedha, itapatia Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) vifaa na zana bora za kisasa kwa lengo la kuwa na jeshi la kivita.

Vievile, imesema itatoa mafunzo kwa wanajeshi ili kuliongeza uwezo na weledi wa kiutendaji, kiulinzi na kivita.

Akiwasilisha hotuba bungeni jijini Dodoma jana kuhusu makadirio ya bajeti yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussen Mwinyi, alisema wizara hiyo pia imepanga kutekeleza vipaumbele 12.

Alivitaja kuwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kikazi kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma.

Alisema wizara yake pia itawapatia vijana wa Tanzania mafunzo ya ukakamavu, umoja wa kitaifa, uzalendo na stadi za kazi.

Alisema wizara pia itaendeleza utafiti na uhawirishaji wa teknolojia kwa kuimarisha na kuanzisha viwanda kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia huku ikiimarisha ushirikiano na jumuiya za kimataifa, kikanda na nchi moja moja katika nyanja za kijeshi na kiulinzi.

Alisema mpango mwingine wa wizara mwakani ni kupima, kuthamini na kulipa fidia ya ardhi katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya jeshi.

Dk. Mwinyi aliongeza kuwa jeshi litaendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura pale inapohitajika,

"Wizara pia italipa stahili mbalimbali za maofisa, askari, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na watumishi wa umma, kukamilisha Sera ya Ulinzi wa Taifa, Mwongozo wa Viwanda Jeshini na Mpango wa Maendeleo wa Miaka 10 yaani 2018/29-2027/28 wa kuliimarisha Shirika la Nyumba," alisema.

Aliongeza kuwa hali ya usalama wa mipaka ya Tanzania kuwa ni nzuri licha ya kuwapo tishio kutoka kwenye vikundi vya kigaidi katika baadhi ya nchi jirani.

Waziri huyo alisema wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali, kubwa ikiwa ni ufinyu wa bajeti, akibainisha kuwa Sh. trilioni 1.9 ilizoidhinishiwa na Bunge kwa ajili ya mwaka huu wa fedha, hazikidhi mahitaji halisi.

Ili kutekeleza majukumu yake, Dk, Mwinyi aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 1.85 kwa ajili ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

Kati yake, Sh. trilioni 1.72 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 128 ni za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.



Mmoja wa wakazi wa kijiji cha Msamalo, wilayani Chamwino, Mkoa wa Dodoma, Kwa niaba ya wenzake akikabidhi zawadi ya mbuzi kwa Mbunge wa Viti maalum mkoa wa Dodoma, Mariam Ditopile, wakati akihitimisha ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo, jana. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Bunge laagiza madeni Wizara ya Ulinzi yalipwe

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kuongeza kasi ya ulipaji wa madeni ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuongeza fedha kwenye fungu la miradi ya maendeleo ya wizara hiyo.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, mjumbe wa kamati hiyo, Victor Mwambalaswa, alisema katika mwaka huu wa fedha, kati ya Sh. bilioni 112.6 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, Sh. bilioni 105.2 (asilimia 93) zilitumika kulipa madeni ya mikataba.

Mwambalaswa alisema kulipa madeni hayo kwa wakati kutasaidia serikali kuokoa fedha zinazoongezeka kwa ajili ya malipo ya riba na kuelekeza fedha kwenye maeneo mengine.

"Serikali itoe fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu la 38 kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Hadi kufikia Machi 2019, fungu hili lilikuwa limepokea Sh. bilioni 3.34 kati ya Sh. bilioni nane zilizokuwa zimeidhishwa na Bunge, sawa na asilimia 41.83. "Sambamba na ushauri huo, serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha za maendeleo zilizotengwa kwa mwaka 2019/2020 na kutoa fedha hizo kwa wakati," alisema.

# Mbunge CCM kuhojiwa Kamati ya Maadili

INATOKA UK. 2

anatafuta kitu gani.

"Hizo vurugu ambazo anazionyesha kwenye Bunge lake huko, sisi hazituhusu sana. Tumemwita aje kwa mambo ya hapa nyumbani ya utovu wa nidhamu.

"Kwa kuwa tumekuwa tukimwita hapa nyumbani tangu Jumatatu hataki kurudi, nimemwandikia barua Rais wa PAP ya kusitisha uwakilishi wa Stephen Masele (pichani) katika Bunge la PAP hadi hapo Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itakapokamilisha uchunguzi na tuhuma dhidi yake."

Ndugai alisema amemsimamisha kwa muda uwakilishi wa Masele hadi pale Bunge la Tanzania litakapomalizana naye.

"Kuna kamati mbili zinamsubiri, Kamati ya Bunge ya Maadili lakini na Kamati ya Maadili ya CCM nayo kuna mambo anahitajika kuyajibu nyumbani.

"Kwa hiyo, kuanzia sasa yeye si mbunge wa Bunge la PAP hadi tumalize masuala ya hapa nyumbani ndiyo tutaamua wenyewe tunaendeleaje kuanzia hapo," alisema.

**CHADEMA WAMTETEA**

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimemkingia kifua Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika (PAP), Stephen Maselle, kwa kulitaka Bunge na



Serikali ya Tanzania kutoa msimamo wake, kuhusu tuhuma zinazomkabili Rais wa Bunge hilo, Roger Nkodo Dang.

Chama hicho kimesema kitendo cha Bunge kumrejesha nchini Maselle wakati alitakiwa kuongoza vikao vya Bunge hilo vinapokuwa vinajadili taarifa ya Kamati Maalum kuhusu tuhuma za Rais wake na kusimamia utekelezaji wa maazimio, inaibua shaka na kujenga taswira mbaya kwa nchi.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Chadema, Tumaini Makene, ilieleza kuwa hatua iliyochukuliwa na serikali inaonyesha kuwa nchi inataka kutumika au inataka kutumika kumwokoa Rais Dang dhidi ya tuhuma zinazomkabili ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka na unyanyasaji wa kingono.

"Katikati ya mkanganyiko huu, Chadema inapenda kuweka msimamo wake wazi kuwa jina la nchi yetu Tanzania lisitumike vibaya wala kuwekewa taswira hasi na kuendelea kuharibu sura yetu kidiplomasia na katika mahusiano ya kimataifa," alisema Makene.

Alisema kwa mujibu wa taarifa walizopata kutoka ndani ya bunge hilo zimedai kuwa Dang, anatumia njia mbalimbali kupambana kujisafisha na tuhuma hizo kwa sababu atapoteza nafasi yake hiyo kwenye PAP, iwapo zikithibitika kuwa ni kweli.

Alisema pia zitamwondolea kinga za kidiplomasia alizo nazo huku ikijulikana wazi kuwa tuhuma hizo zinazomkabili ni mojawapo ya makosa makubwa ya kijinai yanayochukuliwa kwa uzito mkubwa nchini Afrika Kusini.

# Serikali yaeleza sababu kuvunja mkataba

INATOKA UK. 2

yatapitia Benki Kuu. Kwa hiyo, kumwalika ilikuwa ni sahihi na Naibu Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa walikuwa kama sehemu ya wahudhuriaji.

"Kilichonishangaza mimi wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, ni baadhi ya wabunge kupeleka lawama kwa Prof. Kabudi kwamba yeye ndiyo amemshauri Rais, nakanusha Prof. Kabudi hakuhusika wala hatukuwa tumempelekea."

Alisema sababu ya kusitisha mkataba na Kampuni ya Indo Power ni kutokana na kampuni hiyo ya Kenya kukiuka matakwa yaliyokuwapo kwenye mkataba.

"Tuje kwa mnunuzi Indo Power Solutions, kwenye mkataba ule aliahidi kulipa tani 100,000 ndani ya siku 10, baada ya siku tano kupita, akatoa taarifa kwamba anaomba aongezwe muda - badala ya siku 10 iwe mwezi mmoja tukampa.

"Baada ya mwezi mmoja, akaomba tena aongezewe muda, sasa baada ya miezi miwili Machi 30, mwaka huu, timu ya wataalamu ya ushauri ya serikali ilipendekeza tusitishe mkataba ule kwa sababu hauwezi kuwa na tija kwa sababu mnunuzi hakuweza kutimiza masharti.

"Na hilo si jambo la ajabu, kama unashindwa masharti unaondolewa, ile kampuni siyo ya kitapeli, ni kampuni halisi ambayo ipo, mkienda Thika mtaikuta, Balozi wetu na wa Kenya naye walithibitisha ni kampuni halali.

"Kushindwa kununua mzigo wa tani 100,000 siyo sababu ya kuifanya ionekane kampuni ya kitapeli kwani inafanya shughuli zake kihalali pale Kenya," Kakunda alifafanua.

**KAMPUNI 6 KUNUNUA KOROSHO**

Kakunda alisema tayari serikali imeingia mikataba ya awali na kampuni sita zilizojitokeza kununua korosho zilizohifadhiwa kwenye maghala baada ya kukusanywa kutoka kwa wakulima.

"Tumeendelea kutia saini mikataba mingine na kampuni nyingine, mikataba ambayo tumetia saini ni ya awali, mpaka sasa hivi, tumesaini na kampuni sita, nisingependa kuzitaja kwa majina kwa sababu tunajua hali halisi ya biashara ya korosho, watu wanafuatiliana, wanaharibiana biashara na majina.

"Lakini, kuna kampuni moja tuliikaribisha wiki iliyopita, imekuja kukagua maghala ya korosho, wamejiridhisha kwamba korosho zetu ni safi na hazijaharibika.

"Na tumepeleka kuhakiki TBS (Shirika la Viwango) na wameenda kufanya uhakiki katika nchi yao na wamejihakikishia kwamba ni nzuri na wanajiandaa kulipa. Hawa mabwana, wakilipa tunawakabidhi korosho mara moja," Kakunda alisema.

Waziri huyo pia alibainisha kuwa katika kutekeleza maagizo aliyopewa na Rais John Magufuli wakati akiapishwa Novemba 12, mwaka jana kuhusu kusimamia ununuzi wa korosho, alisema tangu Novemba 13, mwaka jana hadi Mei 15, mwaka huu, wamekusanya tani 225,000.

"Kati ya hizo, tani 2200 zinaendelea kubanduliwa na viwanda vyetu vya ndani kwa mikataba maalum. Maana yake zinabaki tani 222,800 katika maghala," alisema.

Aliongeza kuwa walipokea maombi ya kampuni 34 kwa ajili ya ununuzi wa korosho, saba zikiwa za ndani na 27 za nje ya nchi.

"Hizo kampuni zote ziliandika barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara ama kwa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo ipo chini ya Wizara ya Kilimo na kila aliyeleta barua aliitwa kwa ajili ya mazungumzo. Wale ambao wamefikia makubaliano ya bei, walitia saini mkataba wa awali," alisema.

**HESHIMA YA NDOA**

Waziri Kakunda alisema Watanzania wengi hawana desturi ya kula korosho, akiwahimiza kula zao hilo kwa kuwa linaongeza kile alichokiita heshima ya ndoa.

"Watanzania wengi hawali korosho, ukiangalia manufaa ya korosho ni mengi. Unafikiri kwanini kusini angalau wenzetu wanazaliana sana? Korosho inaongeza rutuba kwa mwanaume.

"Tunazungumza ukweli, ukimuuliza Dk. (Faustine) Ngugulile (Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) ambaye ni daktari wa binadamu, atakwambia manufaa ya korosho ambayo ni kuongeza virutubisho kwa mwanaume kuweza kutotoa watoto wengi, hiyo ni sifa mojawapo na kurudisha heshima ndani ya nyumba, watu hawataki kula mpaka waandikiwe na daktari," Kakunda alisema.

# 75 wabainika kuwa na dengue kila siku nchini

INATOKA UK. 2

ufuatiliaji unaendelea na hatujapata wagonjwa wenye dalili za hii," alieleza Prof. Kambi.

Katika kukabiliana na changamoto ya matibabu, alisema serikali imeagiza vipimo vingine vya kupima wagonjwa 30,000 ambavyo vinatarajia kuingia nchini hivi karibuni na vitasambazwa kwenye vituo vya umma katika mkoa wa Dar es Salaam na mingine.

"Ugonjwa huu hauna chanjo wala tiba ya moja kwa moja mpaka sasa na niwatahadharishe wanaoendelea kutoa taarifa za upotoshaji kuhusu tiba ya ugonjwa huu kupitia mitandao ya kijamii," alitahadharisha.

**MKAKATI WA WIZARA**

Prof. Kambi alisema Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na mikoa na Halmashauri, wamechukua hatua mbalimbali ikiwamo kuandaa mpango wa dharura kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema pia wanaendeleza mapambano ya kudhibiti mbu, kuandaa mwongozo wa matibabu ya ugonjwa huo, kuimarisha ufuatiliaji na kutoa elimu.

Alisema pia wizara imetuma timu za wataalamu kuungana na timu za Mkoa wa Dar es Salaam ili kuudhibiti ugonjwa huo.

**HALI ILIVYO DAR**

Maganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Yudas Ndugile, alitaja maeneo yenye wagonjwa wengi katika jiji hilo ni Ilala (253), Vingunguti (86), Kariakoo (79), Sinza (223), Mbezi (78), Kimara (65), Masaki (56), Msasani (50), Wazo (49), Kinondoni (45) na Mikocheni (40).

Mengine ni Gerezani (40), Tabata (41), Mbezi Beach (37), Tandale (38), Ukonga (26), Kijitonyama (34), Mwenge (28) na Tegeta (27).

"Hivi ndivyo vituo ambavyo zimetoa wagonjwa zaidi ya 25, lakini zipo kata nyingine nyingi ambazo zina wagonjwa wa homa ya dengue katika wilaya zote za jiji hili," alisema Dk. Ndugile.

Alitaja dalili za ugonjwa huo ni homa ya ghafla, maumivu ya kichwa hususani sehemu za macho, maumivu ya viungo na uchovu.

"Dalili hizi huanza kujitokeza kati siku ya tatu hadi 14 tangu mtu alipoambukizwa virusi vya homa ya gengue. Hivyo ni muhimu wananchi kuchukua tahadhari," alisema.

**DENGUE NI NINI**

Homa ya dengue ni ugonjwa wa kitropiki unaosababishwa na virusi vya dengue maarufu kama dengue.

Homa ya dengue pia hujulikana kama, homa ya kuvunja mifupa kwa sababu inaweza kuwafanya watu wawe na maumivu makali hadi wahisi kama mifupa yao inavunjika.

Dalili za ugonjwa huu huanza siku tatu hadi kumi na nne baada ya kuambukizwa.

Baadhi ya dalili ni homa kali, kuumwa na kichwa, kuota vipele kwenye ngozi na maumivu kwenye misuli na maungio.

Kwa watu wachache, homa ya dengue inaweza kubadilika na kuwa aina zinazohatarisha maisha.

Dalili kubwa ni ile ya kuvuja damu, ambayo huifanya mishipa ya damu inayobeba damu.

Kwa kawaida matibabu huchukua siku tatu hadi saba hadi mgonjwa kupona na hakuna dawa ya chanjo inayofanya kazi kuwakinga watu dhidi ya virusi vya dengue.

HABARI KITAIFA

# Nyumba 333 Mtwara, Dar kuunganishwa gesi asilia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Nishati, inatarajia ifikapo Septemba mwaka huu nyumba 333 katika Mkoa wa Mtwara na Dar es Salaam zitakuwa zimeunganishwa na gesi asilia majumbani.

Pia, imetoa wito kwa sekta binafsi kushirikiana na serikali katika utekelezaji wa mradi mkubwa kabambe wa kusambaza gesi majumbani na viwandani.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Subira Mgalu, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kibiti(CCM), Ally Ungando.

Katika swali lake, Ugando alisema wananchi wa Kibiti wanategemea nishati yao ya mkaa na kuni na kuhoji ni lini wataunganishiwa umeme wa gesi asilia.

"Kutokana na serikali kujenga mradi mkubwa wa umeme Rufiji, je wananchi wa Kibiti wanaweza kupata vibarua," alihoji.

Akijibu maswali hayo, Mgalu alisema katika kipindi cha mwaka 2010-2020 kumekuwa na utekelezaji wa mradi wa kusambaza gesi katika maeneo mbalimbali.

Alifafanua kuwa hivi karibuni Waziri alizindua uunganishaji wa gesi nyumba 26 na matarajio ni kufikia nyumba hizo 333 ifikapo mwezi septemba mwaka huu.

Aidha alisema kwa Mkoa wa Lindi na Pwani serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) imekuja na mradi mkubwa kabambe wa kusambaza gesi asilia ambao utafanywa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

"Hadi sasa hatua iliyofikiwa amepatikana mshauri mwelekezi anaandaa makablasha na kufanya ficibility study (upembuzi yakinifu) mradi mzima na matarajio yetu ifikapo Mei 2020 kupata wakandarasi wa sekta binafsi," alisema.

Alitoa wito kwa sekta binafsi kujitokeza kushirikiana na serikali katika mradi huo mkubwa wa kusambaza umeme majumbani na viwandani na kwamba wananchi wa wilaya ya Kibiti kwa kuwa imepitiwa na bomba la gesi watanufaika.

Alisema mradi wa umeme Rufiji matarajio yake makubwa ni kuzalisha ajira na kumuahidi wananchi watanufaika na kazi na vibarua kwa sifa zitakazohitajika.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alisema wananchi hao wanatumia nishati ya mkaa na kuni, lakini imekuwa ikisababisha uharibifu mkubwa wa mazingira kwa kukata miti ovyo.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kupeleka nishati mbadala na je ni aina gani ya nishati itakayotumika badala ya kuni na mkaa," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mgalu, alisema katika kipindi kati ya mwaka 2015 hadi 2020 serikali inatekeleza miradi ya kuzalisha umeme kupitia vyanzo vya gharama nafuu vya maji na gesi.

Alisema serikali imeanza kutekeleza mradi wa kusambaza gesi asilia katika miji ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam ikiwa ni nishati mbadala ya kupunguza matumizi ya mkaa na kuni.

"Kwa sehemu kubwa ya kuni na mkaa unaotumika katika Jiji la Dar es salaam huzalishwa katika wilaya ya Kibiti, hatua ya kuanza kutumika gesi asilia kwa kupikia itapunguza uharibifu mkubwa wa mazingira," alisema.



Mkazi wa jiji akichagua nazi kabla ya kuinunua katika soko Mwananyamala, jijini Dar es Salaam jana. Nazi hutumika kwa wingi kwa ajili maandalizi ya futari katika kipindi hiki cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# MCT yasisitiza maadili uandishi wa habari

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limeshauri wanafunzi wanaosomea uandishi wa habari kufuatilia makosa ya kimaadili yanayofanyika kwenye vyombo vya habari na kuyaripoti kwenye Baraza hilo ili hatua zichukuliwe.

Ushauri huo ulitolewa na Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, wakati akizungumza na walimu wa vyuo vya uandishi wa habari Tanzania vinavyofundisha ngazi ya stashahada.

Alitoa ushauri huo katika mkutano wa mashauriano kati ya MCT na wakuu wa Idara za Uandishi wa Habari, unafanyika Tanga ukiwa na

lengo la kuwafanya wanafunzi wanaosomea uandishi wa habari kufuatilia makosa ya kimaadili yanayojitokeza katika vyombo vya habari kwa vitendo na kuripoti makosa hayo MCT kwaajili ya hatua zaidi.

"Wanafunzi watatakiwa kusoma magazeti, kusikiliza redio na kuangalia TV, na kuainisha makosa ya kimaadili," alisema Mukajanga.

# Wenye ualbino vyuo vikuu wakumbukwa

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Under The Same Sun (UTSS), kupitia mfuko wa Vivian Grace Ash, limetoa kompyuta mpakato kwa wanafunzi 21 wenye ualbino wanaosoma vyuo vikuu mbalimbali nchini ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na masomo yao.

Akikabidhi kompyuta hizo jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa shirika hilo, Berthasia Ladislaus, alisema hiyo ni awamu ya tatu ya utoaji wa kompyuta hizo lengo likiwa ni kuwawezesha kielimu wanafunzi wenye ualbino kusoma bila changamoto.

"Matumizi ya visaidizi hivi hayaepukiki hasa katika ulimwengu wa sasa wa sayansi na teknolojia, wanahitaji kutumia kompyuta kufanya kazi mbalimbali wanazopewa na walimu wao vyuoni," alisema.

"Katika awamu zote tatu za msaada huu jumla ya wanafunzi 53 wenye ualbino wanaosoma vyuo vikuu wamenufaika na msaada huu pamoja na mafunzo ya namna ya kutumia yaliyogharimu shirika zaidi ya Sh. milioni 71," alisema.

Alisema kati ya wanafunzi 21 waliokabidhiwa kompyuta hizo, sita wanachukua masomo ya Shahada ya Uzamili, 11 Shahada ya kwanza na wanne wanasoma Stashahada.

Mkurugenzi huyo alisema ndoto ya mwasisi wa shirika hilo, Peter Ash, ambayo aliinukuu ina "Nina ndoto kwamba siku moja, watu wenye ualbino watachukua nafasi yao inayostahili katika ngazi zote za jamii. Na kwamba siku za ubaguzi dhidi ya watu wenye ualbino zitakuwa ni kumbukumbu iliyofifia," alisema

Ladislaus alisema tangu mwaka 2009 shirika hilo limekuwa likiwapatia ufadhili wa masomo wanafunzi wenye ualbino katika kazi mbalimbali za elimu kuanzia elimu ya awali hadi vyuo vikuu.

Alisema zaidi ya wanafunzi 415 wenye ualbino wananufaika na ufadhili huo ambao ni wa asilimia 100.

"Wanapatiwa visaidizi mbalimbali vya masomo ili kurahisisha masomo yao chuoni kama vikuza maandishi, viona mbali na kompyuta. Hadi sasa waliohitimu ngazi mbalimbali za masomo ni 190 akiwamo aliyepata Shahada ya Uzamivu (PHD)," alisema.

Mnufaika wa kompyuta hizo, mwanafunzi wa Shahada ya Kwanza katika Kitivo cha Sanaa na Elimu, Chuo Kikuu cha Waislam Morogoro (MUM), Nuru Kigeza, alisema vifaa hivyo vitawawezesha kuandaa notisi za kujisomea kwa ukubwa wa maandishi wanayoweza kuyasoma.

Kigeza aliiomba jamii itambue kuwa wao wanaweza kama watu wengine hasa wakipewa nafasi.

Mwanafunzi wa Chuo cha Ushirika, Irene George, anayesoma Shahada ya Ushirika na Maendeleo ya Jamii, alilishukuru shirika hilo kwa kudhamini masomo yao kwa sababu kazi nyingi wanazopewa vyuoni zinahitaji kompyuta.

# Tathmini miradi ya umwagiliaji kufanywa

SERIKALI iko kwenye mchakato wa kufanya tathmini ya kina kwa miradi yote ya umwagiliaji nchini ili kubaini thamani ya fedha na ubora.

Hayo yalibainishwa bungeni jana na Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kondoa Mjini (CCM), Edwin Sannda.

Mbunge huyo alisema Halmashauri ya Mji wa Kondoa imewasilisha andiko la mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika kijiji cha Mongoroma, kata ya Serya takribani miaka mitatu sasa na eneo la ekari 3,000 limetengwa kwa ajili ya mradi huo utakaonufaisha takribani wananchi 12,000.

Kutokana na andiko hilo, Sannda alihoji lini serikali italeta fedha hizo ili mradi huo uanze.

Akijibu swali hilo, Mgumba alisema wataangalia ubora wa miradi na mahitaji halisi ya uboreshwaji, uendelezwaji na kuchagua michache kwa utekelezaji wa ujenzi kwa miradi yenye tija, matokeo na manufaa makubwa kwa wakulima na taifa kwa ujumla.

Mgumba alisema baada ya tathmini hiyo na kutegemea upatikanaji wa fedha serikalini, itahakikisha bwawa hilo na skimu zingine zinajengwa.

"Katika bajeti ya mwaka 2010/11 serikali kupitia idara ya umwagiliaji, ilitoa Sh. milioni 300 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya umwagiliaji ya Kisese, Kidoka na Mangoroma Serya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa wakati huo," alisema.

Mgumba alibainisha kuwa kati ya fedha hizo, Sh. milioni 143.3 zilitumika kufanya upembuzi yakinifu na usanifu katika mradi wa Mangoroma Serya ulioko katika kata ya Serya.

Alisema kazi zilizofanyika ni pamoja na upimaji wa sura ya ardhi, usanifu wa kina, matayarisho ya gharama za ujenzi, tathmini ya rasilimali maji, tathimini ya awali ya mazingira, utafiti wa udongo na masuala ya jamii.

"Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bwawa la Mongoroma Serya ulibaini kuwa bwawa hilo lingegharimu Sh. bilioni nne kwa wakati huo,"alisema.

Aidha, alieleza kuwa bwawa hilo lingekuwa na uwezo wa kumwagilia zaidi ya hekta 3,000 na kunufaisha zaidi ya wakulima 12,000 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, matumizi ya binadamu, unyweshaji wa mifugo na wanyamapori, na ufugaji wa samaki katika vijiji vya Mongoroma, Serya na Munguri.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akimsikiliza Meneja wa Mahusiano ya Serikali kutoka Vodacom Tanzania Plc, Grace Lyon, kwenye usajili mpya wa laini za simu kwa kutumia alama za vidole katika viwanja vya bunge jijini Dodoma. **MPIGAPICHA WETU**

# Kanuni za usindikaji chai kupitiwa

BODI ya Chai Tanzania inafanya mapitio ya kanuni zake kuhusiana na usindikaji wa majani mabichi ya chai, Bunge lilielezwa jana jijini hapa.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, aliyasema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Muheza (CCM), Balozi Adadi Rajab.

Katika swali lake, Mbunge hiyo alisema Sera ya Serikali ya viwanda kuhusu chai hairuhusu wakulima wa zao hilo kufungua viwanda wenyewe ili kuongeza thamani, hivyo kufanya kampuni ya East Usambara Tea Co. Ltd (Eutco) iliyoko Amani-Muheza kuathirika.

Kutokana na sera hiyo, Adadi alihoji kwa nini serikali isiondoe hiyo sera ambayo haiendani na ya viwanda nchini.

Akijibu swali hilo, Manyanya alisema kazi hiyo inafanywa na kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, hivyo matarajio yake ni kuwa litapatiwa ufumbuzi.

Manyanya alifafanua kuwa utaratibu wa kuanzisha viwanda vya chai unafanyika kwa kufuata Sheria ya Chai Na. 3 ya mwaka 1997 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2009 na Kanuni za Chai za mwaka 2010.

"Kwa mujibu wa sheria na kanuni, mwombaji wa leseni ya kuanzisha kiwanda cha kusindika majani mabichi au kuchanganya chai anatakiwa kukidhi vigezo vinavyotakiwa," alisema.

Aidha, alisema mnyororo wa uzalishaji wa chai unahusisha hatua mbili ambazo ni usindikaji wa majani mabichi ili kuzalisha chai kavu na uchanganyaji na uwekaji wa chai kwenye vikasha kwa ajili kuuzwa sokoni.

"Kampuni ya Eutco ni miongoni mwa wakulima wakubwa wa chai nchini yenye viwanda vitatu vya kusindika majani mabichi ya chai ikiwa ni hatua ya awali ya kuongeza thamani kwenye zao la chai kwa ajili ya kuuza kwenye soko la nje na kwenye viwanda vya kuchanganya na kufunga chai kwenye vikasha," alisema.

Kadhalika, alisema kampuni hiyo iliomba leseni ya kuchanganya na kufunga chai kwenye vikasha ikiwa ni hatua ya pili ya kuongeza thamani kwenye zao la chai.

Aidha alibainisha kuwa kutokana na sheria ya chai kampuni ilitakiwa kuanzisha kampuni tanzu kwa ajili ya kutekeleza shughuli hiyo kama ambavyo imeainishwa na sheria husika ya kuchanganya na kufunga chai.

"Kwa utaratibu wa sasa hakuna kampuni ambayo imezuiwa kuchanganya na kufunga chai kupitia kampuni tanzu," alisema.

Manyanya alisema lengo la sera ya maendeleo endelevu ya viwanda ni kuhamasisha ujenzi wa viwanda kwa kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini.




**Habari zote na Augusta Njoji,**
DODOMA

## Wizara yakiri changamoto afya wajawazito na watoto

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekiri kuwapo kwa changamoto katika utekelezaji wa Sera ya Afya kwa kutoa huduma za afya bure kwa wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Hatua hiyo inatokana na kuongezeka kwa wagonjwa na idadi ya watu walio katika makundi maalum na kwamba hali hiyo inasababisha watoa huduma kuwa na idadi kubwa ya watu walio katika makundi maalum wakati rasilimali kwa ajili ya kuwahudumia ni ndogo.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri Dk. Faustine Ndugulile, wakati akijibu swali la Mbunge wa Kaliua (CUF), Magdalena Sakaya.

Katika swali lake, Sakaya alihoji kuwa ni lini serikali itatekeleza kwa ukamilifu Sera ya Afya ya kutoa huduma za afya bure kwa wajawazito kuanzia siku ya kupata mimba mpaka anapojifungua, watoto chini ya miaka mitano na wazee wenye umri zaidi ya miaka 60. Akijibu swali hilo, DK. Ndugulile alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada katika kutoa huduma bora za afya na zenye kufikiwa na watu kwa kuandaa sera na miongozo na kusimamia utekelezaji wake.

Alisema katika kutoa huduma hizo serikali imekuwa ikiyapa kipaumbele makundi maalum kama vile wajawazito, watoto chini ya umri wa miaka mitano, wazee wasio na uwezo na wenye ulemavu kwa kuanzisha sera ya matibabu bila malipo kwa makundi hayo. "Tangu kuanzishwa kwa sera hii serikali imekuwa ikisimamia kwa ukaribu na kuhakikisha inatekelezwa ipasavyo na watoa huduma katika vituo vyote vya kutolea huduma za serikali," alisema Ndugulile.

Alieleza kuwa ili kukabiliana na changamoto hiyo serikali ipo katika hatua za maandalizi ya Mkakati wa Ugharamiaji wa huduma za afya ambao lengo lake ni kuibua vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kugharamia huduma za afya.

Alisema moja ya vyanzo vilivyopendekeza katika mkakati huo ni uanzishwaji wa Bima ya Afya moja ambapo uchangiaji katika Bima hiyo utakuwa ni wa lazima kwa wote walio na uwezo wa kuchangia.



Baadhi ya watalii kutoka nchini China, wakipiga picha za vivutio vya asili katika maboma ya kimasai yaliyopo kwenye Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, mkoani Arusha juzi. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Watalii wa China wafurahia vivutio vya utalii Tanzania

**Na Cynthia Mwilolezi**
ARUSHA

WATALII zaidi ya 300 kutoka nchini China waliofika kutembelea Arusha katika hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro na Serengeti, jana wameondoka kuelekea Zimbabwe, huku wakisifia makundi makubwa ya nyumbu Serengeti na wanyama wa aina mbalimbali.

Ujio wa watalii hao ni matokeo ya kampeni maalum ya kutangaza utalii katika Bara la Afrika iliyopewa jina la Tour Africa The New Horizon.

Ofisa Uhusiano Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Geofrey Tengeneza, alisema jana katika kampeni hiyo watalii hao walipanga kutembelea nchi za Afrika ambazo ni Djibout, Tanzania na Zimbabwe.

"Cha kufurahisha katika kampeni hii ilionekana Tanzania ina vivutio vingi vya asili kuliko nchi hizo zingine na kuamua kukaa siku tano Tanzania na siku moja Djibout walikoanza kutembelea kabla ya kufika nchini na jana wameenda Zimbabwe, ambako watakaa siku mbili," alisema.

Tengeneza alisema mafanikio ya kupata watalii wengi ni utekelezaji wa mpango mkakati wa awamu ya pili wa kuingia katika masoko ya China, India, Israel, Australia na Oman waliojiwekea.

Alisema mkakati wao wa kwanza ulilenga kufikia masoko ya mwanzo ya Marekani, Uingereza, Italia na Ujerumani, nchi ya Israel wameshaleta watalii 1,000 siku na China inatarajia kuleta 10,000 kutembelea vivutio hivyo na wameanza kundi la kwanza na kabla ya Desemba, mwaka huu wote watakuwa wameshafika nchini.

Alisema katika kampeni hiyo Tanzania wataendelea kwenda katika nchi hizo na zingine kuhamasisha utalii na wanatarajia kushirikisha makundi mbalimbali wakiwamo wasanii maarufu, waandishi wa habari na wanamichezo ili watumie makundi hayo kutangaza vivutio hivyo.

Aidha, alisema mkakati wa kuwaleta watalii wengi nchini umeanza kuzaa matunda hivyo wanajitahidi kuboresha miundombinu mbalimbali ya maeneo ya utalii ili kuhakikisha idadi yao inazidi kuongezeka badala ya kupungua.

"Katika kuhamasisha watalii hawa wa nje ya nchi tunapenda kuhimiza watalii wa ndani kutembelea vivutio vyetu na tuache kutegemea watalii wa nje ya nchi sababu kuna madhara yake wakati yanapotokea magonjwa ya mlipuko au vita nchi jirani huwa wanaogopa kutembelea," alisema.

Naye mke wa mfanyabiashara wa duka la vinyago, vito vya Tanzanite na nguo za asili la African Galleria lililopo wilayani Karatu, Sisca Dodhia, aliipongeza serikali na Bodi ya Utalii (TTB) kwa jitihada kubwa za kuleta kundi kubwa la watalii toka China.

"Kweli nimeona matunda hasa wamevutiwa na madini ya Tanzanite kwa wingi sababu wanasema wanayapenda sana," alisema.

Alisema pia kahawa ya Tanzania wamenunua kwa wingi kwasababu wanasema ni bora kuliko zingine wanazotumia.

Kwa upande wake Meneja wa Benki ya NMB tawi la Karatu, Willium Nkuna, alisema wao kama wadau wa fedha waliposikia watalii hao watatembelea duka hilo waliamua kutumia fursa kwa kuhamishia huduma zao hapo.

"Kweli tumewarahisishia huduma wengi wao walikuwa wakitoka kwanza kwetu kubadilisha fedha za kigeni na kuingia duniani kununua bidhaa za vinyago na Tanzanite," alisema.

# PM kufungua mkutano wa wanahisa CRDB

**Na Woinde Shizza,**
ARUSHA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, anatarajiwa kufungua semina ya wanahisa wa Benki ya CRDB na mkutano utakaofanyika leo katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC), jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuhabarisha wanahisa wote nchini, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela, alisema semina hiyo itaanza siku moja kabla ya mkutano mkuu huo.

Alisema mwaka huu Benki ya CRDB imefanya semina kwa wanahisa wake ya kuzitambua fursa mbalimbali zilizopo katika benki hiyo.

Abdulmajid alisema wamekuwa na kawaida ya kukutana kila mwaka kupata taarifa ya utendaji kazi wa benki, mienendo na mikakati yake, lakini elimu ya wanahisa kuzifikia fursa zilizopo imetolewa kwa mara ya kwanza mwaka huu.

Aliongeza kuwa mkutano wa mwaka huu pia utajadili mapendekezo ya gawio na litaidhinishwa na wanahisa hao.

"Pia katika semina hii wajumbe watachagua wajumbe wapya wa bodi ambao watatuwakilisha kuandika wanahisa wenye hisa za chini ya asilimia moja, pamoja na uchaguzi wa mjumbe mmoja wa bodi atakayewakilisha kundi la wanahisa kati ya asilimia moja na sifuri," alisema Nsekela.

# ACFE yapania kupambana na ufisadi duniani

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

CHAMA cha wataalamu waliobobea katika kupambana na ufisadi duniani (ACFE), kimejipanga kuanza kutumia teknolojia za kisasa kubaini na kuchunguza uhalifu huo unaoonekana kushika kasi katika nchi mbalimbali duniani.

Akiongea na waandishi wa habari katika mkutano mkuu wa chama hicho, unaofanyika tawi la Tanzania, jijini Arusha, Rais wa ACFE, Emmanuel Johaness, alisema lengo kubwa la mkutano huo ni kuangalia mapambano ya ufisadi katika siku za usoni kutokana na aina ya ufisadi kuhamia kwenye kiteknolojia zaidi.

Alisema taarifa yao ya mwaka jana 2018 imeonyesha kuwa katika kesi 2,690 za ufisadi zilizoripotiwa kutoka nchi 125 duniani katika sekta mbalimbali 23, imeonyesha kuwa kiasi cha Dola za Kimarekani Sh. billion saba zimepotea, kutokana na ufisadi unaofanyika kwenye taasisi za umma, kampuni na sekta binafsi.

Alisema njia sahihi inayotumika kwa sasa kubaini ufisadi ni pamoja na kupewa taarifa za siri kutoka kwa wananchi wazalendo, pamoja na mafanikio hayo ipo haja kwa chama hicho kupeana mbinu mbadala ikiwamo matumizi ya teknolojia za kisasa kubaini ufisadi.

"Kadiri siku zinavyozidi kwenda ndivyo wahalifu hawa wanazidi kugundua mbinu mpya za kufanya ufisadi na ndio maana katika mkutano huu tumealika mwenzetu kutoka nchi ya Afrika Kusini kuja kutupatia uzoefu wa namna wao wanavyopambana na ufisadi kwa kuwa nchi yao imefanikiwa kwa kiwango kikubwa zaidi na mapambano hayo na walianza muda mrefu kupambana na wahalifu hawa," alisema Johaness.

Alisema kasi ya ufisadi unaoongoza nchini ni pamoja na rushwa, ubadhilifu wa fedha na kughushi na kwamba hatua ya serikali kuanzisha mahakama ya mafisadi itasaidia kupunguza uhalifu huo na kuokoa fedha za serikali kutokana na baadhi ya wahalifu kukutwa na hatia na mali zao kutaifishwa.

Hata hivyo, chama hicho kwa upande wa tawi la Tanzania kimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kubaini matukio ya ufisadi kutokana na wanachama wake zaidi ya 200 kutoka sekta nyeti nchini kufanikisha kupata taarifa za siri na kuzifanyia uchunguzi haraka.

Mmoja wa washiriki kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Salum Kessy, alisema serikali ilipoanzisha mahakama ya ufisadi ni miongoni mwa hatua nzuri kwani hata wao wanavyofanya uchunguzi ukikamilika wanapata pa kuwapeleka wahalifu hao.

Alisema kuwa iwapo Watanzania wataungana kwa pamoja zikiwamo taasisi za kiserikali na binafsi kukemea ufisadi, watapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo hilo na hatimaye kulimaliza kabisa.

Mkutano huo mkuu unafanyika kwa siku tatu nchini na unashirikisha wataalamu kutoka nchi tano za Afrika ambazo ni Kenya, Nigeria, Afrika Kusini, Uganda, Zambia na wenyeji Tanzania.





# DC awaonya wanaCCM wanaoleta upinzani

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amesema baadhi ya wanachama wa Chama cha Mapinduzi (CCM) baada ya kuona upinzani umeisha, kazi waliyobakiza hivi sasa ni kuanzisha upinzani wa ndani kwa ndani kwa kuleta majungu na fitina.

"Hamna adui yuko nje, mmeleta adui ndani. Wananiuliza, Mwenyekiti (Patrick Boisafi) na wewe utaniuliza kwa nini umesema hapa hadharani mambo ya majungu na fitina kwa CCM, nitakwambia ni kwa sababu hayo majungu na fitina hawayafanyi kwenye vikao, wanayafanya hadharani na nina wajibu hadharani," alisema.

Ole Sabaya alitoa kauli hiyo juzi ya kukemea wanaoendeleza majungu na fitina, wakati wa hafla fupi ya kukabidhi gari maalum aina ya 'Toyota Hilux Double Cabin 2.8 D' lililopatikana kwa kushirikisha baadhi ya wadau werevu na mchango wake binafsi kwa ajili ya kukisaidia chama hicho.

Gari hilo litatumika kukisaidia CCM kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji baadaye mwezi Oktoba mwaka huu na uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2020.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nje wanachama wenzangu mnisikilize na ninajua wanachama wa CCM hamtapiga makofi, huko nje vyama vya upinzani, vinavyojiita vyama vya upinzani vimeshakufa vifo vya kawaida, vimekufa vifo vya kawaida kwa nini? Kwa sababu yuko mtu kwenye miaka mitatu iliyopita, kwa ridhaa yenu wenyewe, kwa kupenda kwenu wenyewe, mlienda kwenye masanduku ya kura mkamchagua.

Mambo aliyoyafanya kwa miaka mitatu ni muujiza uliofanyika kwa miaka 50.

"Kwa hiyo upinzani umeisha, tatizo lililobaki Mwenyekiti (Boisafi), sasa baadhi ya wanachama wa Chama cha Mapinduzi, wameona upinzani umeisha, kazi waliyobakiza sasa nao wameanzisha upinzani wa ndani kwa ndani, upinzani wa majungu na fitina.

Hamna adui yuko nje, mmeleta adui ndani."

Ole Sabaya akizungumza mbele ya wana CCM waliofika katika ofisi za chama hicho Wilaya ya Hai, aliwataka wanaoendekeza vitendo hivyo waache majungu na fitina na wala wasiende wakawaiga wale watu wa mataifa ambao wanawajua kwamba wameshindwa kufanya lolote. Jimbo la Hai linaongozwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe.

Aidha, Ole Sabaya amewasihi zaidi wana CCM hao wasihame kwenye mstari wa kawaida na wakawaita wale ambao walishindwa kuanzia mwanzo, huku akiwataka kutekeleza majukumu ambayo ndiyo waliyoiombea serikali ikamate na wakifanya hivyo kamwe hayupo mtu wa kukitoa chama hicho madarakani.

Alisema yeye na baadhi ya wenzake ambao ni wadau werevu na wengine ni watendaji serikalini, wamejichangisha na kuamua kwa ridhaa yao kununua gari iliyokuwapo mnadani kwa Sh. milioni 15 na kisha kuitengeneza na kuwapa CCM kama shukrani yao kwa kazi ya heshima wanayoifanya.

"Hatupangiwi na mimi sipangiwi kwa sababu hii nimeamua kuwapa Chama Cha Mapinduzi, mheshimiwa Mwenyekiti wa mkoa, tunawapa gari hii, mnisikilize...

Tunawapa CCM gari hili liwasaidie kwenda duniani, kusimamia utekelezaji wa ilani kwa serikali iliyochaguliwa na kuwekwa madarakani inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa John Magufuli," alisisitiza Ole Sabaya.



Maofisa usajili laini za simu kutoka kampuni ya Tigo, Regan Emmanuel (kulia) na mwenzake, Jackson Jerry, wakisajili laini za wateja wa kampuni hiyo, kupitia utaratibu mpya ya usajili kwa njia ya alama za vidole katika Mji wa Kiserikali wa Mtumba, jijini Dodoma jana. Kushoto ni afisa wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CIT yaleta neema ya ajira zaidi ya 1,000

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHIRIKA la Kimataifa la Compasion International (CIT), kupitia ushirika wa makanisa wenza limetoa neema ya ajira zaidi ya 1,300 katika miradi yake mbalimbali inayotekeleza nchini kama njia mojawapo ya kuunga mkono juhudi za Rais Dk. John Magufuli kupunguza changamoto hiyo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Taifa wa CIT, Agness Hotay, shirika hilo limefanikiwa kutekeleza ndoto yake ya kushiriki katika kupunguza pengo la ajira kwa kutengeneza ajira hizo na kuchangia pato la taifa.

"Shirika linaamini katika uelewa wa kumfunza mtu kuvua, badala ya kumpatia samaki, ndio maana hata kaulimbiu yetu mwaka huu ni wekeza kwa vijana na watoto kwa uchumi endelevu, kwa kuwa tunaamini uchumi imara unategemea nguvu kazi ya vijana," alisema Hotay.

Aliongeza: "Mpaka sasa huduma yetu ya kuwakomboa watu masikini imewafikia vijana 135,750, lakini pia kupitia makanisa wenza tumetoa ajira zaidi ya 1,300 hivyo kushiriki katika kuondoa uhaba wa ajira kwa kutengeneza ajira na kuchangia pato la taifa."

Shirika hilo liko katika mikoa 19 ya Tanzania Bara ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Kigoma, Manyara, Pwani, Morogoro, Iringa, Dodoma, Kilimanjaro, Singida, Shinyanga,Mwanza, Mara, Tabora, Lindi, Geita, Mtwara, Simiyu na Kagera.

Katika Mkoa wa Kilimanjaro, miradi inayotekelezwa kupitia makanisa wenza imo katika Kata za Orkolili na Karansi katika Wilaya ya Siha na msitu wa tembo uliopo mpakani mwa Wilaya ya Moshi na Simanjiro mkoani Manyara.

Miradi iliyoibuliwa na kufadhiliwa na Shirika hilo katika Wilaya ya Siha ni wa ufugaji wa kuku chotara ambao mwaka 2017 unaendeshwa na kinamama wa huduma ya kunusuru pamoja na kanisa.

Mkurugenzi wa Kituo cha PEFA Olkolili cha Wilaya ya Siha ambacho kipo chini ya Kanisa la PEFA (Pentecostal Evengelist Fellowship of Africa Church), Lespice Kiguge alisema:

"Mpaka sasa Compassion International Tanzania, wameshatupa kiasi cha Sh. milioni 91,190,000 kwa ajili ya kujengea maktaba ya kisasa ambayo baada ya kukamilika na kuanza kutumika imekuwa faida kwa jamii ya Orkolili, kwa watoto walioko katika kituo hiki na pia shule yetu ya Ekenywa English Medium School."

"Mradi mwingine tuliowezeshwa na Compassion International Tanzania kwa kutupatia kiasi cha Sh. 34, 000,000 ni wa ujenzi wa choo cha kisasa cha matundu manane ambacho kimekuwa msaada mkubwa kwa jamii ya wafugaji.'

## Utafiti wabaini wananchi hawaridhiki huduma ya maji

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

UTAFITI uliofanywa na Shirika la kiraia la Kinshai linalotekeleza mradi wa ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (PETS), katika Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, unaonyesha kuwa asilimia kubwa ya wananchi hawaridhiki na huduma pamoja na maendeleo ya miradi ya maji katika maeneo yao.

Mkurugenzi Mkuu wa Kinshai, Veronika Shao, akizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalum kuhusu utafiti huo, alisema wananchi hao wameonyesha kukosa imani na miradi hiyo kutokana na kuwapo kwa miundombinu ya maji, lakini haina maji na wakati mwingine miundombinu ni mibovu kiasi cha kutotoa maji.

"Yapo mambo mengi wanayolia nayo ikiwapo pia maji kuwa kidogo na kutolewa kwa mgawo. Hivyo kwa kuzingatia hayo wananchi wanasema bado hawaridhishwi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya maji," alisema.

Kuhusu changamoto za jumla ambazo wananchi wa Mwanga wanakumbana nazo katika sekta ya maji, Mkurugenzi huyo ameeleza kuwa utafiti huo umebaini katika Kata ya Mgagao kunaweza kupita siku mbili hadi tatu bila wananchi kupata huduma ya maji.

Mwezi Aprili mwaka huu, mradi huo wa PETS uliwasilishwa kwa wadau wa maji, ripoti yake ya matokeo ya utafiti kuhusu tathimini ya thamani ya fedha kwenye shughuli mbalimbali zinazofanywa kwa kutumia rasilimali za umma ili kuongeza utawala bora na uwajibikaji kwenye sekta ya maji katika Wilaya ya Mwanga.

Ripoti hiyo pamoja na mambo mengine, imeibua changamoto mbili kubwa ambazo ni ushiriki mdogo wa wananchi katika masuala ya maji na kukosekana kwa taarifa za mapato na matumizi.

Mradi huo wa PETS katika miradi ya maji ya Wilaya ya Mwanga, unatekelezwa na Shirika la Kinshai, kwa ufadhili wa Shirika la The Foundation for Civil Society.



Ukurasa 18

Jaji atathmini mtihani kinamama waliojiajiri kuingia Hifadhi Jamii



Ukurasa 20

DRC: Mji wa Kisangani wakabiliwa na mgawo wa umeme

# BUFE

Ijumaa Mei 17, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Mjasiriamali aliyeajiriwa afunguka neema kuwepo vitambulisho vipya

Ukurasa 19



### UDSM YAWEKEZA BIL 1/- KWENYE UTAFITI

# Pinda awaambia kioo cha taaluma yao, fimbo inayokomboa mipango uchumi

**Na Salome Kitomari**

KATIKA taasisi ya elimu ya juu yoyote, sifa na wajibu wake mkuu ni uwezo wake katika kufundisha, kutafiti na kuishauri kitaaluma. Wasifu wa wataaluma wake, pia wanaofunzwa unapimwa katika vigezo vya ubora katika eneo hilo.

Katika eneo la utafiti, kunajulikana kuwa nyenzo muhimu katika kutatua matatizo ya jamii husika au ile itakayoomba kuhudumiwa.

Hicho inakifanya kuwa moja ya kipimo chenye upekee katika kutathmini chuo chochote cha elimu ya juu; namna wanafanya tafiti, kuzichapisha na matatizo ya jamii duniani kote, ikiwemo maendeleo ya nchi husika.

Ni jambo linaofanya sifa ya taaluma wake ni kufanya utafiti na kuchapisha kwenye machapisho ya ndani na nje ya nchi, hasa katika majarida ya kitaaluma. Ndivyo vigezo pia vinavyopandisha hadhi ya chuo husika.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Biashara Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

## Biashara

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

| | |
|---|---|
| Mauzo | 109,584,255.00 |
| Hisa | 58,317 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

‘BAIBAI’ PLAN KIBAHA

# Miaka 22 wameisogeza K kutoka umasikini wa kija

• Yaondoka ikiwaacha wanavijiji wapya • Wafugaji kukeketa ‘no’;



Mwenyekiti wa Plan International, Nigel Chapman, (katikati) akiwasikiliza wanufaika wake wa Kibaha (hawapo pichani). **PICHA: MTANDAO**



Wanafunzi wanufaika katika halfa ya kuliaga Shirika la Plan International Kibaha. **PICHA: ZUWENA SHAME**

**Na Zuwena Shame, Kibaha**

UMASKINI unatajwa kuwa changamoto kubwa katika kuleta maendeleo na haki za mtoto wa kike. Hapo yanaingia masuala ya elimu, kusikilizwa, kulindwa na kuheshimika katika jamii nchini.

Mkurugenzi wa shirika la Plan International Ukanda wa Kusini mwa Afrika, Charles Businge, anasema katika miaka ya 22 shirika lake lilipoanza kuendesha miradi yake mkoani Pwani, umaskini ndio changamoto kubwa kwa wakazi.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi miradi ya kijamii kwa serikali na kufunga uendeshaji miradi hiyo mjini Kibaha mkoa Pwani, anasema matokeo yake hali hiyo, ni kusuasua maisha ya kazi wengi mkoani humo.

Businge anasema, shirika hilo limekuwa likifanya shughuli mbalimbali za kijamii na kimaendeleo, ikiwamo kuinua maisha ya mtoto wa kike, wanawake na vijana.

> “**Matokeo haya yalifikia maamuzi yetu ya kufunga utekelezaji wetu wa miradi hapa, ili kutoa fursa.**

Bosi huyo wa Plan International, anasema katika miaka 22 tangu aipoanza kufanya miradi mkoani humo, umaskini ndio changamoto kubwa kwa wakazi wa mkoa, hivyo kufanya shughuli za maendeleo kusuasua kwa wakazi wengi.

Anasema umaskini ukichangiwa na mila na desturi potofu za makabila mbalimbali mkoani Pwani, zimekuwa zikikwamisha elimu na haki za mabinti wanaoozwa katika aumri mdogo.

Businge anasema, suala la masomo ni kitu kilicho kinyume na ukiukwaji haki za mtoto, hasa haki kubwa ya kupata eimu.

**PLAN & SERIKALI**

Anasema kwa kuona changamoto hiyo, Plan International, kwa kushirikiana na serikali za mitaa na watekelezaji wa kujitoa (community volunteers) wilayani Kibaha, waliwawezesha wazazi, kuhusu umuhimu wa elimu.

Anasema, hilo la kuinua watoto wa kike, wamelifanya kwa kujenga vyumba vya madarasa 108 na nyumba za walimu 18, vyoo vya kisasa na bora 287 na ofisi za walimu zipatazo 11, mtazamo mkuu ni kuiboresha elimu.

“Katika kumwezesha mtoto wa kike na kumrahisishia masomo, tulijenga bweni la wasichana kwenye Shule ya Sekondari ya Ruvu Station, anasema na kufafanua lengo kuu:

“ Ili kuwapa nafasi za kujisomea zaidi hasa nyakati za usiku na kuwaepusha na vishawashi mbalimbali, hasa ikizingatiwa umbali wa shule na makazi ya wanafunzi hao.”

Anataja baadhi ya miradi mingine inayoweza kusaidia elimu wilayani humo, ni pamoja na ujenzi wa shule za awali kwa watoto wanaojiandaa kujiunga na shule ya msingi, ujenzi wa vituo sita ya elimu ya awali wa watoto chini ya umri wa miaka mitano na uwanja wa watoto katika Shule za Msingi Ruvu JKT na Msongola.

**UMASKINI VS AFYA**

Anataja ukombozi dhidi ya unyonge na umaskini katika mtazamo wa afya, Plan Intenational imejenga zahanati sita katika maeneo ya Magindu, Ruvu, Ngeta, Mwanabwito, Kikongo, Visiga na Mlanidizi, ikiendana na

UCHUMI

DRC: Mji wa Kisangani wakabiliwa na mgawo wa umeme Mei 13, 2019

Ukurasa 20

UCHUMI

Jaji atathmini mtihani kinamama waliojiajiri kuingia Hifadhi Jamii

Ukurasa 18


BIASHARA

Mjasiriamali aliyeajiriwa afunguka neema kuwepo vitambulisho vipya

Ukurasa 19

# ...ibaha ...miii

## ...wote wachumi



nyumba za watumishi wa afya, ili kuwajengea uwezo na ufanisi kazi, wilaya Kibaha.

**ELIMU YA UJASIRIAMALI**

Anaongeza kuwa katika kupunguza umaskini wilayani humo, shirika la Plan International ikishirikiana na serikali, waliweza kutoa mafunzo mbalimbali na kuwawezesha wazazi kwa elimu ya ujasiriamali na kuwaunganisha na taasisi za serikali, zilizowapatia mikopo wa kujiwezesha kiuchumi.

"Tuliona fursa kuwa, ili kuondokana wanafunzi hasa wa kike kukatishwa masomo yao, ni bora wazazi wawe na vyanzo vya mapato, ambavyo ni endelevu. Hivyo, mafunzo ya ujasiriamali na mikopo ndio suluhisho ya tatizo hili kwa wazazi" anasema Businge.

Anarejea mwaka 2015, Plan International ilifanya utafiti kutathmini miradi yake mkoani humo na matokeo yanaridhisha kwa kuwapo na mafanikio makubwa hadi sasa, ikilinganishwa na awali mwaka 1996 ilipoanza kazi zake.

"Matokeo haya yalifikia maamuzi yetu ya kufunga utekelezaji wetu wa miradi hapa, ili kutoa fursa.

"Pia, katika mikoa mingine, Tanzania yenye uhitaji, tunatumiani jitihada zetu na ushirikiano ulioonyeshwa Kibaha, utakuwa endelevu na jamii zitaendeleza ari ya kustawisha haki za watoto na usawa wa msichana" anasema Businge.

Anasema, shirika hilo linaelekeza nguvu zake kwenye mikoa mingine yenye uhitaji zaidi, lengo kuu ni kumpatia elimu na haki mtoto hasa wa kike, usawa, haki, kulindwa, kushirikishwa na uwezo wa kujieleza.

"Huu sio mwisho wetu wa kuisaidia Kibaha, pakitokea fursa zingine za kuwekeza kwenye miradi mingine, basi tuko tayari kuendelea na wananchi wa maeneo haya" anaongeza.

**UKATILI WA MABINTI**

Businge anataja miaka 22 waliofanya kazi Kibaha, wameiona changamoto ya ukatili na ukeketaji kwa mabinti kutoka makabila ya wafugaji.

Aidha, anasema wana ushuhuda wa ndoa za ututoni, jambo ambalo Plan International liliweka juhudi za ziada, kuchangia kutokomeza ukatili huo.

Ofisa Kibaha

Kaimu Ofisa Tarafa wa Kibaha, Anthony Mhango, anaelekeza rai yake kwamba, vijana wilayani humo kuendeleza mafunzo na ujuzi waliopata kutoka shirika la Plan International, ili wamudu kujikimu kimaisha na kuondokana na umaskini.

Katika hotuba yake kwa niaba ya Ofisa Tarafa, Assumpta Mshami, Mhango anasema Plan International imeweza kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa vijana , hivyo hawana budi kuendeleza ujuzi walioupata kwa kujitafutia kipato, ili waondokane na umaskini.

"Leo Plan (International) wanatuachia miradi hii mikononi. Hakuna muda wa kupoteza kwa kukaa vijiweni na kufungia vifaa ndani. Fanyieni kazi ujuzi na kuvitunza vifaa mlivyosaidiwa na shirika hili, kwani wameona umuhimu kwa kumuwezesha na kumuendeleza kijana kiuchumi," anatamka Mhango.

Pia, anawataka wafugaji na wakulima wilayani humo kuacha tabia ya kuingialiana mipaka, badala yake wae kitu klmoja kwa kuheshimiana na uhusiano mzuri.

Anakiri katika miaka 22 ya kuwapo Plan, imewawezesha vijana wa kike 974 na wavulana zaidi ya 833, kujiunga na Chuo cha Maendeleo ya Ufundi Stadi (VETA) na kuwapatia vifaa vya kuanzia kazi baadhi yao ni waliokatisha masomo yao kwa kuwapeleka.

Mhango anasema: "Tunawashukuru Plan, kwani sio tu vijana wanaweza kujipatia kipato chao kwa sasa, pia wanaweza kulipa kodi, kitu ambacho ni chema kwa wilaya yetu na taifa kwa jumla."

Anasema, kwa sasa jukumu linalobaki kwa serikali na wana - Kibaha, ni kuenzi miradi kwa kuiboresha na kuwa na misingi imara ya kuijenga Kibaha kiuchumi.

Ushauri wake kwa wakazi wa Kibaha, ni kwamba wanatakiwa kutathmini michango ya shirika hilo kwa kuwa na mipango endelevu, kuanzia pale Plan International ilikoishia, kwa manufaa ya sasa na vizazi vya baadae Kihaba.

**MWENYEKITI WAFUGAJI**

Mwenyekiti wa Jamii ya Wafugaji, anayehusika na miradi ya elimu ya Plan International, Lenetica Kavuki, anasema shirika limewasaidia wafugaji kielimu na haki ya mtoto wa kike.

Kavuki anasema, kabla ya shirika hilo kuingia wilayani humo, mabinti wafugaji walifanyiwa ukatili mkubwa wa kijinsia, wakikeketwa ambapo na takribani watoto zaidi ya 150 walikeketwa kila mwaka.

Anasema, Plan ilipoliona hilo, ilianza kutoa semina kwa wazazi jamii ya Kimasai kuwafahamisha namna wanavyokiuka haki za mtoto wa kike kupitia ukatili huo wa kabila lao.

Mwenyekiti huyo anaongeza kuwa, hadi shirika hilo linaondoka wilayani Kibaha, hakuna hata mtoto mmoja wa kike anayefanyiwa ukatili huo, kwani elimu na uelewa umekuwa mkubwa miongoni wa jamii ya wafugaji.

Anaongeza kuwa, Plan International imewajengea shule za awali watoto wao wanaosoma, hivyo kudhibiti tabia ya kuhama miongoni mwao, kwani watoto wao wanahitaji kusoma na imedhibiti wazazi kuhama ovyo.

**WATOTO WAIBUKA**

Katika kile kinachoonekana kuiva kichocheo cha kijamii dhidi ya umasikini kupitia miradi ya Plan International, Kibaha, baadhi ya watoto wa shule za msingi walifika kwenye hafla ghafla na 'kufunguka' walio nayo moyoni.

Anasema, kwa sasa wanajua haki zao kama kulindwa, wajiamini na kujieleza, vilevile wamekuwa wakishirikishwa kufanya maamuzi katika ngazi za kifamilia.

Wanafunzi hao waliliomba shirika la Plan International kuendelea kuwapo Kibaha, kwani limewasaidia kwenye suala la elimu, afya, kuwajengea madarasa, vifaa vya shule vya kusomea na kufundishia, zahanati na magari ya kubeba wagonjwa.

Shirika hilo lilianza utekelezaji wa miradi yake nchini mwaka 1991 na lipo katika mikoa 13.

# Watumishi Wamarekani wahamishwa ghafla Irak



Watumishi Wamarekani, katika Chuo Kikuu cha Irak. **PICHA: MTANDAO**

WIZARA ya Masuala ya Kigeni nchini Marekani, imeagiza kuondoka kwa watumishi wake wanaoelezwa 'hawafanyi kazi za dharura' nchini Irak, baada ya kutokea hali ya wasiwasi kati ya Marekani na Iran.

Wafanyakazi katika ubalozi ulioko mjini Baghdad na walioko katika balozi wa mji wa Irbil, wametakiwa kuondoka haraka iwezekanavyo.

Ni hatua inayochukuliwa, huku taifa la Ujerumani likisitisha mafunzo ya wanajeshi wake nchini Irak.

Jeshi la Marekani linasema kuwa siku ya Jumanne iliyopita, vitisho hivyo huko Mashariki ya Kati vilitolewa kutokana na ujasusi unaohusu vikosi vinavyoungwa mkono Iran katika eneo hilo.

Ni maamuzi yanayochukuliwa, kinyume na matamshi ya mwanajeshi Mwingereza, mwenye cheo ngazi ya Jenerali aliyekana kuweko vitisho vya aina yoyote kuongezeka.

Chris Ghika, ni Naibu Kamanda wa Muungano wa Majeshi dhidi ya kundi la wapiganaji wa Islamic State , anasema hatua zilizochukuliwa kuwalinda wanajeshi wa Marekani na washirika wao, kutokana na vikosi vinavyoungwa mkono na Iran nchi ya Irak na Syria zinatosha.

"Tunajua, uwepo wao na tunawachunguza pamoja na wengine, kwa sababu hayo ndio mazingira tuliopo kwa sasa,' anaongezea.

Msemaji wa jeshi la Marekani, baadaye alikanusha matamshi ya Jenerali Ghika akisema kuwa yalienda kinyume na vitisho vilivyotambuliwa na Marekani na mashirika yake ya kijasusi.

Idara ya ulinzi nchini Ujerumani inasema siku ya Jumatano kwamba jeshi la Ujerumani lilisitisha mipango ya mafunzo yake nchni Irak.

Msemaji wake anasema kulikuwako tahadhari miongoni mwa wanajeshi wake 160 wanaohusika katika operesheni hiyo.

BEI YA MAZAO >> MCHELE 184375/- | ULEZI 142642.9/- FEDHA >> RAND 164.66 | KSH 22.75 | USH 0.61

UCHUMI

UDSM YAWEKEZA BIL 1/- KWENYE UTAFITI

# Pinda awaambia kioo cha taaluma yao, fimbo inayokomboa mipango uchumi

• Asimulia 1980 ilivyobeba viwanda nchini • Prof. Ndalichako 'awanong'oneza' mbinu • Ajenda nzima inajibu Tanzania ya Viwanda

**Na Salome Kitomari**

KATIKA taasisi ya elimu ya juu yoyote, sifa na wajibu wake mkuu ni uwezo wake katika kufundisha, kutafiti na kuishauri kitaaluma.

Wasifu wa wataaluma wake, pia wanaofunzwa unapimwa katika vigezo vya ubora katika eneo hilo.

Katika eneo la utafiti, kunajulikana kuwa nyenzo muhimu katika kutatua matatizo ya jamii husika au ile itakayoomba kuhudumiwa. Hicho inakifanya kuwa moja ya kipimo chenye upekee katika kutathmini chuo chochote cha elimu ya juu; namna wanafanya tafiti, kuzichapisha na matatizo ya jamii duniani kote, ikiwemo maendeleo ya nchi husika.

Ni jambo linaofanya sifa ya taaluma wake ni kufanya utafiti na kuchapisha kwenye machapisho ya ndani na nje ya nchi, hasa katika majarida ya kitaaluma. Ndivyo vigezo pia vinavyopandisha hadhi ya chuo husika.



Mgeni rasmi, Mkuu wa Kitengo cha Uratibu Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Aida Juma (kushoto), akipatiwa maelezo na Mtafiti wa Mwani, Dk. Flower Ezekiel, Msuya kuhusu utafiti wa zao hilo.

### KINACHIOFANYIKA UDSM

Kutokana na umuhimu wa utafiti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kimekuwa na maonyesho ya wiki ya utafiti chini ya kaulimbiu "utafiti kwa maendeleo jumuishi na endelevu"; Mtazamo ni kuwaleta pamoja watafiti mbalimbali, ambao ni wahadhiri na wanafunzi.

Maonyesho hayo yaliyopewa jina la 'Wiki ya Tano' yalilenga kuamsha umuhimu wa utafiti kwenye vyuo mbalimbali. Katika kujali hilo, UDSM imetenga bajeti ya Sh. bilioni moja katika mwaka wa fedha 2019/2020.

### MIZENGO PINDA

Waziri mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, aliyefungua maonyesho hayo, anasema historia ya maendeleo katika nchi Kusini mwa Afrika, inaonyesha ina mwelekeo wa kupendelea wachache kwa kuzingatia hali za uchumi, kijamii, kikabila na kijinsia, ikiwaacha walio wengi.

Anasema, kupitia hilo, utafiti unatoa suluhisho. Wakati serikali iliyopo madarakani hivi sasa ikisisitiza maendeleo ya viwanda ni lazima yawe jumuishi.

Pinda ambaye ni mhitimu mkongwe wa UDSM, anasema kwa wingi wa rasilimali zilizopo, matokeo ya utafiti kutoka vyuo vikuu yanaonyesha hatua kubwa ya kuimarisha ustawi wa kiuchumi na kijamii.

"Serikali iko makini kuhakikisha Watanzania wanafahidi matunda

> **"Tutakuwa na wahitimu ambao watatumia ujuzi na maarifa kwa kujiajiri wenyewe, kuajiri vijana wenzao au kuajirika katika fani nyingine kwa urahisi.**

ya maendeleo, kupitia matumizi bora na upatikanaji wa rasilimali za taifa unalenga kuboresha miundombinu, uzalishaji, elimu, huduma za afya, maji na upatikanaji wa fedha.

"Tunahitaji kujenga ukuaji jumuishi wa uchumi utakaoboresha kiwango cha maisha ya Watanzania wote," anasema.

Pinda, anakumbusha uwekezaji katika mpango wa maendeleo ya nchi unahitaji kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za umma na hilo ni jambo linalohitaji mwongozo wa kazi za utafiti.

"Baadhi huamini utafiti na ubunifu ni jambo la gharama kubwa na kuliepuka kabisa. Binafsi, nauchukulia ni rasilimali inayoweza kutumiwa kimkakati kuboresha maisha ya Watanzania," anasisitiza.

### AJENDA YA UTAFITI

Pinda anataja ajenda ya utafiti wa UDSM ya mwaka 2018 iliyoidhinishwa na Baraza la Chuo katika kuchagua mapendekezo ya utafiti yanayofadhiliwa kupitia fedha za ndani, linahakikisha tafiti zinakidhi mahitaji ya taifa.

"Nawaomba watafiti ambao tayari wamenufaika na ruzuku ya utafiti katika awamu ya kwanza, watumie fedha vizuri katika kufanya utafiti utakaoleta matokeo yenye manufaa kwa jamii ya Watanzania, kwa kuzingatia malengo na muda uliopangwa," anasema.

Anataka UDSM kujipanga kuboresha sera, kuhuisha miundombinu ya utafiti na ubunifu, kupangilia na kusimamia raslimali za utafiti na ubunifu ikiwamo rasilimali watu na kubadili desturi za kitaaluma zilizopitwa na wakati.



Waziri Mkuu Mstaatu, Mizengo Pinda, akikagua bidhaa katika mabanda ya maonyesho ya utafiti, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

### UDSM KONGWE

Pinda anasema, katika miaka ya 1980 hadi 1990, UDSM ilikuwa na taasisi za utafiti na ubunifu, zilizofanya kazi nzuri kutatua changamoto zilizopo na kuchangia maendeleo ya nchi, hali iliyoiletea chuo heshima kubwa.

"Mfano ni Taasisi ya Bidhaa ya Ubunifu, ambayo ilijikita kubuni na kusambaza teknolojia zilizotumiwa na wananchi katika shughuli za uzalishaji. Kilikuwa kipindi kigumu kiuchumi kwa nchi kwa kuwa kulikuwa na uhaba wa bidhaa za sabuni, mafuta ya kupikia na sukari.

"Taasisi hii ilibuni tekonolojia na kutengeneza mashine ambazo zilitumiwa na wananchi vijijini kutengeneza bidhaa kwa kutumia malighafi walizozalisha," anasema.

Anasema, taasisi hiyo ilitoa huduma muhimu kwa viwanda na kutengeneza vipuri mbadala wa vilivyoagizwa nje kwa gharama kubwa ya fedha za kigeni.

"Huu ulikuwa ni mfumo wa mzuri wa uchumi endelevu wa viwanda. Nasikitika kuwa halikuendelea na ninaamini lilituturudisha nyuma. "Ninawaomba wataalamu kufanya tafakuri ya kina kubaini palipokosewa na kuchukua hatua na kurekebisha mapungufu, ili kuhakikisha wanawezesha shughuli za utafiti na ubunifu zinashamiri zaidi chuoni," anasema.

### ELIMU ILIYOPO

Pia, Pinda anasema kumekuwapo mjadala mkubwa duniani na hasa kwa nchi zinazoendelea, kuhusu aina ya elimu inayotolewa na vyuo vikuu na shule za sekondari, pia mbinu zinazotumika kufundishia.

"Vyuo vingi duniani hasa katika nchi zinazoendelea, baada ya kubaini elimu ya darasani isiyo na uwiano na uhalisia wa kimaisha ina matatizo, vimeamua kufuata mfumo wa elimu ya juu, unaolenga kuingiza masuala ya ubunifu na ujasiriamali katika mitaala ya masomo na kutumia mbinu ya ufundishaji ambayo inatumia utatuzi wa changamoto halisi," anasema.

Hivyo, anaishauri UDSM kuongeza kasi ya kutumia mbinu hiyo kwa kuwa ndiyo njia pekee itakayowasaidia kukitangaza chuo, kikazalisha wahitimu bora watakaotoa mchango mzuri katika jamii na maendeleo ya tafiti kwa ujumla.

"Tutakuwa na wahitimu ambao watatumia ujuzi na maarifa kwa kujiajiri wenyewe, kuajiri vijana wenzao au kuajirika katika fani nyingine kwa urahisi," anasema Pinda.

" Ni hatua iliyokuja kwa wakati kuonyesha umma matokeo ya utafiti ulifanywa na chuo ili kuchochea ufahamu na ushirikiano baina ya chuo na serikali, sekta binafsi na wadau wengine wa ubunifu na utafiti," anasema.

Waziri Mkuu Pinda anasema ni vyema vyuo vikuu nchini vikatambua kushirikisha umma katika matokeo ya utafiti, ili kuongeza uhusiano baina yao na tasnia mbalimbali na kuvutia rasilimali za kufanya tafiti na kufungua fursa za ushirikiano ndani na nje ya nchi.

### UCHAPISHAJI TAFITI

Waziri wa Elimu, Sayansi, Tekonolojia na Ufundi, Profesa Joyce Ndalichako, ambaye mwanataaluma zao la kilichokuwa Kitivo cha Elimu cha UDSM, rai yake kwa vyuo vya elimu ya juu nchini, kutenga bajeti ya utafiti, kupitia ada za wanafunzi.

"Kupanga ni kuchagua. Chagueni kufanya utafiti. Nasisitiza hili, kwa kuwa kila mwaka kunakuwapo taasisi inapanga vyuo bora na vyuo vyetu havishiki nafasi nzuri. Kitaaluma tuko vizuri lakini kinachotuangusha ni kutokufanya utafiti na kuchapisha," anasema.

Profesa Ndalichako, anatahadharisha kuwapo uwezekano utafiti kuishia kwenye maonyesho na haziendi kwenye machapisho ya kitaaluma, hivyo ni vyema waongeze machapisho katika majarida ya kitaifa na kimataifa.

Anasisitiza, umuhuimu wa wahitimu kuwa na uwezo wa kutatua changamoto za jamii kutokana na elimu yao, na kuondoa dhana "wahitimu wana vyeti vizuri lakini hawawezi kutatua changamoto za jamii."

### SAFARI YA UTAFITI

Makamu Mkuu wa UDSM, Profesa William Anangisye, anasema wametenga fedha Sh. bilioni moja kwa ajili ya utafiti, utakaowasaidia kujifunza ugunduzi, uvumbuzi ili kufanya maamuzi mazuri na sahihi, kwa maendeleo ya binadamu na taifa.

Awali, Mkuu wa Utafiti wa UDSM, Profesa. Cuthbert Kimambo, anasema wiki ya kwanza ya maonyesho ilifanyika mwaka 2015, ikiwa na kaulimbiu ya matumizi ya matokeo ya utafiti kwa maisha bora na kulikuwapo miradi 126 ya utafiti, bidhaa na huduma zilizoonyeshwa katika ngazi ya vitengo na 57 ya chuo.

Anasema mwaka 2016, kaulimbiu ilikuwa utafiti kwa Maendeleo ya Viwanda Tanzania, iliyokuwa na jumla ya miradi 141, iliyojumuisha bidhaa na huduma ikijumuisha maeneo mbalimbali ya UDSM: Shule Kuu na taasisi, vitengo na miradi 61 ngazi ya chuo.

"Idadi hii inakuwa mwaka hadi mwaka na hamasa kwa wanataaluma na wanafunzi kushiriki inakuwa mwaka hadi mwaka, mwaka huu miradi ngazi ya vitengo walionyesha matokeo ya utafiti na jumla ya miradi 309 na 100 inaonyeshwa katika ngazi ya chuo.

## Biashara katika picha




Meneja Uhusiano Mawasiliano Benki ya TPB, Chichi Banda (wa pili kushoto), akikabidhi moja ya mfuko wa vyakula vyenye thamani ya Sh. milioni moja na nusu kwa Mkuu wa Kitengo Maalumu cha Wanafunzi Wenye Ulemavu wa Akili katika Shule ya Msingi Mtambani Boko, Asaph Rukamo Maerere, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Wanaoshuhudia ni walimu wa kitengo hicho. **NA MPIGAPICHA WETU**



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NIC Tanzania, Margaret Karume (kulia), akibadilishana mawazo na wateja wa benki hiyo, katika futari iliyoandaliwa na benki hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**



Wachuuzi wa maparachichi wakisubiri wateja kando ya Barabara ya Kawawa, eneo la Ilala Boma, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MIRAJI MSALA**

BEI YA MAZAO >> MAHINDI 52625/-| MAHARAGE 170000/-

UCHUMI

# Jaji atathmini mtihani kinamama waliojiajiri kuingia Hifadhi Jamii

- Wapigania '50 kwa 50' iliyotimia kazini
- Wadai stahiki inayofanana na kazi zao




Mwenyekiti wa Majaji Wanawake Tanzania, Jaqulin Dimera, akifungua kampeni za 'Ajira Sawa, Ujira Sawa, Tuko Pamoja' katika viwanja Vya TGNP Mtandao, jijini Dar es Salaam, hivi karibuni. **PICHA: YASMINE PROTACE**

**Na Yasmine Protace**

INAPOZUNGUMZIWA kazi au ajira, majukumu yake yanaangukia katika tafsiri kwamba; shughuli yoyote halali ambazo zinampatia mtu kipato.

Katika makundi ya kazi, zipo za kuajiriwa na zingine za kujiajiri, zote zikilenga kujiingizia kipato. Hivyo, mtu akifanya kazi halali, anaangukia katika kunufaika na kipato halali na kazi isiyo halali kama vile wizi, kipato chake kinakuwa batili.

Dhana ya kazi, ina upana mkubwa sana katika jamii. Moja ya masharti yake ya msingi ni watu kutobezana katika shughuli wanazofanya.

Hivi hayo yaliibuka karibuni katika uzinduzi wa kampeni za wanawake zilizokuwa na kaulimbiu ya "Ajira Sawa; Ujira Sawa;Tupo Pamoja' zilizozinduliwa katika viwanja vya TGNP Mtandao.

Mratibu mkuu wa kampeni hizo ni asasi isiyo ya kiserikali ya Action Aid Tanzania, kwa kushirikiana na wadau wengine wa asasi zisizo za serikali: Tawla, TCTA, WILDAF, TGNP Mtandao ,Oxfam na Wilac.

Mkuu wa Programu wa Action-Aid Tanzania, Jovina Mawenzeke, anasema kuwa kampeni hiyo ya kitaifa, inagusa masuala ya kitaifa, ikiwamo masuala ya wanawake kupata haki sawa za ajira.

> **"Mimi mkono wangu nilikatwa panga, nikitoka kufanya biashara. Toka hapo mpaka sasa mkono wangu hauwezi kubeba kitu kigumu.**

Anasema maudhui ya kampeni husika inashughulikia mambo manne, yanayohusu wanawake kuwamo katika ajira, kwani hadi sasa katika ajira wanawake bado ni wachache, kuliko wanaume, hivyo hakuna haki sawa.

Inaelezwa, baadhi ya wanawake hadi sasa hawapewi mikataba ya ajira, kutokana na aina ya kazi wanazofanya, huku baadhi ya wanawake wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kutunza familia.

Jovina analalamika kuwa, jukumu hilo analobeba la kutunza familia limekuwa haithaminiwi na kumnyima thamani mwanamke.

"Serikali inatakiwa iangalie wanawake wapatiwe elimu, ili kuwapunguzia mzigo wa kazi," anasema na kuongeza kuwa, kuna haja ya kinamama ambao wana majukumu kama ya mamalishe na wauza mboga, wawekewe ulinzi katika maeneo yao ya kazi.

Kuhusu sekta ya ajira, Jovina anasema kunapaswa kuangaliwa katika usawa kati ya wanaume na wanawake na nguvu za watu wengi zitumike katika kumpunguzia mzigo wanawake.

Hapo anahimiza kwamba sheria zinazolinda haki za wafanyakazi zitekelezwe na ikiwamo upatikanaji wa kazi za sitaha zipatikane kwa wanawake.

**MDAU TGNP**

Mdau kutoka asasi ya TGNP Mtandao, Gema Akilimali, anasema kampeni hiyo itaendeshwa kwa kipindi cha miaka mitatu, akiwasifu kinamama kuwa ndio wanatumia nguvu nyingi katika uzalishaji.

Anasema wanawake pamoja na kuwa wachapakazi, bado matunda ya kazi zao hazijatambulika kikamilufu na anaongeza:"Uzinduzi wa kampeni ya wanawake 'Ajira Sawa, Ujira Sawa, Tupo Pamoja' utaleta mabadiliko katika masuala ya kuutambua mchango wa mwanamke katika kazi anazofanya, ikiwamo upatikanaji haki sawa katika maeneo ya kazi."

**JAJI DIMERO**

Mgeni rasmi katika uzinduzi wa kampeni hiyo, Joqulin Dimero, Mwenyekiti wa Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania, anasema siku ya wafanyakazi ni miongoni mwa siku muhimu kwa kuangalia wafanyakazi walipotoka na wanapoelekea.

Anasema katika baadhi ya nchi duniani, haki za ajira zinatofautiana kutokana na mazingira ya nchi husika. Anataja tamko la Shirika la Kazi Duniani (ILO), ni maelekezo ya kuhakikisha haki za wafanyakazi zinalindwa na serikali ya Watanzania kwa kuthamini wafanyakazi, inathamini haki za wafanyakazi.

Anaongeza Tanzania ina wanawake wasio na ajira rasmi na aina hiyo ya ajira zimechangia wanawake kushindwa kuingia katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na anakosa mikopo.

Jaji Dimelo anasema, wafanyakazi wanatakiwa kuangalia changamoto wanazokutana nazo katika ajira umefika wakati muafaka kuungana na kujua haki zao.

Pia, alitumia fursa hiyo, kuipongeza ILO kutimiza umri wa miaka 100 ya kuanzishwa kwake, kutokea zama za Vita Kuu vya Dunia.

**USHUHUDA**

Ramla Ally, mkazi kutoka Kigoma, kilio chake ni kwamba wanawake wapatiwe ulinzi, kutokana na mkoa aliyotoka kuwapo vitendo vya kubakwa wanawake, kupigwa na kuporwa mali zao.

Anasema, baadhi ya wanawake wafanyabiashara wa Kigoma, wamekuwa wakinyanyasika kwa matukio ya kikatili, pale wanapokuwa wanatoka kufanya biashara.

"Mimi mkono wangu nilikatwa panga, nikitoka kufanya biashara. Toka hapo mpaka sasa mkono wangu hauwezi kubeba kitu kigumu," anasema.

**KUTOKA OXFAM**

Samwel Masiale, ni Meneja Mawasiliano kutoka shirika la Oxfam, anayesema kuwa kampeni hizo zinaendeshwa ili kuleta haki sawa katika ajira na imelenga kuwatambua wanawake walio katika ajira rasmi na zisizo rasmi na kutompa mwanamke mzigo mkubwa wa kimajukumu.

"Kutambua umuhimu wa mwanamke katika kazi anazofanya na zina mchango kwa jamii," anasema Misale na anaongeza kwamba, kuna kazi ambazo zimekuwa zikifanywa na kinamama, pasipo kulipwa maslahi stahiki au kutolipwa kabisa.

Anasema, asasi yake ya Oxfam wanalizingatia hilo na usawa kwa wanawake wakiwamo mamalishe wasiokuwapo katika ajira. Anashauri watunga sera wawaangalie, ili nao wapate bima za matibabu.

Samwei anahitimisha kwa ushauri kwamba jamii itambue umuhimu wa ajira sawa kwa wanawake.

FEDHA >> USD 2,300.96| Pauni 3,011.73| Euro 2,595.25

# Mjasiriamali aliyeajiriwa afunguka neema kuwepo vitambulisho vipya

• Mwalimu, aongoza chama, mshereheshaji

**Na Mwandishi Wetu,** Kongwa

KATIKA kujiinua kiuchumi, ni kawaida watu kuwa na shughuli zaidi ya moja ya kumuingizia kipato ili kukimu mahitaji ya kimaisha. Nini siri yake na ina tafsiri gani kimaisha?

Nipashe, ilifanya mazungumzo na mmoja wa watu wa wanaofanya shughuli za namna hiyo na siri ya mafanikio yake. Huyo, Katibu wa Chama cha Walimu Tanzaia (CWT) wa Wilaya ya Kongwa, Shaaban Tessua.

Mazungumzo ya 'Ana kwa Ana' yalichukua sura ifuatayo:

**Swali: Ni vyema kujua historia yako ya maisha kwa ufupi na unafanya nini?**

**Jibu:** Mimi ni mwalimu kwa taaluma. Nimefundisha kwa zaidi ya miaka 10 katika Shule ya Msingi Mwendapole wilayani Kibaha. Kwa sasa ni Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) wilaya ya Kongwa, nikitokea Halmashauri ya Mji wa Kibaha mkoa wa Pwani.

**Swali: Ukiacha kazi ya Katibu wa Chama cha Walimu, unajihusisha na shughuli gani nyingine?**

**Jibu:** Ni mpambaji na mshereheshaji wa sherehe za kijamii na za kiserikali kwa zaidi ya miaka 15 sasa. Kwa kifupi, ni mjasiriamli.

**Swali: Unaionaje sekta isiyo rasmi katika kuchagiza ukuaji wa uchumi?**

**Jibu:** Sekta isiyo rasmi ni muhimu sana kwa ukuzaji wa uchumi. Ni faraja kuona serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Dk. John Pombe Magufuli, ikiipa umuhimu na msukumo wa kipekee katika kuhakikisha sekta hiyo inakuwa mdau muhimu katika maendeleo ya nchi.

Ni sekta inayotoa mwanya na fursa kwa wananchi wengi kushiriki katika uzalishaji mali ambao unasaidia katika kukua kwa uchumi kuanzia ngazi ya familia hadi Taifa.

Muhimu ni kuwajengea wananchi uelewa kuhusiana na dhana nzima ya kujitegemea kuanzia mashuleni, vyuoni na kwinginekoko, ili kuondokana na dhana ya kuajiriwa badala ya kujiajiri.

**Swali: Rais Dk. Magufuli ametoa vitambulisho maalum kwa wajasiriamali wadogo, ili viwasaidie katika shuguli zao. Unahisi vitasaidia katika kuwainua wajasiriamali?**

**Jibu:** Nampongeza Rais wetu kwa kubuni vitambulisho vya wajasiriamali wadogo, ambao mitaji yao haizidi (shilingi) milioni nne kwa mwaka. Vitambulisho hivi vinaonyesha nia njema aliyokuwa nayo Rais Magufuli ya kuwainua wajasiriamali wadogo, ili wafanye biashara zao kwa uhuru na kuepukana na usumbufu waliokuwa wakiupata kutoka kwa watendaji mbalimbali wa serikali wanaokusanya ushuru.



Wakazi wa Kongwa, katika moja ya tukio linalowahusu. **PICHA: MTANDAO.**

Hakika vitambulisho hivi vimewanusuru wajasiriamali na utitiri wa kodi ambao ulikuwa ni kikwazo katika biashara zao.

**Swali: Baadhi ya wajasiriamali wanadaiwa kukwepa kuchukua vitambulisho hivi, unawashauri nini?**

**Jibu:** Natoa rai kwa wajasiriamali kutokukwepa kuchukua vitambulisho hivi, kwani vinaondoa usumbufu usio wa lazima.

Pia gharama za kulipa ushuru kila siku ni kubwa kuliko kulipia shilingi elfu ishirini (20,000) tu kwa mwaka. Hivyo, wakjitokeze kwa wingi kuchangamkia vitambulisho kwa ustawi wa biashara zao na kwa maendeleo ya nchi.

**Swali: Ni changamoto gani zinazokabili zoezi la ugawaji wa vitambulisho vya wajasiriamali?**

**Jibu:** Zipo changamoto kadhaa. Kwanza, wapo wafanyabiashara wakubwa ambao wanatumia mwanya huu kukwepa kulipa kodi.

Pili, Wapo wajasiriamali ambao tayari wana leseni za biashara kama vile bodaboda, taxi, wanajikuta wanalazimishwa kuwa na vitambulisho hivyo, jambo ambalo naona sio sahihi na hili limejitokeza katika baadhi ya maeneo. Ni vyema serikali ikazitatua changamoto hizi haraka.

**Swali: Taasisi za fedha ni mhimili muhimu wa kuwasaidia wajasiriamali, nini wito wako kwa taasisi za fedha?**

**Jibu:** Taasisi za fedha zina mchango mkubwa sana kwa wafanyabiashara wadogo. Kwanza, wana jukumu la kuwapa wajasiriamali elimu ya biashara ili waweze kujikita katika bishara zenye tija.

Pili, kuwapa mikopo yenye riba na masharti nafuu, ili wajasiriamali waweze kuanzisha na kuendeleza biashara zao. Hivyo basi, taasisi za fedha ni wadau mkubwa kwa maendeleo wa wajasiriamali na ya nchi.

**Swali: Baadhi ya wajasiriamali wanalalamikia mazingira wanayofanyia biashara zao kutokuwa rafiki na kuchangia kushusha mapato yao. Hili unalizungumziaje?**

**Jibu:** Ni kweli baadhi ya wajasiriamali wanafanya bishara zao katika mazingira yasiyo rafiki. Naishauri serikali kuweka miundombinu iliyo rafiki kwa wafanyabiashara, ili waweze kuvutiwa kulipia vitambulisho wakitegemea kupata huduma bora katika maeneo yao ya kazi.

Serikali pia ihakikishe maeneo wanayoyaandaa kwa ajili ya wajasiriamali yawe yanafikika kwa urahisi, ili waweze kupata wateja kwa ajili ya bidhaa zao.

> **"Serikali pia ihakikishe maeneo wanayoyaandaa kwa ajili ya wajasiriamali yawe yanafikika kwa urahisi, ili waweze kupata wateja kwa ajili ya bidhaa zao.**

Ni vyema pia, serikali ikatenga asilimia ndogo ya mapato yanayotokana na vitambulisho vya wajasiriamali katika kuboresha mazingira wanayofanyia kazi wajasiriamali, ili ufanyaji biashara uwe katika mazingira safi na yenye kuwavutia wateja.

**Swali: Wapo maofisa biashara katika halmashauri zetu zote nchini, nini mchango wao katika kuwasaidia wafanyabiashara na wajasiriamali nchini?**

**Swali: Ni kweli tunao maofisa biashara katika halmashauri zetu. Maofisa hawa wana mchango mkubwa katika kuwahamasisha wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa ili kuwawezesha kupanua uelewa zaidi katika masuala ya biashara, upatikanaji wa masoko na walaji wa bidhaa zao.**

Hii itaharakisha ukuaji wa uchumi kwa kupata masoko na kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Swali: Unadhani wajasiriamali wadogo wana mchango kufanikisha Tanzania ya viwanda?**

**Jibu:** Ndio. Wana mchango mkubwa sana wa kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 kwa kuungana pamoja, ili kukuza mitaji na kukopesheka kirahisi.

Pia, wanaweza kuzalisha bidhaa kwa ajili ya kulisha soko la ndani na nje, ili kupata fedha za kigeni. Wajasiriamali wanaweza kushiriki kikamilifu katika kuzalisha malighafi zitakazotumika viwandani, kwa ukuaji wa viwanda, ajira na uchumi.


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Aprili 18, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Geita | Morogoro | Kagera | Kilimanjaro | Kigoma | Lindi | Manyara |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 57000 | 70000 | 53000 | 57000 | 48000 | 60000 | 40000 | 45000 | 80000 | 60000 |
| Mchele | 200000 | 210000 | 195000 | 130000 | 165000 | 185000 | 180000 | 160000 | 200000 | 200000 |
| Mtama | 40000 | 60000 | 35000 | 180000 | 71000 | 100000 | 80000 | 100000 | 150000 | 42000 |
| Uwele | 40000 | 60000 | 34000 | 180000 | 71000 | 110000 | NA | 100000 | NA | 100000 |
| Ulezi | 72000 | 140000 | 75000 | NA | 155000 | 150000 | 180000 | 150000 | 200000 | 120000 |
| Ngano | 87000 | 130000 | 160000 | 180000 | 163000 | NA | 98000 | 150000 | NA | 120000 |
| Maharage | 150000 | 220000 | 170000 | 170000 | 185000 | 150000 | 180000 | 140000 | 200000 | 130000 |
| Viazi Mviringo | 70000 | 80000 | 66000 | 70000 | 82000 | 75000 | 50000 | 90000 | 100000 | 60000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia April 3, 2019

| | Dsm | Arusha | Kibaha | Dodoma | Geita | Iringa | Bukoba | Mpanda | Kigoma | Moshi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petrol | 2,147 | 2,192 | 2,151 | 2,206 | 2,312 | 2,211 | 2,363 | 2,355 | 2,378 | 2,181 |
| Diseli | 2,192 | 2,196 | 2,196 | 2,250 | 2,357 | 2,256 | 2,407 | 2,400 | 2,423 | 2,186 |
| M'taa | 2,096 | 2,286 | 2,101 | 2,155 | 2,262 | 2,161 | 2,312 | 2,304 | 2,328 | 2,276 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Aprili 23, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,482.82 | -0.18 |
| DSEI | 2,020.08 | -12.15 |
| Thamani za Hisa (bln) | 19,471.20 | |
| Mauzo | 16,751,775.00 | |
| Hisa | 47,125 | |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| ACA | 4,640 | -6.26% |
| KA | 110 | -4.35% |
| EABL | 4,840 | +0.83% |
| JHL | 9,250 | +1.09% |
| DSE | 1,280 | +98.46% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,578.38 | 2,605.09 |
| USD | 2,278.12 | 2,300.91 |
| KES | 22.57 | 22.75 |
| GBP | 2,986.62 | 3,017.64 |

## Bei za hisa hadi kikao cha Aprili 23, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| ACA | 4,640.00 | 4,950.00 | -6.26 |
| CRDB | 125 | 125.00 | 0 |
| DCB | 340 | 340 | 0 |
| DSE | 1,280 | 1,300 | -1.54 |
| EABL | 4,840.00 | 4,800.00 | 0.83 |
| JHL | 9,250.00 | 9,150.00 | 1.09 |
| KA | 110.00 | 115.00 | -4.35 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| KCB | 1,020.00 | 1,020.00 | 0 |
| MBP | 490.00 | 490.00 | 0 |
| MCB | 500.00 | 500.00 | 0 |
| MKCB | 800.00 | 800.00 | 0 |
| MUCOB | 400.00 | 400.00 | 0 |
| NICO | 170.00 | 170.00 | 0 |
| NMB | 2,340.00 | 2,340.00 | 0 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| NMG | 1,500.00 | 1,400.00 | 0 |
| PAL | 400.00 | 400.00 | 0 |
| SWALA | 490.00 | 490.00 | 0 |
| SWIS | 1,700.00 | 1,700.00 | 0 |
| TBL | 10,000.00 | 10,000.00 | 0 |
| TCC | 17,000 | 17,000.00 | 0 |
| TCCL | 600.00 | 600.00 | 0 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 2,244.52 | 2,262.51 |
| UGANDA SHS | 57.47 | 61.52 |
| RWANDAN FRANC | 251.53 | 254.42 |
| BURUNDI FRANC | 218.12 | 219.77 |
| USD | 227,818.81 | 230,097.00 |
| POUND STG | 294,911.45 | 297,952.61 |
| EURO | 254,906.47 | 257,547.57 |
| CANADIAN $ | 169,470.22 | 171,114.00 |
| SWITZ. FRANC | 223,724.65 | 225,873.17 |
| JAPANESE YEN | 2,037.37 | 2,057.56 |
| SWEDISH KRONOR | 24,245.07 | 24,479.71 |
| NORWEG. KRONOR | 26,497.34 | 26,760.76 |
| DANISH KRONOR | 34,148.58 | 34,484.89 |
| AUSTRALIAN $ | 160,133.84 | 161,758.19 |
| INDIAN RPS | 3,258.88 | 3,290.44 |
| PAKISTAN RPS | 1,532.78 | 1,620.40 |
| ZAMBIAN KWACHA | 18,043.25 | 18,334.42 |
| MALAWIAN KWACHA | 289.17 | 309.43 |
| MOZAMBIQUE-MET | 3,537.56 | 3,567.40 |
| ZIMBABWE $ | 42.63 | 43.49 |
| SDR | 316,030.26 | 319,190.56 |
| GOLD (T/O) | 289,729,234.68 | 292,691,184.29 |
| S. AFRICAN RAND | 15,829.33 | 15,980.62 |
| UAE DIRHAM | 62,028.65 | 62,636.99 |
| SINGAPORE $ | 167,513.83 | 169,126.79 |
| HONK KONG $ | 29,049.63 | 29,338.63 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 60,751.68 | 61,354.29 |
| KUWAIT DINAR | 748,788.21 | 756,002.76 |
| BOTSWANA PULA | 21,141.59 | 21,537.08 |
| CHINESE YUAN | 33,906.65 | 34,229.93 |
| MALAYSIA RINGGIT | 55,228.80 | 55,713.56 |
| SOUTH KOREA WON | 197.63 | 199.26 |
| NEWZEALAND | 150,519.89 | 152,117.13 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **24/Apr/2019** | **2.30** | **2,307.00** | **2,298.50** | **2,300.97** |
| 23/Apr/2019 | 6.25 | 2,309.00 | 2,300.00 | 2,300.95 |
| 18/Apr/2019 | 11.55 | 2,308.00 | 2,292.00 | 2,300.90 |
| 17/Apr/2019 | 2.20 | 2,308.00 | 2,298.45 | 2,300.94 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **24/Apr/2019** | **70,700** | **5.75** | **5.00** | **5.17** |
| 23/Apr/2019 | 37,000 | 5.75 | 5.00 | 5.41 |
| 18/Apr/2019 | 43,000 | 6.00 | 5.00 | 5.45 |
| 17/Apr/2019 | 41,200 | 5.50 | 5.00 | 5.29 |
| 16/Apr/2019 | 53,550 | 5.50 | 4.90 | 5.24 |
| 15/Apr/2019 | 18,450 | 6.00 | 5.25 | 5.44 |

# DRC: Mji wa Kisangani wakabiliwa na mgawo wa umeme



Mji Kisangani katika picha tofauti. **PICHA: MTANDAO**

SEHEMU kubwa ya mji wa Kisangani, mji wa tatu kwa ukubwa DRC, haina umeme tangu Alhamisi iliopita.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mamlaka ya huduma za umeme DRC, SNEL, ukosefu huo wa umeme umesababishwa na kuharibika kwa injini mbili zinazo-saidia bwawa la maji la Kisangani linalozalisha umeme.

Taarifa hizo zinasema, hivi sasa injini moja pekee ndiyo inafanya kazi. Kufuatia hali hiyo, kiwango cha nguvu za umeme kimeshuka kutoka kwenye megawati 10 hadi megawati 3 na hivyo kuilazimu mamlaka ya umeme kuanzisha mgawo katika kutoa huduma hiyo.

Wakazi wa mji wa Kisangani wanalalamika wakisema uhaba wa umeme umezorotesha shuguli nyingi kwenye viwanda, hospitali na zahanati, na imeleta hofu kubwa kwa wakazi wa Kisangani wanaotumia chakula kina-chohifadhiwa kwenye jokovu.

Makolo Kotambula, mkazi wa mji wa Kisangani, ameiambia Sauti ya Amerika kwamba, moja ya athari kubwa ya mgawo huo ni kuwa vyumba vya kuhifadhi maiti kwenye baadhi ya hospitali havifanyi kazi.

Mamlaka ya umeme SNEL imesema katika taarifa yake kwamba, wakati shughuli za ukarabati wa injini zilizoharibika zikiendelea, kiwango kidogo cha umeme kinachopatikana kitapelekwa kwenye vituo muhimu, hususani hospitali na zahanati.

Mamlaka hiyo imeahidi kuwa katika kipindi cha wiki moja, umeme utakuwa umerudi katika mji wa Kisan-gani.

Wakazi wa Kisangani wanaiomba serikali kuu kununua injini mpya na kukarabati bwawa la mji wa Kisangani. **DW**





# Mafuriko yaleta maafa Kyela

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya wananchi 2,500 katika Kata nane za Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wameyahama makazi yao huku wengine watano wakipoteza maisha baada ya kukumbwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, Ofisa Tawala wa Wilaya hiyo, Salome Magambo, alisema athari za mafuriko katika wilaya hiyo zilianza kuonekana Aprili 29, mwaka huu, katika kata za Matema na Bujonde.

Alisema mafuriko yaliyoleta athari zaidi yalianza kutokea Mei 4, mwaka huu na yalivamia makazi ya watu na kusomba mali mbalimbali ikiwemo mifugo, chakula na mavazi hali iliyoilazimu serikali kuanza kuwahamisha wanaoishi mabondeni.

Magambo alisema baada ya kufuatilia katika maeneo mbalimbali yaliyoathirika na mafuriko, walibaini kuwa watu watano walikuwa wamefariki dunia kwa kusombwa na maji yalioyotokana na mvua hizo.

"Tumeanzisha kambi 14 kwenye maeneo yaliyokumbwa na mafuriko. Kambi zenyewe ziko maeneo ya kwenye shule na makanisa ambako tumewahifadhi wananchi 2,570, lakini wengine wamehifadhiwa na ndugu zao," alisema Magambo.

Alisema mbali na serikali kuanzisha kambi hizo, pia imewapatia chakula waathirika hao pamoja na dawa za kutibu maji ili kuepuka magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu.

Alizitaja kata zilizoathirika zaidi kuwa ni Ikama, Katumba- Songwe, Mwaya, Talatala Kanjunjumele, Matema, Makwale na Bujonde na kwamba katika baadhi ya maeneo hayo nyumba za wananchi zimezingirwa na maji na zingine zimebomoka.

Ofisa huyo alisema chanzo cha mafuriko hayo ni mvua zinazoendelea kunyesha hasa katika Wilaya ya Rungwe kwa madai kuwa maji yote yanakimbilia Kyela ambako ni bondeni.

Hata hivyo, aliwashukuru baadhi ya wadau wakiwemo wafanyabiashara wa Wilaya ya Kyela na taasisi mbalimbali za serikali zilizojitolea kushirikiana na Kamati ya Maafa ya Wilaya kuwasaidia wananchi walioathirika na mafuriko hayo.

Nipashe ilipita katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo yaliyoathirika na mafuriko na kushuhudia baadhi ya wananchi wakiwa wamepiga kambi kwenye maeneo ya shule na makanisa wakisubiri maji yapungue ili warejee katika maeneo yao.

Katika kijiji cha Masebe kilichoko katika Kata ya Mwaya, barabara hazipitiki na wananchi wanadai mafuriko hayo yamesomba mifugo yao, chakula na katika Shule ya Sekondari Masebe simenti iliyokuwa imehifadhiwa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa imeharibika.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Simon Mwakibuje, alisema mpaka sasa wamebaini kuwa ng'ombe watano wamekufa na wengine ambao bado idadi haijafahamika hawajulikani walipo huku kuku waliokufa wakifikia 2,000.

Alisema kutokana na mazingira kuwa magumu waliamua kuwahifadhi wananchi kwenye vyumba vya madarasa vya Shule ya Msingi Masebe na katika makanisa ili kusubiri maji yapungue.

"Kwa sasa tunaiomba serikali itusaidie chakula maana hapa wananchi wangu hawana chakula, chakula chote kimeharibiwa na mafuriko na sasa hivi hata njia hazipitiki na mashambani kumejaa maji kabisa," alisema Mwakibuje.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Masebe, Daniel Anosisye, alisema kutokana na hali ya mafuriko waliamua kusitisha masomo kwa wanafunzi wa madarasa ya kuanzia darasa la kwanza mpaka la sita ili wabaki nyumbani.

Alisema baadhi ya vyumba vya madarasa wanaishi wananchi na vingine maji yaliingia na kuharibu vitu mbalimbali vilivyokuwemo ikiwemo daftari za wanafunzi na vitabu.

"Hata hawa wanafunzi wa darasa la saba wamekuja hapa kwa sababu wanafanya mtihani wa moko wa Mkoa, lakini kama mnavyoona hata hapa shuleni maji yamejaa kila kona na wenzetu waliokumbwa na mafuriko tumewapatia vyumba wanaishi hapa," alisema Anosisye.



Wafanyabiashara wa mbuzi, wakisubiri wateja katika mnada wa Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana. Mbuzi mmoja aliuzwa kwa bei ya 60,000/- hadi 150, 000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JOHN BADI**

# Waonywa kuingiza mifugo mashambani

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIONGOZI wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wametakiwa kuhakikisha mifugo haingii kwenye mashamba ya mpunga ambayo inavunwa ili kuepuka migogoro ya wakulima na wafugaji.

Agizo hilo lilitolewa jana kwa Wenyeviti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa, wilayani Mbarali na Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya mji huo, Tuntufye Chamba, wakati akizungumza na wenyeviti wa mitaa wa mamlaka ya mji.

Chamba alitoa agizo hilo baada ya kuwapo malalamiko ya wafugaji kuanza kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima.

Alisema wafugaji wanaotajwa kuingiza mifugo kwenye mashamba wanatumia kisingizio cha kutumia malisho ya mashamba yaliyovunwa lakini wakulima wanalalmika kuwa mifugo inavuka na kuingia kwenye mazao ambayo bado hayajavunwa.

Ofisa Mtendaji huyo alisema katika kipindi hiki ambacho bado wakulima wanendelea na uvunaji wa mpunga, ni vyema mifugo ikazuiwa kuingizwa kwenye mashamba yote mpaka pale shughuli za mavuno zitakapomalizika na kama ni kuruhusu iwe ni ridhaa ya wakulima wote.

"Hatutaki migogoro kwenye mji wetu baadhi ya sehemu tuna wafugaji na kwingine kuna shughuli za kilimo hasa mpunga,pande hizi mbili lazima tuzisimamie ili tusiingie kwenye migogoro," alisema.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji huo, Chameta Godigodi, alikiri kuwapo malalamiko ya baadhi ya wenyeviti kutumia madaraka yao kuruhusu mifugo kuingizwa kwenye mashamba yaliyovunwa huku yaliyo jirani yakiwa bado hatua inayoleta migogoro kwakuwa mifugo huingia hadi kwenye mashamba hayo.

Aliwataka wenyeviti kuwa na msimamo katika kutekeleza majukumu yao huku wakitambua kuweka usawa kwenye uamuzi wa mambo yao kutasaidia kuwa na jamii tulivu na isiyo na migogoro itokanayo na muingiliano usiofuata misingi.

Nao baadhi ya wenyeviti wa mitaa ya mamlaka ya mji huo, walisema wako baadhi yao ambao wamekuwa wakiendekeza rushwa ya kupokea fedha kutoka kwa wafugaji na kuwashawishi wakulima waliovuna mapema mpunga kuruhusu mifugo ilishwe kwenye mashamba yao pasipo kuwajali wenzao wanaokuwa bado kukamilisha shughuli ya uvunaji.

# Wadaiwa kupora na kujeruhi watu

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WANANCHI wa Kata za Saza na Mkwajuni wilayani Songwe, wameliomba Jeshi la polisi kuwashughulikia watu wanaojiita walinzi wa maduka ya Saza kwa madai ya kuvamia, kujeruhi na kunyang'anya mali za raia, hali inayohatarisha amani na utulivu.

Wakizungumza juzi kuhusu hali halisi ya usalama katika kata hizo, baadhi ya wananchi walisema kuwa wanalazimika kuwahi kufunga biashara zao wakihofia kuvumiwa na kuporwa mali zao.


Miongoni mwa watu waliojeruhiwa na kikundi hicho ni Amos Kimbra ambaye alidai kupigwa hadi kuvunjika mguu wa kushoto huku mguu wa kulia ukitobolewa kwa vitu vyenye ncha kali.

Alisema tukio hilo lilimtokea wiki moja iliyopita akiwa njiani kwenda nyumbani majira ya saa nne usiku. Alisema kundi hilo lilimvamia na kumjeruhi baada ya kukataa kutoa fedha za mauzo kutoka dukani kwake.

"Mpaka sasa nimepata kilema baada ya kupigwa na kundi hilo la walinzi ambao wanalinda maduka yetu wengine tunawafahamu kwa lakini tumekuwa waoga kuripoti kwani tunapata vitisho, tunaomba Jeshi la Polisi liingilie kati suala hili," alisema Kimbra.

Wananchi wengine walieleza kuwa matukio hayo huambatana na wahalifu kufunga barabara kwa lengo la kutekeleza uhalifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, alikiri kuwapo kwa matukio ya uhalifu na watu kupigwa katika kata za Saza na Mkwajuni na kwamba alitoa maelekezo kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Songwe kuchukua hatua.





# Ukatili kwa wanawake, watoto waongezeka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UKATILI dhidi ya watoto na wanawake umezidi kuongezeka nchini na imebainika kwamba mashauri 16,832 ya migogoro ya ndoa yameripotiwa katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai, mwaka jana hadi Machi, mwaka huu.

Idadi ya mashauri imeongezeka kwa asilimia 34.5 ikilinganishwa na mashauri 13,282 yaliyoripotiwa katika kipindi cha mwaka 2017/18.

Hayo yalibainishwa juzi jijini hapa na Mkurugenzi wa Idara ya ya Watoto katika Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Mwajuma Magwiza, alipokuwa akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani yaliyofanyika kimkoa.

Alisema katika familia nyingi nchini changamoto kubwa ambayo imekuwa ikizikabili ni kukithiri kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake.

Magwiza alisema vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vimeongezeka katika familia nyingi nchini huku wahusika wa matukio hayo wakiwa wanafamilia au watu wa karibu na watendewa. "Kwa mujibu wa taarifa za Jeshi la Polisi kwa mwaka 2017, inaonyesha kuwa matukio ya ukatili 13,457 yaliripotiwa ikiwemo wa kingono 3,583 na mimba za utotoni 1,323," alisema.

Pia alisema taarifa hiyo inaonyesha mikoa ya kipolisi yenye takwimu kubwa za ukatili ni Kinondoni (2,426), Dodoma (1,283), Tanga (1,064), Temeke (984) na Arusha (972).

"Migogoro hiyo si tu inaathiri ukuaji wa familia bali pia inachangia kurudisha nyuma maendeleo ya familia na taifa kwa ujumla," alifafanua Magwiza.

Pia alisema vitendo hivyo kwa kiasi kikubwa vinatokana na mmomonyoko wa maadili kwa familia na kutokuwajibika kikamilifu kwa wazazi kunakosababisha migogoro ya ndoa.

Alitaja changamoto nyingine kuwa pamoja na kukosekana kwa usawa kunakoongeza migogoro katika familia zinapopambana na kuondokana na umaskini.

"Vijana walio katika balehe wanaoishi katika kaya maskini mara nyingine wanajiingiza katika hatari nje ya familia zao ili wapate vitu au yale wasiyoweza kuyapata nyumbani kwao," alisema.

Pia alisema kuhamahama kwa wazazi kunakosukumwa na mahitaji ya kiuchumi na sababu zingine husababisha familia kuwa mbali na ndugu na matandao wa jadi wa kijamii pia huchangia familia kutokuwa na ubora wa kutimiza wajibu kikamilifu.

Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Dodoma, Happynes Mgaluka, akizungumza katika madhimisho hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, alisema jamii inatakiwa kuachana na mila potofu.

Alisema katika maeneo mengi bado pamekuwapo na ukatili dhidi ya watoto na wanawake hasa katika kuwanyima kinamama haki ya kumiliki ardhi na kuwaozesha mabinti katika umri mdogo.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), wakiwaongoza wabunge kupata futari aliyowaandalia katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma juzi. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

## Aomba msaada wa mil. 2/- matibabu viungo vya mwili

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MTOTO Jackilin Kusenha (6) anaomba msaada wa Sh. milioni mbili kutoka kwa wasamaria wema ili kupata matibabu ya ugonjwa wa kupooza viungo vya mwili unaomsumbua toka kuzaliwa kwake.

Akizungumza kwa niaba yake, mama wa mtoto huyo Angel Kusenha (35), alisema fedha hizo anaziomba ili kwenda kutibiwa katika Hospitali ya Mlali, Kongwa mkoani Dodoma.

Kusenha alisema fedha hizo ni kwa ajili ya matibabu na mazoezi ya viungo.

"Ninawaomba wasamaria wema kiasi hicho cha Sh. milioni mbili ili kumsaidia mtoto wangu anayetakiwa akatibiwe hospitali ya viungo Mlali kutokana na tatizo alilonalo ambalo linamfanya kukosa usingizi kwa muda wote wa usiku na mchana,"alisema.

Alisema tangu kuzaliwa kwa mtoto wake huyo, kila usiku mchana akitaka alale ni lazima apewe vidonge ili kupata usingizi.

Alisema pamoja na jitihada zilizofanyika za kumpeleka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma na CCRT, Dar es Salaam, huko kote kunahitajika fedha kwa ajili ya gharama za matibabu.

Kusenha aliomba Mtanzania yeyote atakayeguswa kwa ajili ya kumsaidia mtoto huyo, atume fedha hizo kupitia namba **0753043217** au **0653331440** au **0717540711.**

# Wazazi waonywa kutumia watoto kuomba omba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imekemea tabia ya wazazi kuwatumia watoto kuombaomba misaada mitaani kwa madai kuwa wanawajengea tabia mbaya ikiwamo kuwanyima haki yao ya msingi ya elimu.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi Msaidizi wa Wizara ya Afya, Maendeleo Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Sebastian Kitiku, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani.

Alisema kumekuwa na desturi ya watoto kuomba fedha na misaada mingine katika maeneo ya mijini jambo ambalo linapaswa kupingwa vikali na wazazi na walezi. "Kundi hili ni miongoni mwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ambao wanahitaji malezi, matunzo na ulinzi kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 16 cha Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009,"alisema Kitiku.

"Ili kukabiliana na hali hii, jamii inapasa kuacha kuwatumia watoto katika kuomba na kushiriki katika biashara hatarishi na kuwazuia watoto kushiriki katika matukio yanayofanyika usiku katika kumbi za sherehe, starehe na kwenye baa," alisisitiza.

Aidha, alisema mamlaka za serikali za mitaa zinatakiwa kutunga sheria ili kutokomeza tabia ya watoto kushirikishwa katika mikusanyiko ya usiku. Alisema halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, wanapaswa kuweka utaratibu wa kuwasaidia wazazi na walezi kuanzisha shughuli za kujiongezea kipato ili kumudu majukumu ya familia.

Kitiku alisema Sheria ya Mtoto Na. 21 ya 2009 kifungu cha 17, inakataza mmiliki wa baa au ukumbi wa starehe kuruhusu mtoto kushiriki shughuli yoyote katika maeneo hayo.

Adhabu kwa kosa hilo, alisema faini zisizopungua Sh. milioni moja na zisizozidi Sh. milioni tano au kifungo kisichozidi miezi 12 au vyote kwa pamoja.

Kitiku alifafanua kwamba kifungu cha 158 (1) (c) kinakataza watoto kushiriki katika matukio yanayofanyika usiku yakiwamo harusi, maonyesho ya fasheni na matukio mengine kama hayo na adhabu kwa mkosaji ni faini isiyopungua Sh. 500,000 au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.



## BARAZA LA WAWAKILISHI



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Ussi, akiwasilisha bajeti ya makadirio na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2019/2020, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanaomiliki misumeno ya moto waagizwa kuisalimisha

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ali Ussi, amewataka wananchi wanaomiliki misumeno ya moto kuisalimisha kwa vyombo vya sheria. Alisema misumeno hiyo haikubaliki, na kwamba serikali imeshapiga marufuku matumizi yake ambayo yamekuwa yakichangia uharibifu wa mazingira.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali liloulizwa na Mwakilishi wa Viti Maalumu, Hidaya Ali Makame, aliyetaka kujua serikali inachukua hatua gani juu ya matumizi ya misumeno ya moto ambayo unaathiri mazingira ukiwamo ukataji wa miti.

Naibu waziri huyo alisema imebainika kwamba misumeno ya moto kwa asilimia kubwa imekuwa ikitumiwa kwa ajili ya kukata miti ikiwamo minazi kwa matumizi mengine yanayochangia uharibifu wa mazingira.

Alisema licha ya Serikali kupiga marufuku misumeno hiyo, lakini bado wapo watu wanaoimiliki kinyume cha sheria.

"Napenda kutoa taarifa kwamba serikali imepiga marufuku misumeno ya moto na watu watakaobainika kumiliki wajue kwamba wanafanya hivyo kinyume cha sheria na watachukuliwa hatua kali za kinidhamu," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi wa shehia wakiwamo masheha kusaidia kuwafichua wanaomiliki misumeno ya moto kinyume cha sheria na kuwasilisha taarifa zao katika vyombo vya sheria.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu, zaidi ya misumeno ya moto 1,670 imeteketezwa kwa moto katika visiwa vya Unguja na Pemba.

# Wawakilishi sasa waipa SMZ changamoto posho za walimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi, wameitaka Serikali kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizojitokeza katika mpango wa ugatuzi ikiwamo walimu kushindwa kulipwa posho wanazostahiki kwa wakati.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid, wakati akichangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Halmashauri Serikali za Mitaa) kwa mwaka wa fedha 2019-2020.

Abeid alisema tangu Serikali kutangaza mpango wa ugatuzi wenye lengo la kufikisha huduma muhimu za jamii kwenda Serikali za Mitaa, walimu wamekuwa wakisumbuliwa na kushindwa kulipa fedha za nauli za usafiri.

Alisema suala la elimu ya msingi ni moja ya mambo yaliyoingizwa katika mpango wa ugatuzi ambapo bado hakuna mipango madhubuti iliyofanywa katika kuzipatia ufumbuzi kero za walimu.

"Mheshimiwa Spika, bado sijaridhika na mipango ya ugatuzi katika sekta ya elimu ambapo walimu wanalalamika kwa muda mrefu kushindwa kulipwa posho zao ikiwamo nauli za usafiri," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, Rashid Makame Shamsi, aliitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuongeza kasi ya utekelezaji wa mpango wa ugatuzi katika kufikisha huduma muhimu ikiwamo upatikanaji wa vifaa vya shule.

Alisema ukosefu wa fedha za ruzuku za kuendesha shule ni moja ya kasoro kubwa ambayo wakati mwingine inawapa usumbufu mkubwa walimu kuendesha shule.

"Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kutoa fedha za ruzuku kwa wakati kwa shule za msingi ili ziweze kutekeleza majukumu yao bila ya kuanza kuwachangisha wanafunzi,"alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Bububu, Masoud AbrahmanMasoud, aliitaka Wizara kuongeza kasi ya ujenzi wa vituo vya afya ili kurahisisha huduma kwa wananchi katika majimbo.

"Wizara hii imepewa majukumu ya kusimamia mpango wa ugatuzi wa kufikisha huduma muhimu za jamii kwenda kwa wananchi ikiwamo sekta ya afya," alisema.

# Kamera zadhibiti vitendo vya wizi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUFUATIA kutekelezwa kwa mradi mkubwa wa kuweka kamera za ulinzi katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Zanzibar, matukio ya vitendo vya uhalifu yamepungua.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalumu), Haji Omar Kheir, wakati akiwasilisha hotuba ya makadirio mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019-2020.

Kheir alisema mradi huo sasa umeufanya mji wa Zanzibar likiwamo eneo la Mji Mkongwe kuwa na utulivu mkubwa, hivyo kuwafanya watalii kutembea bila ya bughudha.

Alisema tangu kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo, hata matukio ya uhalifu na vitendo vya uporaji dhidi ya wageni wakiwamo watalii vimepungua.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Baraza la Wawakilishi kwamba utekelezaji wa mradi wa mji salama umeleta mabadiliko makubwa ya utulivu wa wageni na usalama wao yakiwamo maeneo ya Mji Mkongwe," alisema.

Kheir alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa uamuzi wake wa kuweka kipaumbele katika utekelezaji wa mji salama ambao umetumia fedha za ndani ya nchi.

"Mheshimiwa Spika, mradi wa mji salama umetekelezwa kwa kutumia fedha za ndani ya nchi zinazotokana na makusanyo ya vianzio vya kodi zetu," alisema.

Alisema kuimarika kwa usalama wa mji wa Zanzibar kwa kiasi kikubwa utakwenda sambamba na ukuaji wa miji mingine na kufikia kiwango cha kutoa huduma kwa wananchi.

# Mkakati TFS kuingia mapato ya huduma utalii

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), umeweka mikakati kadhaa katika kuhakikisha misitu yake inaingiza mapato ya kutosha kupitia huduma za utalii sambamba na kuuza mazao ya misitu.

Mtendaji Mkuu wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, amesema miongoni mwa mikakati hiyo ni kuvitangaza vivutio vya utalii ekolojia vilivyopo kwenye misitu ya mazingira asilia iliyo chini ya taasisi hiyo.

Akizungumza wakati wa ufunguzi mkutano wa nane wa baraza la wafanyakazi wa TFS lililofanyika Morogoro, Prof. Silayo alisema aina hiyo ya utalii na biashara ya mazao ya misitu na nyuki ni nguzo ya utendaji kazi wa taasisi hiyo.

Akitolea mfano wa uvunaji wa utomvu wa miti inayokaribia kuvunwa katika shamba la Sao Hill, alisema bidhaa hiyo inahitaji kufanyiwa utafiti na kuangalia uwezekano wa kuongeza uzalishaji wake.

Alisema katika eneo hilo pia upo uwezekano wa kuongeza uzalishaji wa gundi kutoka katika miti ya migunga, zao linalotarajiwa kuingiza fedha nyingi siku za usoni.

Alisema ni jukumu la watumishi kuongeza jitihada katika utendaji wao ili kuhakikisha lengo hilo linatimia na kuleta matokeo chanya.

Prof. Silayo aligusia pia suala la udhibiti wa usafirishaji wa mazao ya misitu na nyuki pamoja na kushindwa kuimarisha huduma katika vivutio vya utalii.

"Haya ni maeneo ambayo inabidi tujipange vizuri zaidi kuyatekeleza katika kipindi cha miaka mitano ijayo ili kuondoa kero na kutoa huduma bora kwa umma.

"Endapo tutaimarisha maeneo haya, itasaidia kuongeza tija katika jukumu letu la ukusanyaji wa maduhuli ya serikali, kuongeza mauzo ya nje na fedha za kigeni kupitia huduma za utalii na uuzaji wa mazao ya nyuki," alisema Prof. Silayo.

Mwenyekiti wa TUGHE wa TFS, Francis Kiondo alisisitiza umuhimu wa kuzingatia sheria na kanuni za utumishi wa umma kwa kila mtumishi anapokuwa akitekeleza majukumu yake.

# EAC yajipanga kukabiliana na majanga

**Na Mwandishi Wetu,** GENEVA

NCHI za Afrika Mashariki (EAC), zimewasilisha mapendekezo tisa kwenye mkutano wa dunia wa wadau kujadili utekelezaji wa mkataba wa kupambana na majanga duniani uitwao Sendai.

Mkataba wa Sendai ulisainiwa na nchi mbalimbali duniani Tanzania ikiwamo mwaka 2015 nchini Japan, na kufuatiliwa na tamko la pamoja la Tunisia.

Utekelezaji wa mkataba huo ambao utaenda hadi mwaka 2030, una lengo la kuongeza jitihada za kukabiliana na majanga ya asili na yanayosababishwa na binadamu yanayotokea duniani kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Majana hayo ni tetemeko la ardhi, magonjwa, njaa, ukame kupindukia, mafuriko, mvua nyingi, mabadiliko ya vipindi vya mvua, maporomoko ya ardhi na miamba na kuongezeka kwa kina cha bahari huku sehemu ya ardhi ikimezwa.

Mkataba wa Sendai una malengo manne na vipaumbele saba, kwa wadau wa serikali, sekta binafsi, vyombo vya habari, makundi maalum na wananchi kuweka juhudi za pamoja katika kupunguza athari zinazosababishwa na majanga.

Akizungumza na Nipashe jijini Geneva, Uswis, Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi wa EAC, Dismas Mwikila, alisema majanga yanapotokea kuna kuwa na athari kubwa za kiuchumi kwa nchi husika kwa watu kufariki, kujeruhiwa na uharibifu mkubwa wa miundombinu.

Alisema athari nyingine ni watu kukosa makazi baada ya mafuriko kuharibu nyumba na mali zao nyingine, magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

"Hivi karibuni tumeona kilichotokea Msumbiji na Malawi ilikuwa ni janga kubwa kutokana na kimbunga ambacho ni matokeo ya mabadiliko ya tabianchi. Mkataba wa Sendai unataka kuwa na mkakati wa kukabiliana na matokeo ya majanga kwa kujiandaa vyema," alisema.

Alitaja mapendekezo hayo ni kuzijengea uwezo taasisi ikiwamo Mamlaka za hali ya hewa za nchi husika, kuwa na tekonolojia ya kutabiri karibu na usahihi majanga kabla na kusambaza taarifa kwa wananchi.

Alisema pia kuwa na sera pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa mkataba huo kuanzia ngazi ya jamii ambako kuna waathirika wa majanga husika.

Alisema kuimarisha mpango wa kukabiliana na majanga kwa kila nchi, kuwa na utaratibu wa kutoa taarifa na data za kabla ya janga kutokea kutolewa na mamlaka ya hali ya hewa.

Jingine ni kuyajengea uwezo makundi ya wanasayansi na wataalamu wa teknolojia, vijana, asasi na sekta binafsi ikiwamo kushirikiana nchi moja na nyingine kwa majanga yanayoweza kutokea na kuhusisha nchi zaidi ya moja kwa wakati mmoja, kwa kuwa na mpango shirikishi.

Mwikila alisema eneo jingine ni kuwekeza kwenye kujenga uwezo wa kisayansi na teknolojia kwa vyuo vikuu, vyuo vya mafunzo ya ufundi ikiwamo shule za msingi na sekondari kwa kuwa na uelewa wa kukabiliana na majanga.

Alisema EAC imeridhia mkataba huo na kuupitisha kwa ajili ya utekelezaji wa nchi wanachama, kwa kuwa ndani yake kuna malengo manne yanayopaswa kutekelezwa ifikapo 2020.

Mkutano huo ulioitishwa na Umoja wa Mataifa kupitia shirika la kukabiliana na majanga duniani (UNDRR), umewaleta pamoja wadau zaidi ya 500 kutoka nchi mbalimbali duniani, ikiwamo wanawake, walemavu, asasi za kiraia, serikali na vyombo vya habari.



Mkurugenzi wa Wilaya ya Musoma, John Kayombo (wa tatu kulia) na viongozi wenzake, wakiwa katika ziara ya kukagua majengo ya kituo kipya cha afya cha Kata ya Mugango, Musoma Vijijini juzi. Kituo hicho kimejengwa na serikali kwa kushirikiana na wakazi wa kata hiyo. **PICHA NA MPIGA PICHA WETU**

# Vifungashio vyawakwaza wajasiriamali

**Na George Tarimo,** IRINGA

KUKOSEKANA kwa upatikanaji wa uhakika wa vifungashio kumetajwa kuwa chanzo cha kuathiri soko la bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo mkoani Iringa, kutokana na kutumia vifungashio visivyokidhi vigezo na ushindani kwenye soko.

Wakizungumza na Nipashe baada ya kumalizika kwa kongamano la wajasiriamali na wanunuzi, wamesema pamoja na kuzalisha bidhaa bora zinazokidhi viwango bado ukosefu wa vifungashio unachangia bidhaa hizo kukosa ushindani wa masoko na mvuto kwa walaji wa nje ya mkoa.

Theodori Msigala na Genoveva Barnabas, waliwaomba wajasiriamali kuungana kwa lengo la kuagiza vifungashio nje ili kupunguza gharama.

Msigala alisema wapo baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wanauliza kwanini hawaoni bidhaa kutoka Iringa, ila jibu la haraka bidhaa za Iringa zipo sokoni, lakini changamoto kubwa ni kukosekana na vifungashio na kutangazwa ipasavyo.

Stela Mdahila, Meneja wa mradi wa Tanzania Local Enterprise Development (TLED), alisema mkoa una zaidi ya wajasiriamali 460, lakini changamoto kwa wajasiriamali hao ni ugumu wa upatikanaji wa masoko ya uhakika wa bidhaa wanazozalisha.

Alisema kuwa lengo kuu la mradi ni kuhakikisha wanunuzi na wauzaji wanakaa pamoja mezani, wanajadili na baadaye wanatoka na maazimio juu ya kupata vifungashio na masoko ya uhakika.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, aliliomba Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) kuwapatia wajasiriamali mikopo, huku akiahidi kuwatafutia vifungashio.

## HABARI KIMATAIFA

# Watu 80 wamekamatwa kwa kula mwezi mtukufu

**LAGOS,** Nigeria

POLISI wa Sheria ya Kiislamu katika Jimbo la kaskazini mwa Nigeria la 'The Islamic Sharia Kano' wamewakamata watu 80 kwa kudaiwa kula hadharani.

Kwa sasa, waumini wa dini ya kiislamu wapo katika mfungo wa mwezi wa Ramadhan ambapo kuanzia alfajiri hadi jua linapotua hawatakiwi kula chakula, lakini inasemekana watu hao walikwenda kinyume na sheria hiyo.

Polisi wa Sheria nchini Nigeria wanaofahamika kama Hisbah, wamesema kuwa watu hao walikamatwa kwa nyakati tofauti katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Kano katika kipindi cha siku kadhaa.

Jimbo la Kano ni moja kati ya majimbo kadhaa ya kaskazini mwa Nigeria ambako Sheria ya kislamu ilianzishwa upya tangu mwaka 2000. Sheria ya kiislamu inatekelezwa sambamba na sheria ya kawaida kwenye majimbo hayo.

Msemaji wa Hisbah katika jimbo la Kano, Adamu Yahaya, alisema kuwa wote waliokamatwa walikuwa ni Waislamu na maafisa hawawalengi wasio Waislamu kwa sababu hawafungwi na sheria ya kiislamu.

**Waislamu hufanya juhudi za kipekee kuungana na wengine katika jamii na kuwasaidia wale wanaohitaji usaidizi.**

Alisema kuwa baadhi ya wale waliokamatwa waliiambia ofisi ya Sheria kuwa walikuwa wanakula kwasababu hawakuuona mwezi wa Ramadhani, huku wengine wakisema walikuwa ni wagonjwa.

Lakini maafisa hao wa Polisi walisema kuwa madai yao hayakuwa na msingi wowote.

Yahaya alisema watu hao 80 walionywa na kuachiliwa huru kwa sababu walikuwa wamefanya kosa hilo kwa mara ya kwanza, na kwamba walionywa kuwa iwapo watakamatwa tena watapelekwa mahakamani.

Polisi wa Hisbah wamesema kuwa wataendelea kufanya doria katika kipindi chote cha Ramadhani kwa lengo la kuwakamata Waislamu wote ambao hawafungi katika mwezi huu.

Mfungo wa Ramadani ni lazima kwa kila mtu mzima ambaye ni Muislamu lakini baadhi ya watu ambao ni wagonjwa hawatakiwi kufunga.

**RAMADHANI NI NINI?**

Ramadhani ni moja ya nguzo tano kuu katika dini ya Kiislamu, mwezi huo, Waislamu hujifunga kula na kunywa kuanzia macheo hadi machweo.

Kufunga wakati huko huwawezesha Waislamu kujitolea zaidi katika dini na kumkaribia Allah.

Kando na kufunga, ni wakati pia wa kutafakari kiroho, kuswali, kutenda matendo mema na kujumuika na familia na marafiki.

Waislamu hufanya juhudi za kipekee kuungana na wengine katika jamii na kuwasaidia wale wanaohitaji usaidizi.

Huwa ni kawaida kwa Waislamu kula chakula asubuhi kabla ya mawio, suhur, na jioni wakati wa kufungua baada ya jua kutua, ambacho hufahamika kama iftar.

Mwisho wa kufunga, baada ya machweo, familia na marafiki hujumuika pamoja kufungua. Wengi pia huenda Msikitini kuswali.

Ramadhan imekuwa mwezi huu kwa sababu ndio wakati Qu'ran tukufu ilipofichuliwa kwa mara ya kwanza kwa Mtume Muhammad S.A.W.

Ramadhan huwa ni mwezi wa tisa katika kalenda ya Kiislamu, lakini tarehe hiyo hubadilika kila mwaka.

Hii ni kwa sababu dini ya Kiislamu hufuata kalenda inayotumia mzunguko wa mwezi, hivyo hubadilika tofauti na kalenda inayotumiwa na mataifa ya Magharibi inayofuata jua. **BBC**

## Marekani yaondoa wafanyakazi wake nchini Iraq

**WASHINGTON,** Marekani

WIZARA ya Mambo ya Nje Marekani, imeagiza kuondoka kwa wafanyakazi wake wasiofanya kazi za dharura nchini Iraq kufuatia hali ya wasiwasi kati ya nchi hizo mbili.

Wafanyakazi walioambiwa kuondoka haraka ni wale waliopo katika ubalozi wa mjini Baghdad na ubalozi wa Irbil.

**Wakati huo huo**, Ujerumani imesitisha mafunzo ya wanajeshi wake nchini Iraq. Jeshi la Marekani lilisema kwamba kiwango cha vitisho hivyo mashariki ya kati vilitolewa kutokana na ujasusi kuhusu vikosi vinavyoungwa mkono na Iran katika eneo hilo.

Kauli hiyo inakinzana na ile iliyotolewa na Jenerali mmoja wa Uingereza aliyesema kuwa hakuna vitisho vyovyote vilivyoongezeka nchini Iraq.

Naibu Kamanda wa muungano wa majeshi dhidi ya kundi la wapiganaji wa Islamic State, Chris Ghika alieleza kwamba hatua zilizochukuliwa kuwalinda wanajeshi wa Marekani na washirika wao kutokana na vikosi vinavyoungwa mkono na Iran nchini Iraq na Syria zinatosha. **BBC**

## Kiir: Sitoruhusu maandamano ya kuniondoa

**JUBA,** Sudan kusini

RAIS wa Sudan Kusini, Salva Kiir, ameonya kuwa serikali yake hataivumilia maandamano au mbinu zisizokuwa za kisheria kumshinikiza kuondoka madarakani.

Wiki mbili zilizopita, vuguvugu linalojiita 'Red Card Movement', lilianzisha harakati za kumtaka Rais Kiir kuondoka madarakani, kuanzia Mei 16. Maandishi kama #KiirMustGo na #SouthSudanUprising, yamekuwa yakishuhudiwa kwenye mitandao ya kijamii, huku waandaaji wakiwa nje ya nchi hiyo.

Harakati hizi zinatarajiwa kufuata mfano wa hali ilivyokuwa katika nchi jirani ya Sudan, baada ya waandamanaji kuanzia Desemba mwaka jana kuanza kushinikiza kuondoka madarakani kwa Rais wa zamani, Omar Al Bashir.

"Wale watakaojaribu kuharibu utulivu wa nchi watashughulikiwa," alionya Rais Kiir.

Rais Kiir na Machar wametia saini mkataba wa amani, kuunda serikali ya pamoja lakini imesalia vigumu kutekeleza mkataba huo, huku Machar akisalia kuwa nje ya nchi. **RFI**




Kiongozi wa kijeshi nchini Sudan, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, akitangaza kuahirishwa mazungumzo kati ya Jeshi la wananchi jana, baada ya kutokea vurugu. **PICHA: AFP**

# Jeshi Sudan lasitisha mazungumzo na waandamanaji

**KHARTOUM,** Sudan

WATU 14 wamejeruhiwa kwa risasi nchini Sudan baada ya jeshi kujaribu kuwaondoa waandamanaji waliopiga kambi nje ya makao makuu ya jeshi jijini Khartoum.

Makabiliano haya yalitokea saa chache baada ya jeshi na viongozi wa waandamanaji kukubaliana kuunda serikali ya mpito itakayodumu kwa muda wa miaka mitatu.

Jeshi kupitia kiongozi wake Jenerali Abdel Fattah al-Burhan alitangaza kusitisha mazungumzo na viongozi wa waandamanaji kwa saa 72, wakati ambao waandamanaji wakiendelea kusisitiza hawataacha kupiga kambi nje ya makao makuu ya jeshi.

"Kulikuwa na watu ambao walikuwa na nia mbaya kati ya wanadamanaji waliowalenga maafisa wetu wa usalama," alisema Jenerali Burhan.

Hata hivyo, waandamanaji wanawalaumu wanajeshi kwa kuwashambulia, kauli ambayo pia imeungwa mkono na Balozi wa Uingereza nchini humo, Irfan Siddiq.

Kupitia katika ukurasa wake wa Twitter, Siddiq alisema anasikitishwa kuona jeshi likitumia risasi kuwashambulia waandamanaji.

Kabla ya kusitishwa kwa mazungumzo hayo, wanajeshi na waandamanaji walikuwa wamekubaliana kuunda serikali ya mpito kwa muda wa miaka mitatu. **RFI**

# Tanzania yapongezwa kuzuia mifuko ya plastiki

**Na Mwandishi Wetu,** GENEVA

SHIRIKA la Kimataifa la kutetea na kulinda Wanyama, limeipongeza Tanzania kwa kuzuia matumizi ya plastiki, kwa kuwa ni uamuzi mkubwa wa kulinda mazingira kwa faida ya kizazi kilichopo na kijacho.

Akizungumza na Nipashe mjini Geneva, nchini Switzerland, Mkuu wa kitengo cha mawasiliano na majanga duniani, Scott Cantin, alisema uchafuzi wa mazingira ya bahari usipochukuliwa hatua madhubuti ni janga jingine kwa dunia.

Alisema uamuzi wa serikali kuwa na sheria na sera zinazolinda mazingira hasa kwenye eneo la kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ni wa kupongezwa na unastahili kuungwa mkono.

Alisema shirika hilo pia linafanya kampeni ya kulinda uchafuzi wa bahari kwa kutumia plastiki, kwa kushirikiana na jamii za maeneo husika kusafisha fukwe za bahari.

"Plastiki ni hatari kwa mazingira na bahari kwa ujumla kwa kuwa yanaweza kuua viumbe hai ikiwamo samaki, lakini zinaweza kuishi kwenye mwili wake na kuliwa na binadamu kisha kuleta madhara makubwa kwa afya zao," alisema.

Alisema kwa nchi zinazopiga marufuku matumizi ya plastiki zinastahili kuigwa kuwa wamebaini chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira.

"Tunafahamu kuwa plastiki zinaishi kwenye ardhi kwa zaidi ya miaka 500 kama hazijaondolewa na kuharibiwa," alisema.

"Uamuzi wa Tanzania ni mzuri sana kwa kuwa sasa wanakwenda kupunguza kiwango cha plastiki zinazokwenda kwenye ardhi, vyanzo vya maji na habari. Hivi ndivyo nchi zinapaswa kufanya kwa kuwa na mpango endelevu wa kutunza mazingira kwa miaka mingi ijayo," alisema.

Aidha, kwa mujibu wa takwimu ya Umoja wa Mataifa, inakadiriwa kuwa miaka mitano hadi kumi ijayo kutakuwa na plastiki nyingi kwenye bahari, ambazo kwa kawaida zinaishi kwa zaidi ya miaka 500. Aprili mwaka huu, serikali alitangaza uamuzi wa kupiga marufuku uzalishaji plastiki ifikapo Mei 31, na itakapofika Juni mosi, hakuna kuzalisha mifuko au kutumia plastiki ambazo hazina ubora unaotakiwa.

Februari mwaka huu, katika mdahalo ulioitishwa na Ubalozi wa Ufaransa nchini, mtafiti wa Mazingira na Afya wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili, Hussein Mohamed, alisema upo uwezekano mkubwa wa plastiki kuwa chanzo cha maradhi ya saratani, mfumo wa uzazi na ini.

Mhandisi wa Viwanda Idara ya Mazingira ya Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano, Julius Mushi, alisema plastiki ni changamoto ya dunia kutokana na ukweli huduma kwenye mazingira kwa miaka 500 hadi 1,000.

"Uchafuzi ukiendelea hivi utaathiri mazingira na afya zetu, lakini pia suala la kiuchumi. Taka zinapoingia kwa wingi kwenye bahari zitaathiri afya kupitia samaki, pia mifugo hupenda kula plastiki kutokana na chumvi chumvi iliyopo," alisema.

Kwa mujibu wa Mushi, takwimu zinaonyesha Tanzania inatumia mifuko bilioni mbili hadi tano, ikiwa ni wastani wa kila Mtanzania wa Bara kutumia mfuko mmoja hadi miwili kwa wiki.

"Kwenye uzalishaji tunazalisha tani 60,000 kwa mwaka za taka za plastiki na asilimia 70 hadi 80 huingia kwenye mazingira na hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa mazingira na maeneo ya ikolojia," alifafanua.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na uongozi wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, katika ukumbi wa Ikulu Ndogo Kibweni, jana, wakati wa mkutano wa Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Wizara hiyo, kwa mwezi Julai 2018 hadi Machi 2019. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Mashamba yaliyofutiwa milki

INATOKA UK. 4

wananchi na wamiliki, wizara yake imeamua kupeleka timu kutoka wizarani kwa ajili ya kuyafanyia uhakiki. Kwa mujibu wa Lukuvi, timu hiyo inajumuisha Kamishna wa Ardhi, Mary Makondo; Kaimu Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani, Samweli Katambi;, Mthamini Mkuu wa Serikali, Evalyne Mugasha; Kamishna Msaidizi wa Ardhi Kanda ya Kati, Ezekiel Kitilya; na wataalamu kutoka idara za Mipango Miji wizarani.

Alisema uamuzi wa kwenda na timu kutoka wizarani unalenga kumaliza kabisa migogoro ya ardhi katika wilaya hiyo hasa baada ya kubaini ofisi za wilaya na Mkoa wa Morogoro kushindwa kutatua mgogoro huku viongozi wake wakituhumiwa. Waziri wa Ardhi alitaja kazi kubwa itakayofanya timu hiyo kuwa ni kupitia mashamba 15 yaliyofutwa na Rais sambamba na kufufua mipaka ya mashamba hayo na kazi hiyo itafanywa kwa na ushirikiano wa ngazi za wilaya.

"Tutayapitia mashamba yote yaliyofutwa na Rais na kujua kilichomo ndani yake na timu ya uhakiki niliyokuja nayo itanilitea mapendekezo ya namna ya kutumia mashamba na mengine watapewa wanaostahili na si kila mtu atapewa," alisema Lukuvi.

Alisisitiza kuwa wale wote waliojimilikisha mashamba yaliyofutwa na Rais watanyang'anywa na kupatiwa wanaostahili na mengine yatatolewa kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa ajili ya kupatiwa wawekezaji. Mkuu wa Idara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira katika Halmashauri ya Kilosa, Ibrahim Mndembo, alisema mashamba 25 yenye ukubwa wa ekari 23,596 kwenye maeneo ya Msowero, Magole na Chanzulu katika wilaya ya Kilosa yamebatilishwa umiliki baada ya wamiliki wake kushindwa kuyaendeleza.

Alisema kati ya mashamba hayo, 15 yalibatilishwa miliki zake katika kipindi cha uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

Mashamba yenye mgogoro na wananchi katika wilaya ya Kilosa ni Noble Agriculture Enterprises, Magereza dhidi ya wananchi wa Mabane, Mbigiri na Mabwegere, Chadulu Estate, Shamba la Swai dhidi ya wananchi wa Ilonga na shamba la Mauzi Estate Malangali.

## Shahidi adai maneno

INATOKA UK.4

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, kuhusu watu waliokamatwa kwa kuzomea polisi, alidai hakuna aliyekamatwa.

Shahidi huyo aliangalia Youtube akiwa Kimara Korogwe, Dar es Salaam. Kesi itaendelea kesho saa tatu asubuhi.

Awali aliposomewa maelezo ya awali, Zitto alikana kwamba Oktoba 28, 2018 katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika ofisi za makao makuu ya chama cha ACT-Wazalendo kwa nia ya kuleta chuki miongoni mwa wananchi wa Tanzania dhidi ya Jeshi la Polisi, alitoa maneno ya uchochezi.

Zitto alikana maneno ambayo anadaiwa kuyasema: "Watu ambao walikuwa ni majeruhi katika tukio la mapambano baina ya wananchi na polisi, wakiwa wamekwenda hospitali kupata matibabu katika kituo cha afya cha Nguruka, polisi wakapata taarifa kuwa kuna watu wanne wamekwenda hospitali kituo cha afya Nguruka kupata matibabu wakawafuata kule wakawaua".

Jamhuri inadai maneno hayo yalikuwa ni ya uchochezi yenye kuleta hisia ya hofu na chuki.

Mshtakiwa anadaiwa kutoa maneno kwamba: 'Lakini tumefuatilia kwa kina jambo hili, taarifa ambazo tumezipata kutoka kijijini Mpeta Nguruka, Uvinza ni mbaya ni taarifa ambazo zinaonyesha wananchi wengi sana wameuawa, na Jeshi la Polisi, pamoja na kwamba Afande Sirro wamekwenda kule, halijatoa taarifa yoyote kuhusu wananchi... kama hawa Wanyantuzu walivamia eneo la Ranchi, kuna taratibu za kisheria za kuchukua nasiyo kuwauwa, wananchi wengine sana wamekufa'.

## Rais wa AfDB aipongeza Tanzania

INATOKA UK.5

masoko ya mazao yanayozalishwa katika kanda mbalimbali za Tanzania na kuongeza thamani.

Kuhusu miradi mingine ya maendeleo alisema kwa hivi sasa AfDB imetoa ufadhili kwa miradi yenye thamani ya Sh. trilioni 4.55 na kwamba hivi karibuni benki hiyo imeidhinisha ufadhili kwa miradi ya ujenzi wa barabara za mzunguko (ring road) za Jiji la Dodoma zenye urefu wa kilometa 110.

Alisema fedha zingine ni za ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato mkoani Dodoma na pia alipongeza Tanzania kwa kuanza mradi mkubwa wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa kati ya Dar es Salaam na Dodoma kwa kutumia fedha zake na ameahidi kuwa benki hiyo itaunga mkono mradi huo hasa kwa ujenzi wa kuanzia Isaka kwenda Kigali nchini Rwanda na kunufaisha nchi nyingine za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kwa upande wake, Rais Magufuli alimshukuru Dk. Adesina kwa ushirikiano mkubwa ambao AfDB inautoa kwa Tanzania na amemhakikishia kuwa Tanzania itahakikishia fedha zinazotolewa na benki hiyo zinatekeleza miradi iliyokusudiwa kwa uhakika na inaleta matokeo yanayotarajiwa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.

### MCHANGANYIKO

**NYUMBA INAUZWA**,NYUMBA INAUZWA YENYE VYUMBA SITA, UZIO NA NAFASI KUBWA, MAJI YAPO, IPO TEMEKE JIRANI NA SHULE YA SANDALI, BARAZA LA KATA. BEI NI NAFUU. PIGA SIMU: 0719 698680, 0654 766168, 0762 014266. MADALALI HAWATAKIWI.

**MONKAL I INSULIN:** Inaponya maradhi mbalimbali sugu kwa waliogua muda mrefu,inarejesha kongosho ktk utoaji ute mchungu na kuwa normal balance 4- 5- 6, iko katika mfumo wa maji na vidonge,husaidia mmengenyo wa chakula,tiba lishe,gout,vidonda vya tumbo kuunguruma na kujaa gesi n.k kama umehangaika huku na kule bila mafanikio njoo nikusaidie acha kutes eka:0713293988/0758078288kutese ka:0713293988/0758078288

NIPASHE NI JIBU LAKO

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
15/05/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 19-05-2019 kampuni ya **MSELLE CIVIL ENGINEERS CO. LTED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MLANDIZI** kuelekea **MBWEWE,** gari lenye namba za usajili **T 670 DPD.** Gari linalosafirisha namba za usajili; **STH 2712, STH 2782.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:


| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 9.7** |
| **Upana** | - | **mita 2.5** |
| **Kimo** | - | **mita 3.3** |

3. Njia itakayotumika: **MLANDIZI hadi MBWEWE kupitia CHALINZE,** Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115233402

### PASSPORT IMEPOTEA



**ALERON ADRIAN MTENDA** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **TAE088502** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam 11/02/2019.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi DAR/KIJ/RB/1453/2019.**

115232902

### PASSPORT IMEPOTEA



**ALATRINA ADRIAN MTENGA** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **TAE088501** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam 11/02/2019.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi DAR/KIJ/RB/1453/2019.**

115233002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MWANZA**
**SHAURI NA 263 LA 2016**

**ZUBEDA IDD MABUSI.....................MDAI**
**DHIDI YA**
**MAGANGA SHIJA............................MDAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: MAGANGA SHIJA**

Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ ombi dhidi yako katika baraza la ardhi na nyumba mko wa Mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 06/06/ 2019 katika chumba cha baraza , barabara ya posta jinge liko mkabala na mahakama kuu ya biashara, Tanzania.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.

KAANI- ukijua kwamba kushindwa kufika, baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na chapa ya Baraza leo tarehe 02/05/2019

215233302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**TANGA**
**SHAURI LA MAOMBI YA GHARAMA NA 06 LA 2019**
**LUCAS FRANCIS NA WENZAKE 7.....MSHINDA TUZO**
**DHIDI YA**
**TROIKA DEVELOPERS LTD................MDENI TUZO**

**KWA:**
**TROIKA DEVELOPERS LTD**

**KUITWA SHAURINI**

Mshinda tuzo amefungua maombi ya madai ya gharama mbele ya Mahakama Kuu ya Tanzania-Tanga. Shauri limepangwa kusikilizwa tarehe 17/6/2019 saa tatu asubuhi.

Hivyo basi unatakiwa kuhudhuria wewe mwenyewe au wakili wako kwa tarehe iliyopangwa. Endapo hutahudhuria shauri hili litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.

Imetolewa na kutiwa Saini na Muhuri wa Mahakama Kuu ya Tanzania Tanga leo Tarehe 13 mei 2019.

115233102

### KUPOTEA KWA KADI

**Salome M. Pallangyo** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba **T922 DJJ** aina ya **NISSAN EXTRAIL.** Yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MPW/RB/383/2019**

115232002

### KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**CHRISTOPHER D. SANGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI AINA YA TVS KING YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 818 BCC** RANGI NYEUSI CHASSIS NAMBA **MD6M14PK1B4C18030** ENGINE NAMBA OK4CB1035656. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MB/RB/TRL/SLS/19.**

115234102

### PASSPORT IMEPOTEA



**NURU NICHOLAUS LUVINGA** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **TAE088503** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam 11/02/2019.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi DAR/KIJ/RB/1453/2019.**

115232802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;109/2019**

**Ombi la ZAHARANI ABDALLAH NGUPEPE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ABDALLAH ALLY NGUPEPE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/05/2019.

115233902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 111/2019**

**Ombi la JUMA. A.KABELWA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ZUBEDA SELEMAN KABELWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 30/05/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/05/2019.

115234002

*KWA MATANGAZO MADOGO, MADOGO*

*Tupigie 0767 223311*

### CHETI KIMEPOTEA



**MWINGA GEORGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1820-0024** kilichotolewa na HILL CREST SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MW/RB/1315/2019.**

115232402

### CHETI KIMEPOTEA



**AMANI ELIRINGIA MAKYAO** anatangaza kupotelewa na cheti cha FTC chenye index namba U005/0210 kilichotolewa na ARUSHA TECHNICAL COLLEGE mwaka 1999.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: DAR/URA/RB/16957/2019.**

115232702

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA/PASSPORT



**Frank Gervas Fungameza** anatangaza kupotea kwa Passport au Hati ya kusafiria yenye namba **AB 223921** iliyotolewa na Ofisi ya Uhamiaji Dar es Salaam mwaka 2007. Yeyote ataeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MW/RB/1315/2019**

115231902

KWA MATANGAZO

MADOGO MADOGO

TUPIGIE

*0767 223311*

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HABARI MICHEZO


## BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

## TANGAZO KWA UMMA

## TAARIFA YA UZINGATIAJI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA MAZINGIRA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 ili kuhakikisha usimamizi na hifadhi endelevu ya mazingira nchini unafanyika. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Baraza kama yalivyoainishwa katika Kifungu Na. 17(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ni pamoja na kusimamia uzingatiaji na utekelezaji wa sheria; kufanya mapitio ya taarifa za tathmini ya athari na uhakiki wa mazingira; kuhakikisha ushirikishwaji wa umma katika maamuzi yanayohusu uhifadhi wa mazingira; na pia kushiriki katika masuala yote yanayohusu usimamizi na uratibu wa mazingira nchini.

Aidha, Serikali imelipa Baraza dhamana ya kuhakikisha usimamizi na hifadhi endelevu ya rasilimali na mazingira nchini ili kuboresha hali ya maisha ya watu na maendeleo endelevu ya viwanda na miradi yote inayoanzishwa nchini. Hivyo basi, Baraza limekuwa likisimamia mchakato wa Tathmini ya Athari na Uhakiki wa Mazingira ili kuhakikisha shughuli za maendeleo hususan viwanda haziathiri mazingira.

Katika kutekeleza majukumu yake, Baraza limefanya kaguzi na ufuatiliaji wa miradi mbali mbali na maendeleo katika mikoa mingi hapa nchini. Ukaguzi na ufuatiliaji huo umebaini kuwepo kwa kasoro kadhaa ambazo zinatokana na kutokuzingatia na kutokutekelezwa kwa matakwa ya sheria ya mazingira na kanuni zake. Kasoro hizo zimesababisha uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na uchafuzi wa vyanzo vya maji, hewa, na udongo. Aidha, kutokuzingatia Sheria kumesababisha athari nyingine ikiwa ni pamoja upotevu na uharibifu wa makazi ya viumbe hai (mimea na wanyama).

Ukaguzi na ufuatiliaji huo umebainisha sababu mbalimbali zinazosababisha uharibifu na uchafuzi wa mazingira ikiwa ni pamoja na:

- Baadhi ya miradi kuanza kutekelezwa bila kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira;
- Wamiliki wa miradi kutotekeleza kwa ukamilifu masharti ya vyeti vya Tathmini ya Athari na Uhakiki kwa Mazingira;
- Baadhi ya miradi kutokuwa na mitambo ya kutibu majitaka inayokidhi mahitaji;
- Miradi kutokuwa na vifaa na mifumo maalum ya kudhibiti uchafuzi wa hewa;
- Miradi kutoajiri wataalamu wenye fani husika ya kusimamia masuala ya mazingira;
- Miradi na shughuli za maendeleo kutokuwa na utaratibu binafsi wa ufuatiliaji wa matokeo ya masuala ya mazingira (self-monitoring);
- Miradi kutokutunza taarifa za kimazingira kwa mujibu wa sheria;
- Wamiliki wa miradi kutokulipa ushuru na tozo mbalimbali za kimazingira kwa mujibu wa sheria;
- Wamiliki wa miradi kutokutii na kutekeleza maagizo na makatazo mbalimbali yanayotolewa na Baraza; na
- Baadhi ya wamiliki kusajili miradi kwa ajili ya kufanya uhakiki wa mazingira na kusitisha mchakato husika bila kutoa taarifa kwenye ofisi za Baraza.

Kwa kuzingatia masuala yaliyoainishwa na kuepuka madhara zaidi yasitokee kwenye mazingira na kulinda afya ya binadamu, Baraza linawaagiza wamiliki wote wa miradi kuzingatia na kutii sheria kwa hiari. Ikumbukwe kuwa uwekezaji nchini unakua kwa kasi katika sekta za viwanda, madini, miundo mbinu, majengo, kilimo, uzalishaji nishati, utalii n.k. Iwapo uwekezaji huu hautakidhi matakwa ya uhifadhi wa mazingira, madhara yatakuwa ni makubwa yasiyoweza kurekebishika. Hivyo basi kwa tangazo hili, Baraza linawataarifu kuwa ili kuhakikisha shughuli zote za maendeleo haziathiri mazingira, litaendelea kufanya kaguzi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja kuipitia miradi yote ya maendeleo nchini ili kuhakikisha matakwa ya sheria yanazingatiwa ipasavyo. Katika zoezi hilo, ukaguzi na ufuatiliaji utalenga katika masuala yafuatayo:

- Vyeti vya tathmini ya athari na uhakiki wa mazingira kuthibitisha kama tathmini imefanyika;
- Utekelezaji wa mpango wa usimamizi na ukaguzi wa mazingira (Environmental Management and Monitoring Plan- EMP);
- Utekelezaji wa masharti ya jumla na mahsusi ya vyeti vya tathmini ya athari na uhakiki wa mazingira;
- Uhakiki wa kila mwaka wa mazingira na uwasilishaji wa taarifa zake kwa Baraza;
- Mifumo ya usafishaji wa majitaka;
- Mifumo ya udhibiti wa maji ya mvua ili yasichanganyike na majitaka;
- Mifumo ya ukusanyaji, utunzaji, udhibiti na utupaji wa aina zote za taka zinazozalishwa;
- Vifaa maalum vya kudhibiti uchafuzi wa hewa;
- Utaratibu wa ufuatiliaji wa matokeo ya shughuli za miradi (self-monitoring) na uwasilishaji wa taarifa kwenye ofisi za Baraza;
- Uwepo wa wataalamu mahsusi walioajiriwa kusimamia masuala ya mazingira;
- Utekelezaji wa maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Baraza kwa nyakati tofauti;
- Ulipaji wa ushuru na tozo mbalimbali kwa mujibu wa sheria; na
- Utunzaji na uwasilishaji wa taarifa za mazingira zenye kuonyesha mwenendo wa utekelezaji wa mradi.

Tangazo hili linahusu miradi yote inayotekelezwa na watu binafsi na serikali kupitia wizara, taasisi za umma na serikali za mitaa. Aidha, kutokuzingatia utekelezaji wa masuala yaliyotajwa hapo juu kutapelekea Baraza kuchukua hatua za kisheria kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Iwapo utahitaji ufafanuzi zaidi usisite kuwasiliana na Ofisi za Baraza makao makuu zilizopo katika Kiwanja Na. 28-30, Mtaa wa Regent, au katika ofisi za kanda za Baraza zilizopo Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Mtwara.

**Tangazo limetolewa na:**
**MKURUGENZI MKUU ,**
**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)**
**Limesambazwa na:**
**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma,**
**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**
**Viwanja Na. 28, 29 &30-35, Mtaa wa Regent, S.L.P 63154, Dar es Salaam.**
**Simu ya mezani: +255 22 2774889, moja kwa moja: +255 22 2774852**
**simu za mkononi: 0713 608930/ 0692108566**
**Fax: +255 22 2774901, Barua pepe: dg@nemc.or.tz**




# SOLSKJAER AJIPANGA KUWATEMA MASTAA

**LONDON,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesisitiza atawaondoa wachezaji wengi kwenye dirisha lijalo la usajili.

Hata hivyo, kocha huyo huenda akagusa wachezaji wote, lakini si kinda, Anthony Martial, ambaye mmiliki mwenza wa timu hiyo, Joel Glazer, anamwona kama Pele wa United.

Martial kujituma kwake kwenye kikosi hicho kumetiliwa mashaka na makocha wote, Jose Mourinho aliyeondoka na huyu wa sasa Solskjaer jambo linalotia wasiwasi mkubwa wa hatima ya Mfaransa huyo kuendelea kubaki Old Trafford msimu ujao.

Hata hivyo, kutokana na kuwa mchezaji kipenzi cha bosi, Martial anaweza kuwa salama.

Januari mwaka huu, Martial alisaini mkataba mpya hadi mwaka 2023 ambao utamshuhudia akiweka kibindoni pauni 200,000 kwa wiki.

Makamu Mwenyekiti wa United, Ed Woodward naye anamwona Martial ni silaha ya siku za baadaye.

Kipindi kile Mourinho alitaka kumwondoa ili kumleta winga Ivan Perisic, lakini mabosi Glazer na Woodward wakamtaka Martial kwenye timu hiyo.

Kutokana na hilo, Kocha Solskjaer atakuwa na orodha yake ya wachezaji kadhaa ambao hataguswa akiamua kuwaondoa kwenye kikosi hicho ili kupunguza bili ya mishahara na kuwanasa wachezaji wengine wapya watakaokuwa na faida kwenye kikosi hicho.

Ripoti zinadai kuna orodha isiyopungua ya wachezaji wanane wataachana na maisha ya United kwenye dirisha lijalo la usajili, huku ikidaiwa kuna sura tano mpya zitatua hapo kabla ya Julai Mosi watakapoanza mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya.


Wachezaji Antonio Valencia na Ander Herrera hao hawatakuwapo Old Trafford msimu ujao, lakini panga la Ole huenda likapitia pia majina ya mastaa kama Matteo Darmian, Marcos Rojo, Eric Bailly, Juan Mata, Romelu Lukaku na Alexis Sanchez.

Kuna taarifa pia zinazomtaja Paul Pogba kuwa ni miongoni mwa mastaa watakaofunguliwa milango ya kutokea licha ya bosi Woodward kumtaka mchezaji huyo aendelee kubaki Old Trafford kwa sababu za kibiashara.

Ole hataki mzaha na ndio maana kwenye orodha ya wakali wanaotajwa kwamba watapigwa panga Old Trafford kuanzia sasa wote ni mastaa wakubwa.

# Neymar ajiandaa kutua Madrid

**PARIS,** Ufaransa



MCHEZAJI wa kimataifa wa Brazil, Neymar, ameripotiwa anawasubiri Real Madrid watoe ofa ya kumchukua na hatasita kuondoka PSG.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Hispania, mchezaji huyo ameshapanga hadi mabegi yake akijiweka tayari kabisa kwa ajili ya kurejea kwenye La Liga.

Neymar amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Hispania, lakini si kwenda kuichezea timu yake ya zamani ya Barcelona, bali kujiunga na mahasimu wao, Real Madrid.

Ni miaka miwili tu imepita tangu PSG ilipovunja benki kuweka rekodi duniani ya kutumia pauni milioni 198 ili kunasa huduma ya mshambuliaji huyo.

PSG iliamini baada ya kumnasa Mbrazili huyo inaweza kushinda ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini jambo hilo limeshindwa kutokea na msimu huu ilitupwa nje na timu dhaifu ya Manchester United katika hatua ya 16 bora.

Neymar sasa anaona anapoteza tu muda kwenye timu hiyo na hivyo kufikiria kurudi Hispania ambako kuna timu 'siriazi' kwenye kusaka mataji kwa kila msimu.

## HABARI MICHEZO

# Man City yakosolewa kuwakejeli Liverpool

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City, wamekosolewa juu ya video ya wimbo wao iliyoonyesha wachezaji na wahudumu wa timu hiyo wakiungana katika kuimba wimbo wa kejeli wa kusherehekea mashabiki wa Liverpool "wakichapwa mtaani".

Video hiyo inadhaniwa kuwa ilichukuliwa kutoka kwenye ndege wakati timu hiyo ilipokuwa ikisafiri kutoka katika sherehe za ushindi wa Ligi Kuu England wa 4-1 dhidi ya Brighton.

Ushindi huo uliiwezesha City kuipita Liverpool kwa ushindi mwembamba wa pointi moja.

Manchester City bado haijatoa kauli yoyote juu ya video hiyo.

Haijabainika wazi ni wachezaji wala wahudumu gani wa klabu hiyo walishiriki katika wimbo huo, ambao unakumbusha kushindwa kwa Liverpool katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mjini Kiev.

Wimbo huo unaelezea jinsi mashabiki wa Liverpool walivyochapwa katika mitaa na kulia na wimbo huo unaelezea pia kuwa mshambuliaji wa Liverpool, Mo Salah alijeruhiwa, lakini pia ikielezea kwamba aliumizwa na Vincent Kompany.

Hata hivyo, waliojiunga kuimba wimbo huo walisikika kwenye kibwagizo tu cha wimbo wakiimba "Allez, Allez, Allez".






# BERAHINO AMFUATA BEKHAM KIFUNGONI

**LONDON,** England

MCHEZAJI Saido Berahino, amepatikana na hatia ya kuendesha gari huku akiwa amekunywa pombe.

Mshambuliaji huyo wa Stoke City, alikuwa amezidisha takriban mara tatu ya kiwango cha kileo wakati gari lake aina ya Range Rover liliposimamishwa katika eneo la West End jijini London majira ya saa tisa usiku Februari 18 mwaka huu.

Mahakama ya Highbury Corner ilisikiliza kesi ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25.

Mahakimu walisema 'hakuwa na uoga wa kifo wala wa kujeruhiwa vibaya' kabla ya kupigwa faini ya pauni 75,000 na kumzuia kuendesha gari kwa kipindi cha miezi 30.

Jaji mkuu, Mark Oxenham, alisema kuwa rafiki wa kike wa Berahino alikuwa ameendesha gari hilo kabla, "angeweza kuendelea na safari kutoka kwenye eneo la tukio ".

Mahakama iliambiwa kuwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Burundi, awali alipatikana na hatia ya kuendesha akiwa amelewa mnamo mwaka 2015 na kuwa mmiliki wa gari lililoendeshwa na mlevi mwaka 2012.

Berahino, ambaye anaishi Old Penkridge Road, Staffordshire alikuwa anaendesha gari ya Range Rover wakati polisi walipolisimamisha katika eneo la Bedford Square.

# *Mourinho aanika kinachoitafuna Utd*

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesema kuwa matatizo yanayoisumbua klabu ya Manchester United yapo kwa wachezaji, mfumo na malengo huku akimtaja mchezaji, Paul Pogba anahusika kwa kutimuliwa kwake kazi.

Mourinho ambaye alikuwa Kocha Mkuu ndani ya timu hiyo ya Man United, alitimuliwa kazi Desemba mwaka jana, wakati matatizo ya mahusiano yake dhidi ya Pogba yaliyoanza Septemba mwaka huo hadi kupelekea kuporwa kitambaa cha unahodha ili kuweka mambo sawa ndani ya uwanja, ingawa haikuwa kama ilivyotarajiwa.

Alipoulizwa kama alikuwa ameathiriwa na Pogba, raia huyo wa Ureno aliliambia gazeti maarufu la michezo nchini Ufaransa L'Equipe, "Hapana, matatizo yapo pale, unaweza kuwaamini kuwa matatizo ni wachezaji, mfumo na malengo."

"Nitaweza kusema tu kwamba, siwezi kusema ndiyo, uliponiuliza kama Paul Pogba ni yeye tu anayewajibika, Mourinho alisema anadhani Paul Pogba ndiyo chanzo.

Ole Gunnar Solskjaer alichukuliwa kuziba nafasi ya Mourinho kwa kupewa mkataba wa miaka mitatu baada ya kuitumikia United kama kocha wa muda huku akishinda mechi 14 kati ya 19 alizoisimamia United na kuisaidia kurudi katika nafasi nne za juu.

Hata hivyo, ameshindwa kumaliza ligi hiyo akiwa kwenye nne bora baada ya kushika nafasi ya sita.



HABAR

# DOND A SOKA MAGAZ A ULAYA




# BALE KUWAAGA MADRID JUMAPILI

●●● Nyota huyo wa kimataifa wa Wales anajiandaa kuaga baada ya kucheza kwa mafanikio makubwa...

**MADRID,** Hispania

GARETH Bale anataka kuaga kwenye dimba la Bernabeu wikiendi hii wakati Real Madrid itakapocheza dhidi ya Real Betis kwenye mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu Hispania msimu huu.

**Kwa takribani miaka sita iliyopita, mashabiki 30,000 wa Madrid walihudhuria kumkaribisha mchezaji huyo wakati aliposajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 86 kutoka Tottenham.**

Na sasa nyota huyo wa kimataifa wa Wales anajiandaa kuaga baada ya kucheza kwa mafanikio makubwa hapo kwenye mji mkuu wa Hispania.

Kuondoka kwa Bale hapo Bernabeu kumechagizwa na kocha Zinedine Zidane ambaye anajipanga kufanya usajili mkubwa kipindi hiki cha majira ya joto.

Na kwa mujibu wa gazerti la Hispania la Marca, Los Blancos hao watampa nafasi Bale kwenye mchezo huo wa Jumapili ili kuwaaga mashabiki wake, baada ya kubeba mataji 13 kwa kipindi chote alichocheza hapo.

Winga huyo mweye umri wa miaka 29, anaondoka hapo baada ya kutokuwa kwenye mipango ya Zidane ambaye alimweka nje ya dimba katika mchezo dhidi ya Villareal na Real Sociedad.

Wakati huo huo, taarifa zaidi zinasema kwamba, klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur imeambiwa ikamchukue kwa mkopo wa pauni milioni 10. Kinachoelezwa ni kwamba Real Madrid inataka kumwondoa mchezaji huyo kwenye kikosi chake hasa baada ya Zidane kuonekana wazi kuwa hamtaki.

Wababe hao wa Bernabeu wanataka kujinasua kwenye shida ya mshahara mkubwa wanaomlipa mchezaji huyo huku mwenyewe akigoma kung'atuka kuacha fedha ndefu kiasi hicho cha pauni 600,000 kwa wiki.

Sasa Madrid ipo tayari kumtoa kwa mkopo kwa timu itakayokuwa tayari kulipa mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki, ikitoa pauni milioni 10, basi itamchukua mchezaji huyo.

Bale amekuwa adui namba moja wa mashabiki wa Madrid wakimzomea mchezaji huyo kiasi cha kumfanya Zidane kumwondoa kikosini kwenye mechi za karibuni.

Spurs imeambiwa ikamchukue mchezaji wake huyo iliyemuuza kwa ada iliyovunja rekodi ya dunia mwaka 2013 ya pauni milioni 86. Lyon pia inamtaka Bale kwa mkopo, lakini shida inakuja kwenye kumudu mshahara wa pauni 250,000 kila wiki.

Manchester United ilitajwa kumtaka mchezaji huyo, lakini shida inakuja kama Madrid itakuwa tayari kumpeleka kwa mkopo huko Old Trafford.

Wakala wa Bale, Jonathan Barnett, alisema mchezaji wake ataendelea kubaki Madrid na kwa muda wa mkataba wake uliobaki utamshuhudia akipokea pauni milioni 100 hata kama hatakuwa akicheza.

## ZISIKUPITE

### BARCA, PSG VITANI

BARCELONA na Paris-St Germain, zimetajwa kumwania kiungo mshambuliaji wa Manchester United, Angel Gomes (18), ambaye ni raia wa England. ***(Star)***

### MADRID KUTEMA 14

REAL Madrid inatarajia kuwaacha wachezaji wake 14 ifikapo majira ya joto, baadhi ya nyota hao ni mshambuliaji, Gareth Bale (29), kipa raia wa Costa Rica, Keylor Navas (32) na mshambuliaji wa Colombia, James Rodriguez (27). ***(Marca)***

### ZAHA KUONDOKA PALACE

MSHAMBULIAJI wa Crystal Palace, Wilfried Zaha ameiambia klabu hiyo kuwa anataka kuondoka katika majira ya joto na kwamba anahitaji kutua kwenye timu inayoshiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Klabu hiyo maarufu kama Eagles itahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 80 ili kumruhusu kuondoka nyota huyo raia wa Ivory Coast. ***(Mail)***

### SANCHEZ ANUKIA JUVENTUS

JUVENTUS imeanza mazungumzo na Manchester United kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Chile, Alexis Sanchez, ambaye pia anahusishwa na tetesi za kujiunga na Inter Milan. ***(Independent)***

### UNITED KUIBOMOA PALACE

KLABU ya Manchester United, inajiandaa kutoa kaisi cha pauni milioni 50 ili kuwasajili mabeki wawili wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka (21) raia wa England na Mholanzi Patrick Van Aanholt ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Sun)***

### JAMES KUTUA UNITED

MANCHESTER United, inakaribia kukamilisha mchakato wa kumnasa winga wa Swansea na Wales, Daniel James (21), huku ikihofia kumkosa winga mwingine ambaye waliweka jina lake juu katika orodha ya usajili kutoka Borussia Dortmund, Jadon Sancho (19). ***(London Evening Standard)***

### HIGUAN KUREJEA JUVE

CHELSEA haina mpango wa kumpa mkataba mpya straika, Gonzalo Higuain (31), ambaye yupo klabuni hapo kwa mkopo na inajiandaa kumrejesha Juventus baada ya mechi ya fainali ya Ligi ya Europa. ***(Mail)***

### SARRI TUMBO JOTO

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, bado anahofia kuhusu hatima yake ndani ya Stamford Bridge hata kama atafanikiwa kutwaa taji la Ligi ya Europa League, lakini Roma na AC Milan zikitajwa kumhitaji Mtaliano huyo ambaye nafasi yake hapo darajani inaweza kuchukuliwa na Kocha wa Watford, Javi Gracia. ***(Express)***

### CHELSEA MAMBO BADO

MABOSI wa Chelsea watafanya uamuzi kuhusu hatima ya kibarua cha Sarri klabuni hapo mpaka baada ya kumalizika kwa mechi ya fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Arsenal ambayo itachezwa Mei 29 mwaka huu. ***(Telegraph)***

### LAMPARD APIGIWA CHAPUO

KOCHA wa Derby County, Frank Lampard, ambaye timu yake imetinga fainali za mtoano za Championship, amechaguliwa kurejea klabu yake ya zamani ya Chelsea kurithi mikoba ya Sarri. ***(SportMediaset, via Star)***

HABARI MICHEZO

## Azam FC yawaendea Mtibwa kambini

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Kombe la Kagame, Azam FC ,wameingia kambini jana kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Afisa Habari wa Azam FC, Jaffer Iddi, alisema jana kuwa lengo la kuingia kambini ni kutaka kuona wachezaji wao wanakuwa imara na tayari kusaka pointi tatu muhimu katika mchezo huo wa marudiano.

Iddi alisema kuwa wachezaji wao wote ni wazima na wameahidi kupambana ili kulinda heshima ya klabu baada ya kuondoka kwenye mbio za kuwania ubingwa wa msimu huu.

'Kikosi chetu kimeingia kambini ili kujilinda kukaa sawa, tunataka kujiandaa mapema na kujiweka sawa, tunataka kupata ushindi ili kulinda heshima, tunajua hatuko tena kwenye mbio za ubingwa au kumaliza katika nafasi ya pili," alisema Iddi.

Aliongeza kuwa wanatarajia kutumia mechi hiyo na nyingine dhidi ya Yanga ambayo itakuwa ya kufunga pazia la msimu huu ili kujiandaa na mchezo wao wa fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Lipuli FC itakayochezwa Juni Mosi kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

Azam FC yenye pointi 69 iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara nyuma ya Simba na Yanga ambao ndio wamebakia kwenye mbio za ubingwa.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 34 | 27 | 4 | 3 | 72 | 14 | 85 |
| 2. Yanga | 36 | 26 | 5 | 5 | 55 | 25 | 83 |
| 3. Azam | 36 | 19 | 12 | 5 | 50 | 21 | 69 |
| 4. Kinondoni MC | 36 | 11 | 16 | 9 | 36 | 25 | 49 |
| 5. Mtibwa Sugar | 36 | 14 | 7 | 15 | 36 | 32 | 49 |
| 6. Lipuli | 36 | 12 | 12 | 12 | 30 | 36 | 48 |
| 7. Ndanda | 36 | 12 | 11 | 12 | 23 | 31 | 47 |
| 8.Singida United | 35 | 11 | 12 | 13 | 28 | 35 | 45 |
| 9. Coastal Union | 35 | 10 | 14 | 11 | 31 | 41 | 44 |
| 10. Mbao | 36 | 11 | 11 | 14 | 26 | 38 | 44 |
| 11. Mbeya City | 34 | 12 | 7 | 15 | 35 | 36 | 43 |
| 12. Tanzania Prisons | 36 | 10 | 13 | 13 | 27 | 29 | 43 |
| 13. Kagera Sugar | 35 | 10 | 13 | 12 | 31 | 37 | 43 |
| 14. Ruvu Shooting | 36 | 10 | 12 | 14 | 33 | 41 | 42 |
| 15. Alliance | 35 | 10 | 11 | 14 | 28 | 38 | 41 |
| 16. JKT Tanzania | 36 | 9 | 14 | 13 | 22 | 32 | 41 |
| 17. Stand United | 35 | 11 | 8 | 16 | 33 | 44 | 41 |
| 18. Biashara United | 34 | 10 | 10 | 14 | 26 | 31 | 40 |
| 19. Mwadui | 36 | 10 | 8 | 18 | 38 | 48 | 38 |
| 20. African Lyon | 35 | 4 | 10 | 21 | 21 | 47 | 22 |

# UCHAGUZI MKUU ZFF KUFANYIKA JUNI MOSI

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HATIMAYE Kamati ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), limetangaza kuwa uchaguzi mkuu wa shirikisho hilo utafanyika ifikapo Juni 2 mwaka huu, imeelezwa.

**Viongozi watakaochaguliwa katika uchaguzi huo, watakaa madarakani kwa muda wa miaka minne kama katiba inavyoeleza.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Uchaguzi ya ZFF, Omar Makungu, alisema kuwa wamefikia uamuzi wa kutangaza uchaguzi huo baada ya kupitishwa kwa katiba mpya na kumalizika kwa chaguzi katika mikoa yote mitano ya visiwani hapa.

Makungu alisema kuwa shirikisho hilo litafanya uchaguzi huo kwa kufuata ibara ya 52 (1) (a) (2) ya katiba ya ZFF iliyopitishwa mwaka huu.

Alisema kuwa mchakato wa kutoa fomu kwa ajili ya wagombea ulitarajiwa kuanza jana na utamalizika ifikapo Jumatatu wakati usaili kwa wagombea watakaokuwa wamechukua fomu hizo kwa upande wa Pemba utafanyika ifikapo Mei 21 mwaka huu na siku inayofuata itakuwa ni zamu ya Unguja.

Kiongozi huyo alisema kuwa kati ya Mei 24 hadi 26 kutakuwa ni muda wa kuweka pingamizi na rufaa wakati siku za wagombea kufanya kampeni zitaanza Mei 27 hadi Juni Mosi.

Aliizitaja nafasi zitakazowaniwa katika uchaguzi huo ni pamoja na Rais, Makamu wa Rais na Ujumbe wa Kamati ya Utendaji lakini akaweka wazi sifa mojawapo ya nafasi mbili za juu ni kuwa na elimu ya ngazi ya digrii huku pia uzoefu wa miaka mitano wa kuongoza mpira ukitajwa.

"Kamati ya uchaguzi inapenda kutoa wito kwa wadau wa soka hapa Zanzibar ambao wamekidhi vigezo wajitokeze kwa wingi katika kugombea nafasi hizo kwa ajili ya kuleta maendeleo ya soka visiwani hapa," alisema Makungu.

Kwa mujibu wa katiba ya ZFF iliyopitishwa mapema mwaka huu, ibara ya 20, inataja wapiga kura katika uchaguzi huo ni Mwenyekiti na Katibu wa kila chama cha mkoa huku mjumbe mmoja kutoka katika klabu zote za Ligi Kuu Zanzibar na vyama shiriki ambavyo vimesajiliwa pia watashiriki katika mchakato huo.



Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa nchini, Tarimba Abbas (kushoto), akimkabidhi cheti cha ushirikiano mwema Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia. **PICHA: SPORTPESA**

# *Karia: Sevilla wataipaisha Tanzania*

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema kuwa ujio wa timu ya Sevilla kutoka nchini Hispania chini ya udhamini wa Kampuni ya michezo ya kubahatisha ya SportPesa utaongeza hamasa na maendeleo ya mchezo huo hapa nchini.

TFF pia imewataka wachezaji wa Simba kutumia fursa ya mechi hiyo itakayoonyeshwa na DStv kupitia Supersport 9 kuonyesha vipaji vyao.

Sevilla FC inatarajiwa kuwasili nchini Jumanne na Alhamisi Mei 23 mwaka huu itacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kwenye Uwanja wa Taifa kuanzia saa 1 usiku.

Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema kuwa Sevilla FC ni timu kubwa yenye historia kubwa katika soka duniani na hivyo ujio wao utawavutia mashabiki wa soka hata wa nchi jirani ili kuja kushuhudia wachezaji nyota wa wanaocheza bara la Ulaya.

Karia alisema kuwa ni historia kwa Tanzania kwani tangu mwaka 2017, SportPesa imekuwa ikileta hamasa kubwa kwa mashabiki wa soka, wachezaji, viongozi na makocha kutokana na shughuli mbalimbali za kimichezo zilizofanikishwa na kampuni hiyo.

"Walianza na ujio wa timu ya Everton ambayo ilicheza mechi kwenye Uwanja wa Taifa dhidi ya Gor Mahia ya Kenya. Mastaa kama Wayne Rooney na wengine kibao walicheza kwa mara ya kwanza Tanzania na kuleta hamasa," alisema Karia.

Alifafanua kuwa Sevilla FC ni mabingwa mara nyingi wa michuano ya Europa na ujio wao utaongeza hamasa iliyoanzishwa na Everton hapa nchini.


Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema kuwa wanajivunia kuwa wadau wa kweli wa maendeleo ya soka na kuwaomba mashabiki wa soka kujaa uwanjani kuishangilia Simba.

Tarimba alisema kuwa kwa kuzingatia hilo, wameamua kuanzisha promosheni ya "Usibahatishe Cheza na SportPesa" ambayo mbali ya washindi kuzawadiwa gari aina ya Toyota IST tatu, pia watatoa tiketi 45 ambapo washindi watano watalipiwa usafiri na malazi kuja kuiona mechi hiyo ya Simba dhidi ya Sevilla.

# Michezo

Ijumaa Mei 17, 2019

Nipashe

Bale kuwaaga Madrid Jumapili

HABARI UK.30



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Mtibwa Sugar, Cassian Ponera, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: TFF**

## Yanga kutwaa ubingwa hivi

**Na Somoe Ng'itu**

WAKIWA wamebakiwa na mechi mbili mkononi, uongozi wa Yanga unaamini kuwa timu yao bado ina nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kwa sababu watani zao Simba "pumzi" yao imekata.

Mechi mbili za Yanga zilizobakia msimu huu ni dhidi ya Mbeya City inayotarajiwa kuchezwa Jumatano na ile ya kufunga msimu huu kwa kukutana na Azam FC, mechi zote kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, aliliambia gazeti hili kuwa wanachama na mashabiki wa timu yao wanatakiwa kuwa watulivu kwa sababu kwenye soka lolote linaweza kutokea.

Mwakalebela alisema kuwa licha ya watani zao kuwa na mechi nyingi mkononi, bado hiyo haina maana wanaweza kupata ushindi katika michezo yote.

"Bado hatujakata tamaa, kikubwa tunatakiwa kushinda mechi zetu mbili zilizobaki, mpira ni mchezo wa makosa, lolote linaweza kutokea kwa Simba na hatimaye tukafanikiwa kupata ubingwa," alisema Mwakalebela, Katibu Mkuu wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Alisema kuwa mbali na kutwaa ubingwa, wanahitaji kushinda mechi hizo ili kulinda heshima ya Yanga ambayo imepotea kuanzia msimu uliopita kutokana na changamoto mbalimbali walizopitia.

Mabingwa watetezi, Simba ambao wamecheza mechi 34, wamebakiza michezo dhidi ya Ndanda FC, Singida United, Biashara United na Mtibwa Sugar.

# Simba yarejea kileleni

## ●●● Sasa inahitaji pointi nne kujihakikishia ubingwa wa Ligi Kuu Bara kwa ...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi, Simba, wamefanikiwa kurejea tena kileleni kwa kishindo baada ya kuichapa Mtibwa Sugar mabao 3-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es salaam.

**Mabao ya vinara hao walifungwa na John Bocco, Clatous Chama na Emmanuel Okwi ambayo yaliifanya timu hiyo ifikishe pointi 85, na sasa ikihitaji walau pointi nne tu ili iweze kushinda ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya pili mfululizo.**

Simba ilipata pointi nne, itafikisha pointi 89 sawa na Yanga, lakini Simba ina mtaji wa magoli mengi ya kufunga ikifikisha magoli 72 na kufungwa 14, huku Yanga ikiwa na magoli 55, ikifungwa mabao 25.

Kama Yanga itashinda mechi zote itafikisha pointi 89, na kama ikiwa sawa na Simba inahitaji kufunga magoli zaidi ya 28 kwa mechi mbili ili kutwaa ubingwa huo ambao unatoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wakati Yanga imebakisha mechi mbili dhidi ya Mbeya City na Azam FC, Simba imebakisha michezo minne dhidi ya Ndanda FC, Biashara United, Singida United na Mtibwa Sugar, mechi ya mwisho itakayochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Dakika ya kwanza tu ya mchezo, timu zote zilikosa magoli kila moja, Mtibwa Sugar ilianza kwa Rifat Hamisi kukosa bao la wazi, baada ya uzembe uliofanywa na kiungo wa Simba, Jonas Mkude aliyekuwa karibu na goli na dakika hiyo hiyo, Bocco alikosa bao la wazi, aliposhindwa kuunganisha krosi safi kutoka kwa Mnyarwanda Kagere.

Beki mkongwe wa Mtibwa Sugar, Dickson Daudi aliinyima Simba bao la mapema baada ya kufanikiwa kuokoa mpira kwenye mstari wa goli kufuatia mpira uliopigwa na Kagere ambao ulikuwa unaelekea wavuni dakika ya 23.

Alikuwa ni nahodha wa mabingwa hao na mshambuliaji wa zamani wa Azam FC, Bocco aliyerekebisha makosa yake dakika ya 32 kwa kufunga bao la kwanza baada ya kuitendea haki krosi ya Kagere.

Chama alifunga goli la pili dakika ya 47, baada ya mabeki wa Mtibwa Sugar kutegeana kuokoa mpira, mfungaji akamlamba chenga kipa Shaaban Kado na kuujaza wavuni na kuwafanya mashabiki wa timu hiyo wasahau machungu waliyopata katika michezo miwili iliyopita.

Bao la tatu na kikosi hicho kilichoko chini ya Mbelgiji Patrick Aussems halikutofautiana na la pili, kwani Okwi aliipokea pasi ndefu ambayo mabeki wa Mtibwa Sugar walisimama kucheza mchezo wa kuotea, lakini mfungaji alidokoa mpira, kipa Kado akiwa ametoka golini kujaribu kuukoa mpira huo, akaukosa na hatimaye shuti hilo la Mganda kutinga wavuni.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >